*MAYA* 💃

*SEHEMU YA 01---05*

"dadaaaa!! dadaaaa!!!" mtoto mdogo aitwae Livia alikimbia mbiombio kuelekea nyumbani akiwa ametokea sokoni, alipofika akaingia ndani na kumkuta dada yake yupo jikoni

"kulikoni Livia?" aliulizwa
"soma hapa!" alionyeshwa kikaratasi akakishika na kutazama akaona tangazo

"linahusu nini Livia?"
"aah dada huoni?"
"sijui kusoma mdogo wangu"

"ooh nimesahau dada ni hivi imeandikwa hapa kuwa kuna mashindano ya mpishi bora ambayo yatafanyika kesho na mshindi ataingia kwenye kasri la mfalme yaani atakuwa mjakazi ndani ya kasri la mfalme"

"kweli unayoyasoma ndiyo yaliyoandikwa Livia?!"

"ndiyo dada Maya sasa mimi nikudanganyaje jamani?"

"jamani lazima niende nika...."

"ukafanyaje??" walisikia sauti nyuma ikiuliza kabla hajamaliza sentensi yake, wote wakageuka na kutazama wakamwona shangazi Leti akiwa amesimama na uso wake wa ukali akiwaangalia, Maya na mdogo wake huyo mtoto wa shangazi huyo walitazamana huku Maya akiwa amekishikilia kikaratasi hicho mkononi amekificha kwa nyuma

"hapana mama ni kwamba nilikuwa namwambia dada Maya kuwa tutaenda tutaenda.." Livia alishikwa na kigugumizi akishindwa kuzungumza mbele ya mama yake huyo mkali

"wewe Livia toka nenda kacheze na wewe Maya nini hicho ulichokificha nyuma?"

"sijaficha kitu shangazi"
"kwahiyo mimi sina macho naongea uwongo siyo?"

"kweli shangazi sijaficha kitu" Maya alijibu huku akitikisa kichwa akikanusha katakata akimuhofia shangazi yake huyo mkali asiye na huruma, ambae alimfuata taratibu na kumsogelea kisha akanyoosha mkono wake akikiomba kitu ambacho Maya amekificha nyuma mikononi, na Maya hakuwa na namna akakitoa taratibu kijikaratasi hicho alicholetewa na mdogo wake, Livia, cha tangazo la mashindano ya mapishi

Maya msichana mrembo sana na mzuri alikuwa ni hodari wa mapishi mwenye kipaji cha pekee ambacho amekirithi kutoka kwa marehemu mama yake ambae alikuwa mpishi hodari sana

Shangazi Leti alikichukua na kukisoma akamtazama Maya kwa jicho kali kisha akakichana chana kijikaratasi hicho vipande vipande na kuvitupa chini

"unafikiri unaweza kupika vizuri mpaka uende huko unapotaka kwenda?"
"nataka kwenda kujaribu shangazi"

"kujaribu tu, unadhani nani atakayekupitisha wewe msichana masikini tena usiye na wazazi ambae hata mimi nilikuchukua tu ulivyokuwa mdogo kama msaada tu ili uishi namimi kwa sababu hata marehemu baba yako sina undugu nae wa karibu ni jamaa tu wa mbali mbali na nimekuleta tu ili ufanye kazi siyo uzubae zubae tu, wewe siyo mwanafamilia humu ni mjakazi tu hakikisha unapika chakula kizuri tunakula tunashiba maana ndo kinachokuweka hapa mjini sawa??!!"

"sawa shangazi"

"eeh ndo hivyo sahau kuhusu kitu kinachoitwa kuolewa au kwenda kwenye mashindano yoyote kwanza hata kusoma kwenyewe na kuandika hujui hapo ulipo unadhani nani atakaekukubali au ni mchumba gani atakayekuja kukuchumbia msichana mjinga mjinga kama wewe?" mwanamama Leti alimwambia Maya maneno ya kashfa, msichana huyo akabaki kimya hana cha kujibu mbele ya shangazi yake huyo, muda huohuo binti mkubwa wa mwanamama huyo aitwae Lidia alikuja jikoni na kumkuta mama yake anamsema Maya

"mama kuna wageni" alimwambia mama yake
"wageni gani?"

"sijajua ila wanaonekana ni watu wa maana sana"

"sawa twende" mwanamama huyo alimjibu bintiye na kutoka nae jikoni wakamwacha Maya peke yake, akashusha pumzi ndefu na kujikuna kichwani, akageuka na kuendelea na mapishi akiwaza mengi kichwani mwake

Maya alikuwa hana wazazi wote wawili wamefariki, alitangulia baba yake kisha akafuata mama yake na huku ndugu wakiwa hawampendi wa upande wa baba kwa sababu alihadithiwa kuwa mama yake ndiye aliyekuwa chanzo cha kifo cha baba yake, na Maya hakuwa mtoto wa kumzaa wa baba huyo alimkuta mama yake Maya tayari ana mtoto ambae ni maya alipomuoa, hivyo Maya akachukuliwa na mmoja wa ndugu hawa wa marehemu baba yake huyo (wa kambo) na kufanywa mfanyakazi wa ndani akitumikishwa kama punda kwa kila aina ya kazi kutwa nzima

"karibuni wageni" shangazi Leti aliwakaribisha ndani wanaume wanne, watatu watu wazima na mmoja ni kijana mtanashati, wakiwa wamekuja na gari (la farasi) usafiri mkuu ndani ya nchi hiyo ya karne ya kumi nane (A. D)

"asante sana" mzee mmoja aliyeonekana ni baba mzazi wa kijana huyo aliutikia wakaingia mpaka ndani na kuketi wakionekana wana jambo muhimu wamekuja nalo kwenye nyumba hiyo

"karibuni sana!" shangazi Leti alitabasamu

"asante sisi siyo wakaaji ndani ya nyumba hii tumekuja kwa sababu maalumu tunamuhitaji baba wa mji huu yupo?"

"amepumzika chumbani kwake ngoja nikamwamshe"
"kabla hujamwamsha tunahitaji kujua kwa msichana Ma..." mzee huyo alionekana kusahau jina alilotaka kulitaja

"Maya baba" kijana wake alimsaidia
"eeh Maya samahani limenitoka yupo?" aliwauliza, shangazi Leti na binti yake mkubwa Lidia wakageukiana na kutazamana, Lidia akamkonyeza mama yake

"mh hayupo tangu jana ameondoka" mama huyo alidanganya

"ooh basi sawa mguu huu tumekuja kwa ajili yake maana mtoto wangu amempenda anataka kumuoa" mzee huyo aliongea na kijana wake huyo akatikisa kichwa huku akitabasamu, kitendo hicho kilimuuma Lidia ambae aliumia kimoyo moyo alipoona Maya anakuja kuchumbiwa na kijana huyo mwenye maisha mazuri kwao wazazi wake wakiwa na gari na huku yeye akiwa bado yupo tu nyumbani, akamwacha mama yake anaendelea kuongea na wageni akaenda jikoni alipokuwa Maya anapika, akamkuta anakaangiza huku anaimba imba nyimbo za kujifariji

"wewe punda wewe?"

"abee!" Maya aligeuka kiunyonge akiitwa majina ya ajabu ajabu yote ni kumdhalilisha tu
"umefanya tukio gani huko mjini sijui sokoni ulipotoka?"
"kwanini dada?"

"askari wamekuja nyumbani wanakuulizia Maya!"
"askari??" Maya alishtuka mpaka akaangusha bakuli la mboga alilokuwa amelishika mkononi akitaka kutia mboga, hakuna kitu alichokuwa anakiogopa kwenye maisha yake kama askari, hata akikutana nao sokoni wakiwa wamebeba silaha zao huwakwepa na kuwakimbia

"ndiyo askari kwahiyo usitoke inawezekana kabisa kuna kitu umefanya au wamekufananisha hata kuongea usiongee sawa?!"

"sawa dada" Maya alimuitikia msichana huyo ambae wanalingana tu umri tena akimpita miezi kadhaa ila kwakuwa anaishi kwao nae ni mtumishi alikuwa anamuita dada na kingine ni kutokana tu na tabia njema aliyonayo Maya ya kumweshimu kila mtu

Lidia alirudi mpaka sebuleni alipokuwa mama yake na wageni

"vipi Lidia Maya yupo?"

"hayupo ametoka" Lidia alimjibu mama yake wakikonyezana

"ndiyo kama mlIvyosikia Maya hayupo ametoka halafu kingine hayupo tayari kuolewa kuna mtu anampenda na kuna binti yangu huyu mrembo anaitwa Lidia yeye hana mtu yupo tayari kuolewa" mwanamama Leti alitabasamu huku akimshika begani binti yake huyo...

*MAYA* 💃

*SEHEMU YA 02*

Ndani ya kasri la mfalme Bono, vijana wake watatu mapacha waliofanana, mwanamfalme Piso mkubwa, Teri anayefuata na Adrian wanaitika wito wa baba yao anaowaita kupitia mlinzi wake mkuu jenerali Fidel, wanasogea mbele ya kiti cha enzi cha baba yao na kuinamisha vichwa vyao (salamu ya heshima)

"uishi milele mtukufu mfalme" wanamsalimia wakimwita mfalme ingawa ni baba yao mzazi, mfalme alikohoa kidogo akapewa kitambaa na jenerali Fidel akajifuta kwa sababu anaumwa kwa muda mrefu huku umri wake ukiwa umeenda

"nimewaita hapa nataka jambo moja kwenu nataka kuwaona wakwe zangu, nataka muoe ili muwe na watoto mniletee wajukuu hapa niwabariki kabla sijaenda kwenye makaburi ya baba zangu, nilichelewa kuwazaa ninyi kwa sababu ya matatizo ya uzazi ya mama yenu lakini nakumbuka nina mtoto mahali ambae ni nje ya ninyi, katika kuhangaika kupata uzao nilibahatika kupata mwanamke nje nikampa ujauzito akajifungua mtoto wa kike lakini kwa bahati mbaya sikuwa mfalme wakati huo nilikuwa mwanajeshi tu wa kawaida ingawa nilikuwa ni mwanamfalme kama ninyi, nilijiunga na jeshi kisiri siri ili kuupigania na kuurudisha ufalme alionyang'angwa hayati baba yangu na jenerali wake, sikufanikiwa kumchukua

yule mwanamke wala mtoto wangu kwa sababu ya harakati za vita ila ninajua ni wa kike, sikuwahi kuwaambia kitu kama hiki ila leo ndiyo ninawaambia ninyi ni wanaume tupu lakini kaeni mkijua mna dada yenu ingawa ni kwa mama mwingine..." mfalme Bono akakohoa kidogo kisha akaendelea

"ila hilo siyo jambo nililowaitia, nilichowaitia ni kimoja tu, nataka kuwaona wajukuu kabla sijaondoka kwenye uso wa dunia hii, Piso, Teri, Adrian mnanisikia?"

"ndiyo baba tunakusikia" walijibu kwa pamoja wakiwa wameinamisha vichwa vyao chini

"mnaweza kwenda" aliwaruhusu wakaondoka taratibu mbele ya baba yao kila mmoja

Piso alielekea moja kwa moja bustanini akaenda kukaa akiwaza na kuwazua kuhusu alichokiongea baba yake, Piso akiwa na mchumba tayari anayempenda sana anayeitwa Sethi ambae ni mtoto wa Waziri Mkuu wa nchi hiyo mzee Gonde

Sethi mchumba na mpenzi wa Piso, alikuwa msichana mrembo sana ambae hakuwa tayari kuolewa na Piso kwa wakati huo na kwa sababu zake binafsi jambo ambalo lilimuumiza sana mwanamfalme ambae alihitaji kumuoa msichana huyo waliependana lakini Sethi alimtaka Piso asubiri kwanza

Teri kwa upande wake yeye hupenda sana kuogelea kila wakati, ana mchumba na mpenzi wake ambae ni bintimfalme kutoka nchi jirani lakini Teri hana mpango wa kuoa kwa sababu kwanza hana msichana mmoja ila anao kadhaa yupo anakula ujana kwanza

Upande wa Adrian yeye ndo kabisa hana mpango wa kuoa wala wa kuwa na msichana kabisa kwa wakati huu yeye muda wote ni mtu wa kufanya mazoezi tu ya kupigana kwa mwili na kwa silaha bado hafikirii kabisa kuwa na msichana

Adrian alikuwa na mpango wa kutoka kimya kimya kwa siri ndani ya kasri ili aende msituni akafanye mazoezi binafsi jambo ambalo lilikuwa marufuku kwa mwanamfalme kutoka ndani ya kasri bila ulinzi wowote wa askari, kijana huyo akaamua kuvaa nguo za kike kama mjakazi akajibadili na nywele zake na kujipodoa podoa akijifunika uso kidogo akatoka kimya kimya akipitia dirishani bila mtu kumuona akaenda mpaka kwenye geti kuu la kasri askari wakiwa wamesimama getini na silaha zao

"unakwenda wapi wewe msichana na kwa kibali cha nani?" aliulizwa

"naenda nje nimeagizwa na mwanamfalme Adrian kuna matunda ameniagiza" aliongea kwa kuigiza sauti ya kike tena ile ya kubembelezea

"lete kibali" aliombwa akatoa karatasi ya kibali yenye saini ya mwanamfalme Adrian, askari wakajiridhisha

"nitakusindikiza mimi mrembo"
"hapana nitakusindikiza mimi" askari walianza kubishana kuhusu nani atamsindikiza wote wakipagawa wakijua ni mtoto wa kike kumbe ni mwanamfalme

"mimi nataka unisindikize wewe hapo" alimshika askari mmoja kwa kidole kifuani

"teh teh si umeona mwenyewe mtoto mzuri amenichagua mimi hapa" askari huyo alimcheka mwenzake huyo, akapanda juu ya farasi, mwanamfalme Adrian (aliyejifanya mwanamke) nae akapanda kwa juu nyuma ya askari huyo wakatoka ndani ya kasri huku askari yule mwingine akiwa amechukia sana...

Farasi alitembea taratibu kuelekea nje ya kasri la mfalme, askari akiwa juu ya farasi huyo akicheka cheka huku akigeuka geuka nyuma akimtazama mwanadada huyo aliyedhani ni mjakazi wa ndani ya kasri

"kaka mbona unanitazama sana jamani?" alimwuliza kwa sauti ya kubana kama ya kike

"nimekupenda sana vipi kwani umeolewa au una mchumba?"

"hapana sina naomba simamisha farasi hapo nikojoe tafadhali mkojo umenibana"

"teh teh mrembo mbona unanipa majaribu mie jamani jamani sawa tu!" askari alitangulia kushuka juu ya farasi wakati wakiwa kwenye barabara yenye miti mirefu pembeni, lakini askari huyo aliposhuka tuu ya farasi alishangaa farasi anavutwa nira na kuanza kuuchapa mwendo yeye akiwa chini akaanza kumkimbiza farasi bila mafanikio yoyote

Mwanamfalme Adrian akiwa juu ya farasi huyo aliuchapa mwendo akipandisha njia ya milimani akielekea juu kabisa ili kwenda kutafuta eneo la siri ambalo atajifua vyema kimazoezi na kwa usiri mkubwa, akiwa na kitabu kidogo cha mafunzo ya mazoezi cha siri kutoka nchi ya KUSINI ambacho hakutaka mtu yeyote ajue kama ana kitabu hicho kwa sababu ya uhasama mkubwa walionao baina ya nchi yao na nchi hiyo ya KUSINI uliopelekea vita na kufungiana mipaka ya nchi

Mwanamfalme Adrian alifika mpaka mlimani porini mahali palipotulia asipoonekana mtu akashuka juu ya farasi, kukiwa ni nyika na vichaka kadhaa akashuka juu ya farasi na kutazama kulia na kushoto kisha akatoa kijitabu chake ili aanze mazoezi lakini kabla hajafany chochote

"wrrrrrruuuu!!" farasi aliyekuja nae alilia akiinua miguu ya mbele akageuka na kukimbia mbio mwenyewe

"wewe rudi hapa!" Adrian alimwita farasi huyo akijaribu kumfuata bila mafanikio

"gggggrrrrh!" ndipo aliposikia muungurumo mzito wa sauti ya mnyama pembeni yake uliomfanya mpaka vinyweleo kwenye mwili wake vikamsimama, Adrian kwa hofu huku akitetemeka akageuza shingo na kutoa macho alipokutana na simba dume mwenye njaa akiwa anamtazama, kumbe ndiye aliyefanya farasi akimbie...

"oooh kaka samahani sana kumbe upo kwenye mawindo sikukuona samahani sana" Adrian alicheka cheka akimuongelesha simba huku akirudi kinyume nyume kwa magoti yakigongana na akihisi kubanwa na mkojo ghafla

"ggggrrrhh" simba aliunguruma kwa sauti ya chini akitembea kwa madaha akimfuata Adrian akiwa wala hana haraka

"teh teh kwanini hujamfuata farasi yule mkimbize tu ndugu yangu wala hajafika mbali na ana minofu kuliko hata mimi, tafadhali usinirarue rarue" Adrian alimuongelesha simba huyo ambae wala hakuwa na mdomo wa kujibu haraka akageuka na kuchomoka mbio, simba nae akaanza kumkimbiza kwa kasi isiyokuwa ya kawaida....

*MAYA* 💃

*SEHEMU YA 03*

Maya aliendelea kupika jikoni bila kujua nini kinachoendelea sebuleni maana Shangazi yake Leti na bintiye Lidia walifanya kila walichoweza kuhakikisha binti huyo hapati mchumba kama huyo ambae alikuwa kwao wana uwezo kiuchumi, hatimae wageni waliondoka wakiwa hawajamuona Maya wakiambiwa kuwa hayupo kumbe masikini binti wa watu alikuwepo jikoni ila ni hila tu za mtu na mama yake zimesababisha bahati hiyo ya mtende aliyoipata kupeperuka kama unyoya kwenye upepo

Baba wa nyumba hiyo ambae alikuwa amelala aliamka baada ya kusikia sauti sebuleni kama za wageni ndipo akatoka na kumkuta mkewe mwanamama Leti na binti yao Lidia wakiwa mlangoni na wageni wakiwa wanaondoka wanaishia ishia

"kuna nini?" aliuliza mzee Tando, akimwuliza mkewe
"kulikuwa na wageni tu wamekuja"

"mbona sikuamshwa?"
"niliona nitakusumbua mume wangu"
"wanahitaji nini?"

"walikuwa wamekuja kumuona Maya kijana wao anataka kumuoa ndo Maya amekataa katakata amesema hataki kuolewa na watu masikini kama wao" Lidia alijibu kabla mama yake hajajibu maana aliishiwa uwongo akawa anatafuta uwongo wa kudanganya ikabidi binti yake huyo amsaidie mbele ya baba yake huyo mwenye mengi kwelikweli

"kwahiyo Maya amegoma kuolewa kisa watu masikini haya sasa yeye huyo Maya ni tajiri, mbona yupoyupo tu humu ndani akifanya kazi za ndani, Mayaaaaaa!!" mzee huyo aliita kwa ukali

"abee mjomba" Maya aliitikia jikoni

"njoo hapa haraka mshenzi wewe" "mume wangu taratibu usimuumize msichana huyo" shangazi Leti alijifanya kumuhurumia Maya ambae alikuja mbio mbio akiwa amelishikilia gauni lake refu na kuu kuu

"abee mjomba" alisimama mbele ya mzee huyo ambae alimtazama Maya tangu chini mpaka juu kisha akamtazama tangu juu mpaka chini kisha mzee huyo akasonya

"nionyeshe utajiri ulionao kiasi cha kukataa mchumba kisa masikini?" alimwuliza Maya akabaki anashangaa maana hajui kinachoendelea

"Baba kuna ni... "

"we Maya kelele acha kumjibu mjomba wako"

Shangazi Leti alimkemea Maya akimzuia kwa makusudi asijitetee, mjomba Tando akamtandika msichana huyo kofi zito la usoni kwenye shavu Maya akabaki amejishika shavu akiugulia maumivu asijue hata kosa alilolitenda masikini

"wewe wa kukataa wachumba kwa utajiri gani ulionao eti pumbavu nenda chumbani huko" Maya alifukuzwa akakimbia mbiombio mpaka chumbani kwake na kulala kitandani kifudi fudi akilia peke yake

"Maya!" shangazi yake alimfuata na kusimama mlangoni kwake

"abee shangazi" Maya akajifuta machozi haraka haraka na mafua ambayo hayakawii kumtoka kila anapolia kisha akasimama na kuinamisha uso wake akimsikiliza shangazi yake

"kaa tu" shangazi yake alimwambia akakaa kitandani

"abee shangazi"
"yule kijana aliyekuja leo unamfahamu?" Maya aliulizwa akasita kujibu kisha akaulizwa tena swali hilo hilo

"ndiyo shangazi ninamfahamu"
"anaishi wapi?"
"nakutanaga nae sokoni baba yake ni mmiliki wa maduka mengi pale sokoni"

"najua ndomana nimekuuliza maana nimeshangaa ujio wao hapa, wamefikaje fikaje?"
"sijui hata wamefikaje shangazi inawezekana amenifuata nyuma nyuma akapajua kwetu maana aliniambia amenipenda anataka anioe"

"kijana muhuni sana yule Maya hakufai usidanganywe na utajiri wake wewe jiulize kwanini awaache mabinti wote wenye uwezo wao aje akufuate wewe, anataka akuharibie maisha tu"

"sawa shangazi nimekusikia" Maya alitikisa kichwa
"haya nenda mtoni bondeni kachote maji hakuna maji humu ndani"

"sawa shangazi" Maya aliinuka kitandani na kutoka haraka haraka chumbani akiwa amelishikilia gauni lake refu linalofunika mpaka miguu lakini limechoka sana akiwa na magauni matatu tu ya kuvaa

"nyau mweusi wewe yaani uolewe na kijana wa kutoka familia yenye uwezo wa kifedha halafu binti yangu Lidia abaki nyumbani tu nani kasema, labda kama mimi siyo mama yake msssyuuuu" shangazi Leti alisonya na kutoka taratibu na yeye chumbani mwa mwanadada huyo

Maya ambae kutwa nzima hana muda wa kupumzika hata kidogo alitoka ndani akiwa na mtungi wake wa asili wa kuchotea maji chombo maalumu chenye mkono kilichonakshiwa kwa urembo nje, kikubwa cha kujaa maji, akaondoka kwenda kuchota maji muda mfupi tu baada ya kutoka jikoni kuipikia familia hiyo nzima chakula...

Ndani ya kasri la mfalme mfalme Bono, muda wa chakula umefika, familia ya mfalme inakusanyika mezani, mfalme Bono mwenyewe na mkewe malkia Zilpa na watoto wao, na ndugu wachache wa karibu wa mfalme na malkia waishio ndani ya jumba hilo la mfalme, wajakazi wanahangaika kuandaa kila kitu mezani na chakula kizuri cha hadhi ya juu kinaandaliwa na kuanza kuliwa

"Adrian yupo wapi?" mfalme anauliza wote wanatazamana na kugundua kumbe mwanamfalme Adrian hayupo

"hajaonekana muda mrefu mtukufu mfalme" mjakazi mkuu alijibu

"kamuangalie chumbani kwake" malkia Zilpa alimuagiza mjakazi mkuu ambae kabla hajageuka kutoka mbele ya mfalme aliingia askari mbio mbio

"mtukufu mfalme, mtukufu malkia"
"kuna nini?" malkia Zilpa alimwuliza askari huyo
"mwanamfalme Adrian ametoroka hayupo ndani ya kasri..." aliwaambia wote wakageukiana na kutazamana mezani....

Upande mwingine mwanamfalme Adrian akiwa nyikani mlimani alikuwa anaendelea kumkimbia simba aliyekuwa anamfukuza nyuma akiwa na njaa kweli kweli, Adrian alililikunja mpaka kiunoni vazi lake refu la kike alilolivaa na kulitumia kutorokea ndani ya kasri akiwa hageuki nyuma anachanja mbuga huku akiwa peku peku, viatu vya kike alivyovivaa pia akiwa amevitupa akiona vizito na makucha ya simba yalikuwa yanakaribia kumshika miguuni, akaenda mpaka kwenye korongo akatazama chini na kuona mto mkubwa utwao Selebu akageuka nyuma na kumwona simba anakuja kwa kasi ya kimbunga, Adrian akaona kuliko araruriwe vipande vipande na simba huyo mwenye njaa kali ni bora

hata ajitupe kwenye korongo hilo refu mto mkubwa ukipita chini, anaweza kufa au kupona, akajitupa mzima mzima na simba alipofika akafunga breki kali akitaka kuangukia korongoni akasimama na kutazama chini akakiona kitoweo chake kinaanguka chini korongoni,

"Grrrrrrh grrrh!!" simba alinguruma akisikitika kuukosa mlo wake huo wa mchana akageuka na kuondoka

Maya alifika kwenye mto huo mkubwa uitwao Selebu akiwa na mtungi wake mkubwa wa asili, akachuchumaa pembezoni mwa mto na kuanza kuchota maji taratibu huku akiimba imba nyimbo anazozipenda, alipomaliza kuchota akaubeba mtungi wake huo taratibu na kujiweka kichwani tayari kuondoka lakini kabla hajageuka akaona kitu kikitoka juu na kutumbukia kwenye maji pwaaaaaaa!! Maya akatoa macho kwa hofu akishtuka sana na ndipo alipogeuka kutaka kukimbia kwa bahati mbaya akajikwaa kwenye kisiki kilichojiotea chini, akapepesuka na kushindwa kuuzuia mtungi uliokuwa kichwani mwake ukamteleza na kuanguka chini puuh, ukapasuka vipande vipande maji yakimwagika yote, Maya akabaki

amejiziba mdomo huku ametoa macho

"Nitamweleza nini mimi shangazi jamani uuuwiiii" alijishika kichwa akiwaza jinsi shangazi yake huyo atakachomfanya atakapomwambia kuwa ameuvunja mtungi huo wa maji....

*MAYA* 💃

*SEHEMU YA 04*

Maya alibaki amejishika mdomo baada ya kuangusha mtungi wa maji wa shangazi yake, akajishika na kichwa akiwaza ni jinsi gani shangazi yake atakavyozipokea taarifa hizo za chombo chake cha thamani kuvunjika, msichana wa watu kwa unyonge akainama na kuanza kujaribu kuokota vipande vya mtungi huo akijaribu kuviunganisha na ndipo aliposikia sauti ya mtu akiogelea ndani ya maji Maya akashtuka na kugeuka kutazama ni nani akamuona kijana mmoja akipiga piga mbizi kwenye maji akija nchi kavu akamfuata na kusimama nchi kavu kwa hasira huku akiwa amejishika kiuno

"nakusubiri huku uje kunilipa mtungi wa shangazi yangu maana ni wewe uliyesababisha niuangushe na kuupasua" alimwambia kijana huyo kwa hasira huku akiwa amejishika kiuno chake

"mimi nimekishika hicho kimtungi chako nikakivunja!?" Adrian aliuliza akitoka kwenye maji hayo mengi ya mto kwa kuogelea akanyoosha mkono kwa Maya akiomba msaada avutwe kwa juu, Maya akamtazama kwa sekunde kadhaa akimwacha kijana huyo atape tape kwenye maji kisha akamnyooshea mkono kishingo upande na kumvuta kwa juu akamsukumia nchi kavu

"umekosa sehemu ya kuogelea mpaka uje kuogelea hapa wakati unajua ni sehemu ya watu kuchota maji kwa matumizi ya nyumbani na hairuhusiwi?"

"maji ni maji na naogelea popote pale hakuna wa kunigusa wewe unasemaje, koh koh koh!!" Adrian alikohoa na kutema maji akiwa amekaa chini amelowana maji akiwa na mavazi yake ya kike

"kumbe ni mwanaume hahaha amevaa mavazi ya kike uuuwiiii lazima itakuwa umefumaniwa wewe huko ulipotoka" Maya alimcheka kijana huyo aliyekasirika na kuinuka akamsogelea msichana huyo karibu kabisa wakitazamana uso kwa uso, macho kwa macho

"unanijua mimi ni nani?"
"nachokujua wewe ni kijana uliyekuwa unaogelea kwenye maji basi"

"mimi ni mwanamfalme kuwa na adabu walau kidogo mimi nimetokea ndani ya kasri la mfalme na baba yangu ni mfalme Bono wa nchi hii yote ya TSALA kwahiyo nitakufanya kitu kibaya usipojiangalia wewe msichana" Adrian aliongea kwa hasira akimtolea macho Maya, ambae nae alimsogelea kijana huyo karibu zaidi

"nawewe unanijua mimi ni nani, mimi ni Maya msichana asiyeogopa chochote na kutishwa na chochote kile ninayejiamini na kujikubali hata uwe nani mimi sikuogopi tangu lini mwanamfalme akaja huku kuogelea kwa masikini kama sisi acha kujitapa na kujisifu kwa sifa zisizokuwa za kwako, mwanamfalme yupo kule ndani ya kasri zuri la mfalme akiogelea kwenye bwawa la maji safi na ya baridi yenye maua mazuri ndani yake, mwanamfalme hawezi kuja huku ndani ya mto wa kuogelea kwenye maji ya mto kama haya tunayooga sisi huku wananchi wa kawaida" Maya nae alitiririka

"hivi unajiona wewe ni nani haswa mwanamke wa kunijibu mimi kama hivi?" Adrian alishikwa na hasira akimsagia meno Maya huku akimtazama usoni machoni mwanadada huyo aliyekuwa anamjibu anavyojisikia

"Maya!" mara rafiki yake wa kike aliyekuja mtoni kuchota maji alimwita wakati akiwa amesimama na kijana huyo wanatunishiana misuli

"abee??!" Maya akageuka na kumtazama rafiki yake,

"umesikia taarifa zilizosambaa eti mwanamfalme Adrian amepotea ndani ya kasri la mfalme hajulikani alipo basi maaskari kibao mjini wanamsaka kwa amri ya mfalme" rafiki huyo wa Maya alimwambia ndipo Adrian alipogeuka pembeni asije akagunduliwa na wasichana hao wawili mtu na rafiki yake kuwa yeye ndiye mwanamfalme Adrian anayetafutwa akaanza kuondoka mdogomdogo eneo hilo lakini akiwa na hasira sana na msichana Maya

"mh kumbe mimi sijui mwenzako" Maya alimjibu rafiki yake
"yule mwanamke  ni nani mliyekuwa mnatazamana?"

"hata simjui, na wala siyo mwanamke yule ni mwanaume amevaa nguo za kike, sijui ndo nani eti anasema yeye ndo mwanamfalme sijui alikuwa ananitisha tisha hapa ndo amesababisha mpaka nikavunja mtungi wa shangazi nitajibu nini mimi sijui kwa shangazi mwenzenu aah" Maya alilalamika akikaa chini

"inawezekana ndiye yeye kweli mwanamfalme Maya twende tukamwangalie huenda tukashinda zawadi nono kutoka kwa mfalme iliyotangazwa Maya"

"mh wala siyo yeye angekuwa yeye angevaa mavazi ya kike na huku mabondeni mtoni afuate nini?" Maya alimjibu rafiki yake huyo aliyebaki anamchungulia chungulia kijana huyo kama atamuona lakini hakumuona tena alikuwa ameshaondoka kwenye upeo wa macho yao

"kweli wala siyo yeye" rafiki yake alijibu na akarudi kwa Maya na kuanza kumsaidia kuokota okota vipande vya mtungi uliovunjika wakivikusanya pamoja Maya akiwa amejawa huzuni kwelikweli akiwaza atakavyopokelewa na shangazi yake Leti ambae ni mkali sana..

Mfalme Bono alikuwa ndani ya kasri lake akiwa kwenye baraza kuu ya kifalme akitazama chini maana ni ghorofani, jenerali Fidel mlinzi wake mkuu alimfuata na kuinamisha kichwa chake (salamu ya heshima)

"uishi milele mtukufu mfalme"
"yupo wapi Adrian?"
"bado wanaendelea kumtafuta mtukufu mfalme"
"jua likizama na bado kijana wangu hajapatikana basi jihesabu huna kazi Fidel hautanifaa tena"

"sitaruhusu hilo litokee mtukufu mfalme" jenerali alijibu mfalme akageuka na kutazama upande wa pili

"baba!" mwanamfalme Piso alimuita baba yake
"zungumza Piso sina muda wa kutosha"
"mimi nahisi kama Adrian hajapotea ila ameondoka makusudi ndani ya kasri kwa sababu ya kumfuata msichana wake baada ya wewe kutuita na kutuambia habari za kuoa"

"una uhakika na unachokisema, msichana gani huyo na ni wa hadhi gani unamfahamu, mimi ndiye nitakayewatafutia wasichana wa hadhi yenu, wasichana kutoka familia za kifalme ndiyo mtakaowaoa na siyo vinginevyo"

"neno hilo ninawaambia pia na kulirudia rudia kila siku lakini hakuna anayenielewa ila Teri tu na siyo Piso wala mwenzake Adrian wanadhani wao wana maamuzi ya mwisho kuliko mimi mama yao na wewe baba yao" Mama yake, malkia Zilpa nae alijibu, malkia Zilpa huku akija na kumshika mumewe mfalme Bono begani huku wakimtazama kijana wao huyo kwa pamoja

"lakini baba na mama mimi ninampenda Sethi na ndiye msichana pekee ninayetaka nimuoe"

"Sethi ni binti wa Waziri Mkuu tu na siyo msichana kutoka katika familia ya kifalme hilo halitawezekana hata siku moja" mama yake alimjibu

"neno la mama yako ni neno langu,, sitazungumza tena"

Mfalme aliongea na kuondoka taratibu "msikilize baba yako Piso" malkia Zilpa alimwambia kijana wake huyo akamwacha, Piso akawatazama wazazi wake hao wawili wakati wanaondoka kisha akaupiga ngumi ukuta kwa hasira...

Upande mwingine ndani ya msitu mkubwa wa Tono uliozunguka nchi ya TSALA kwenye pango moja katikati ya ni msitu kijana mmoja akiwa juu ya farasi anafunga breki nje ya pango hilo lililo katikati ya msitu na kushuka juu ya farasi na anaingia mbio mbio ndani ya pango hilo mpaka ndani kabisa kukiwa na taa na mioto ikiwaka kila mahali kukiwa na maharamia wamepiga kambi, waasi na genge la uhalifu lililo na makazi yake ndani ya msitu

"mkuu" alimwita kiongozi wake alipoingia
"kuna habari gani huko utokako?" aliuliza

"mwanamfalme amepotea ndani ya kasri inasadikika ametoroka yupo uraiani"

"habari njema sana hakikisheni mnamtafuta na kumpata kabla hata askari wa mfalme hawajampata"

"sawa mkuu!" walimwitikia na kutawanyika muda huohuo...

*MAYA* 💃

*SEHEMU YA 05*

Maya anaingia nyumbani kwao taratibu na kwa unyonge akiwa hana mtungi mkononi ambao alikwenda nao kuchota maji, na wa kwanza kumuona ni shangazi yake Leti aliyekuwa nje amekaa, Maya akarudi uso akiwa ameinamisha chini huku amevibeba vipande kadhaa vya mtungi huo kwenye gauni lake refu

"maji yako wapi?" shangazi yake alimkata jicho
"samahani shangazi"
"mtungi uko wapi?"
"umepasuka samahani shangazi"
"umepasuka, umepasukaje pasukaje yaani?" mwanamama huyo aliinuka uso ukiwa umembadilika

"niliuangusha kwa bahati mbaya shangazi samahani sana"

"ooh kwahiyo ukaona uniletee hivyo vijipande kwa dharau kabisa ili nichezeshe chezeshe kabisa kama mtoto?"
"hapana shangazi siyo ili uchezeshe ila ni..." kabla Maya hajamalizia sentensi yake alishtukia mvua ya makonde mazito kutoka kwa shangazi yake ikimshukia mwilini

"nimekuvumilia sana lakini nakuua leo naona unanipanda kichwani" shangazi alimwambia akimtwanga makonde mgongoni

"samahani shangazi nisamehe" Maya alilia akafurukuta na kufanikiwa kujichomoa mikononi mwa shangazi yake huyo aliyekuwa akimwangushia kipigo cha mbwa mwizi

"na leo usirudi kabisa hapa nyumbani paka pori mweusi wewe unajua huo mtungi una thamani kiasi gani, hata baba yako angekuwa hai na mama yako wasingeweza kuununua shenzi kabisa wewe, nenda huko unapopajua, ulale huko na ule huko huko ukija hapa kwangu tena nakuua"

Maya aliondoka nyumbani kwao kimya kimya asijue pa kwenda baada ya kutimuliwa na shangazi yake huyo ambae licha ya kumtolea tu maneno makali pia alimshikia gongo kabisa akitaka kumpiga nalo, alichoona Maya ni kwenda sokoni tu kutembea tembea ili jioni ajaribu kurudi kumbembeleza shangazi yake huenda hasira zake zikapungua

Katikati ya mji, kwenye soko kuu ndani ya nchi ya TSALA msafara wa mwanamfalme Piso unapita akiwa ndani ya gari (la farasi) anaenda hekaluni, askari wapatao kumi wakiwa juu ya farasi kila mmoja na silaha mkononi wakiwa wanaulinda msafara huo kulia na kushoto, mbele na nyuma

Mwanamfalme Piso alikuwa amejawa mawazo tele kichwani kutokana na shinikizo la wazazi wake kukataa asimuoe binti wa Waziri Mkuu, Sethi wakitaka aoe binti mfalme kama hadhi yake ilivyo,

Wananchi walikuwa pembeni wakiinamisha vichwa vyao (salamu ya heshima) kila msafara huo ulipopita huku wakiupungia mikono, mara nyingi msafara wa mwanamfalme ukipita basi anapita na zawadi mbalimbali anazozirusha kuwagawia wananchi masikini wanaosimama kandokando ya barabara na wasiojiweza na watoto lakini leo Piso hakufanya hivyo

"mwanamfalme vipi upo sawa?"
msaidizi wake alimwuliza
"nipo sawa"
"haupo sawa naona una mawazo mengi sana"
"geuza gari lipeleke kwa Waziri Mkuu"
"mwanamfalme hilo siyo agizo kutoka kwa mfalme samahani"
"Utanisikiliza au utamsikiliza baba tuliyemwacha ndani ya kasri?"

"lakini mwanamfalme??!"
"fanya ninachokuagiza"

"sawa mwanamfalme" msaidizi wake alijibu kiunyonge akijua tu jinsi ambavyo itakuwa ngumu kwake ikijulikana kuwa amebadili safari ya mwanamfalme kwenda hekaluni na kumpeleka kwa mwanadada Sethi mpenziwe, mtoto wa Waziri Mkuu

Kundi la wahalifu sugu na maharamia, watekaji na wanyang'anyi pia ni wauaji lilikuwa limeshaingia mjini tayari kwa ajili ya kumsaka mwanamfalme Adrian ambae inasemekana amepotea yupo mtaani bila ulinzi wowote ule sasa wakihangaika wampate wamtie mikononi mwao kisha wadai pesa nyingi (kikombozi) kutoka kwenye familia hiyo ya mfalme

Walikuwa wamejigawa watatu watatu wakipita mjini huku wakiwa na silaha (upanga, mishale) wameificha kwenye manguo yao makubwa waliyovaa

Muda huo huo Maya alikuwa ameshaingia mjini, akizunguka zunguka kumtafuta rafiki yake mmoja wa karibu sana ili apate pa kukaa giza likiingia maana alijua usiku huo kwa hasira za shangazi yake asingeweza kulala nyumbani maana siyo mara ya kwanza kwa mwanadada huyo kutimuliwa nyumbani na kulala nje hata kwa makosa madogo tu yanayosameheka

"Maya! Maya!!" kijana Ausi alimwona akiwa juu ya farasi wake, ni yule ambae alikuja nyumbani kwao ili kumchumbia na wazazi wake, Maya akageuka na kumtazama akiwa juu ya farasi sokoni anakagua biashara za wazazi wake, Maya

"Ausi?"
"nilikuja kwenu lakini ulikuwa haupo na umeondoka makusudi kwa ajili hutaki kuolewa kwa sasa" alishuka kwenye farasi wake

"mimi mbona nilikuwepo nyumbani na sijakuona wala?"

"katika wanawake wanaocheza na bahati kwenye maisha yao wewe ni mmojawapo na mara nyingi huwa sijuagi kumbembeleza msichana mimi, wapo wengi sana humu mjini, nikutakie maisha mema Maya" Ausi alijibu huku akitabasamu na kumtazama Maya kwa dharau kisha akageuka na kuondoka, Maya akabaki kinywa wazi akishangaa anachoambiwa

"mimi mbona nilikuwepo nyumbani jamani??!!" alijiuliza na muda huo huo mtandio aliojifunga shingoni kutokana na upepo ukatoka mwilini mwake na kuanza kupaa juu juu Maya akageuka na kuanza kuukimbiza ukiwa juu juu nae akiwa katikati ya umati wa watu sokoni akijitahidi kujichomeka na kupita kwa tabu akiufuata mtandio wake

Mtandio uliruka juu juu na kuingia ndani ya gari la farasi dirishani lililokuwa limembeba mwanamfalme Piso wakati akipita na msafara wake barabarani, mtandio huo ukamfunika usoni mwanamfalme, akautoa na kutazama nje ulipotoka na ndipo Maya bila kuelewa alilifuata gari hilo akachungulia dirishani na askari wakashtuka na kumzingira Maya walipoona amevamia msafara wa mwanamfalme wakamnyooshea mikuki na upanga, Maya akabaki ametoa macho alipojikuta ameuvamia msafara wa mwanamfalme bila kujua, akabaki anatetemeka

"wewe ndiye mwenye mtandio huu!?" aliulizwa

"ndiy...o mwanamfalme... ni wa...ngu" alishikwa na kigugumizi cha ghafla

"chukua mtandio wako, mwacheni tu!" mwanamfalme Piso aliwaambia askari huku akimpa Maya mtandio wake

"asante mtukufu mwanamfalme" Maya alitetemeka
"unaitwa nani jina lako?"
"Maya mtufuku mwanamfalme mtukufuuu samahani" mpaka alichapia akijiiuma uma maneno msichana wa watu

"unaweza kwenda!" Maya aliambiwa lakini kabla hajageuka askari walinzi wawili wa mwanamfalme miongoni mwa walinzi wake kumi waliokuwa bize juu ya farasi wao wamemzunguka, walitandikwa mishale ikitokea nyuma yao, mmoja kisogoni kichwani ukitokea mpaka mbele kwenye paji la uso na mwingine mgongoni ukitokea mpaka kwa mbele kifuani wakaanguka kutoka juu ya farasi mpaka chini

"msafara wa mwanamfalme umevamiwa shambuliaaa!" msaidizi mkuu mwanamfalme alitoa amri, na watu sokoni wakawa wanakimbia ovyo ovyo, kukawa na taharuki kubwa....

Hakikisha umelipia TSH1000 mara moja tu ili uwe member/mwanachama wa kudumu humu

*MAYA* 💃

*SEHEMU YA 06---10*

Taharuki ilitanda mjini, watu wakikimbia kimbia ovyo baada ya msafara wa mwanamfalme Piso kuvamiwa na watu wasiojulikana, askari wawili walinzi wa mwanamfalme walikuwa wameshatandikwa mishale ya kushtukiza (ambush) wapo chini wamepoteza maisha, askari nane waliobaki walikuwa na kazi ya kuhakikisha mwanamfalme haguswi na mashambulizi hayo kutoka kwa kundi hilo la wahalifu

Maya msichana wa watu alibaki amejificha kwa kuegemea kwenye gurudumu (tairi) la chuma la gari hilo la mwanamfalme huku farasi wanne waliokuwa wanaliendesha gari hilo wakivunjwa miguu ili walale chini wasikimbie ovyo na kusababisha hatari zaidi kwa mwanamfalme kama ajali kwa kupinduka kwa gari

Mwanamfalme Piso alichukua upanga wake nae akitaka kutoka akapambane na wavamizi hao ambao walijificha kwenye umati wa watu waliokuwa wakikimbia ovyo ovyo

"mtukufu mwanamfalme hapana usitoke baki humohumo ndani, huku nje ni hatari sana kwa usalama wako" msaidizi wake alimwambia akimzuia kwa mikono asitoke nje

"acha nikapambane mimi sijazoea kufanyiwa kila kitu nipishe" alililazimisha

"ni heri uniue hapa kuliko kukuruhusu utoke nje ya gari na kuhatarisha maisha yako" msaidizi wake aligoma kumpisha mwanamfalme ambae alimtazama mlinzi wake huyo mkuu kisha akatikisa kichwa na kurudisha upanga wake akarudi ndani ya gari, mlinzi wake akarudi kwenye uwanja wa mapambano wakirusha mishale nao wakarushiwa watu wakiwa wameshatawanyika eneo hilo kwa kuhofia maisha yao wakiwa wamesimama kwa mbali

Msaidizi wa mwanamfalme Piso alifanikiwa kumtandika mshale mmoja wa wavamizi hao na kufanikiwa kuzima mashambulizi hayo ambapo wavamizi hao waliamua kukimbia baada ya kuona kundi kubwa la askari likiongezeka, askari wote waliokuwa maeneo jirani na lilipotokea tukio hilo walipigiwa mbiu ya kuhashiria hatari wakaja kuongeza nguvu, kumlinda mwanamfalme Piso

Taharuki ilikwisha, askari wawili wale wale walinzi wa mwanamfalme Piso ndio waliokuwa wamepoteza maisha, wawili wengine wakiwa wamejeruhiwa huku askari sita wakiwa wazima wanaendelea kumzunguka mwanamfalme baada ya kuzima mashambulizi ya wavamizi hao waliotaka kumuua mwanamfalme na kushindwa kufanikisha zoezi lao hilo

Maya alibaki amelala chini akiwa anatetemeka sana, amejikunyata akiwa amefumba macho pale pale nje ya gari (la farasi) la mwanamfalme Piso akijua bado mapambano yanaendelea kumbe yalishamalizika, askari wawili wakamfuata na kumkamata juu juu wakampeleka mpaka mbele ya mwanamfalme Piso aliyekuwa amejawa hasira akiwa ameshuka kwenye gari akitembea tembea na joho lake la kifalme na taji kichwani

"mtukufu mwanamfalme tumemleta huyu msichana" askari walimwambia, wakimsukuma Maya akapiga magoti huku akiogopa na kutetemeka, Piso akainama na kumtazama usoni msichana huyo akimwinua kidevu chake

"wale ni akina nani?" alimwuliza
"siwajui mtukufu mwanamfalme"
"unanitania wewe msichana wakati umetumwa na haohao uuzuge msafara wa mwanamfalme kwa mtandio wako huo ili wafanye waliyoyakusudia halafu unasema huwajui waliokutuma?" msaidizi wa mwanamfalme na mlinzi wake mkuu alimwuliza Maya kwa ukali

"kweli siwajui mimi na wala sijashirikiana nao tafadhali"

"lete upanga" Piso aliomba akapewa upanga na kumwekea mwanadada Maya shingoni, Maya akatoa macho akihisi mkojo unataka kumtoka alipokiona kifo mbele yake kinamnyemelea

"tafadhali mtukufu mwanamfalme usiniue tafadhali maisha yangu yawe juu ya rehema zako mimi mtumwa wako sihusiki na kilichotokea sihusiki na wala siwajui wale siwajui hata kidogo" alitetemeka Maya akilia, machozi na makamasi vikiwa vimeambatana pamoja na jasho likimtoka na kulowesha gauni lake

Mwanamfalme Piso kwa hasira alinyanyua upanga juu na kutaka kuushusha shingoni mwa Maya lakini mkono wake ukazuiwa na msaidizi wake huyo aitwae Desha, kabla haujatua kwenye shingo ya Maya na kukata kichwa chake, akamgeukia msaidizi wake

"Desha kwanini umekuwa mpinzani wa kila jambo nilalolifanya?"

"mtukufu mwanamfalme mara zote ninakupinga katika mambo yasiyo sahihi tu hasa hili la kumuua msichana mbele ya watu hapana litaharibu sifa yako mtukufu mwanamfalme ukashindwa hata kuurithi ufalme baadae"

"nitakusikiliza kwa hili tu" mwanamfalme alirudisha upanga wake akimsikiliza msaidizi wake huyo

"mkamateni huyo dada mwingizeni kwenye gari" Desha aliwaamuru askari wakambeba Maya wakimfunga kamba mikononi na kumpakiza kwenye gari jingine la farasi lililoletwa, sambamba na miili ya askari wawili wale waliopoteza maisha

Maya alijikuta ndani ya gari la askari akiondolewa eneo hilo huku akiangua kilio akiwa chini ya ulinzi mkali wa askari wenye silaha akiwa hajawahi kuwaza kuwa kuna siku anaweza kupatwa na kadhia hiyo

Shangazi Leti alikuwa na bintiye Lidia wamekaa nje ya nyumba yao wakizungumza

"mama njaa inauma kweli yaani" Lidia bintiye alilalamika
"huna mikono nenda kapike chakula"
"mama mimi siwezi kwanza kucha zangu ndefu kapike wewe mama"

"komaaa mimi mfanyakazi wako kwani we mtoto vipi?" shangazi Leti alimkaripia bintiye huyo

"basi mama ungempiga tu Maya usingemfuk...."

"nani aliyenipikia hiki chakula?" mumewe aliuliza alipotoka nje

"mimi hapa mume wangu"
"umepikaje pikaje mbona hakina ladha kama niliyoizoea sikuzote, Maya yupo wapi?"

"amekimbia amenivunjia mtungi wangu sidhani kama atarudi leo"

"pumbavu nimekuruhusu kumpiga na siyo kumfukuza nani atatupikia chakula sasa huyo mtoto wako uliyemlea kimayai mayai au?"

"eeh baba Lidia usimseme binti yak..." kabla shangazi Leti hajamalizia sentensi yake alikuja mtoto wao wa mwisho Livia mbiombio huku akihema

"kuna nini mbona unatushtua?" Lidia alimwuliza mdogo wake huyo aliyeinama huku akihema

"dada Maya amekamatwa na askari alikuwa..." aliwasimulia alichokiona, wote wakatazamana

"mh aendage tu huko hakuna atakayethubutu kwenda akaunganishwe kwenye kesi" shangazi Leti aliongea huku akiingia ndani...

Upande mwingine ndani ya kasri la mfalme, mfalme Bono na mkewe malkia Zilpa walikuwa nje hawana amani baada ya kusikia kuwa mtoto wake Piso ameshambuliwa na ndipo msafara wa mtoto wake huyo uliingia ndani ya kasri yeye na mkewe wakaufuata na Piso akashuka kwenye gari lake (la farasi) taratibu akiwa amejishika begani mkono wake ukiwa umeteguka

"upo salama mwanangu?" mama yake alimkimbilia

"nipo salama mama usijali"
"aliyehusika na hili lazima atalipa mara mia" mfalme aliongea akitikisa kichwa chake na wakati huo huo msichana Maya alishushwa kwenye gari alilopakizwa na askari kama muhalifu,

"Mungu wangu nimeletwa ndani ya kasri la mfalme??" alishangaa
"twende!" alipigwa teke na askari nyuma yake....

*MAYA* 💃

*SEHEMU YA 07*

"mtu yeyote ambae amehusika na uhalifu huu dhidi ya kijana wangu lazima atalipa" mfalme Bono aliongea

"haina haja baba usifikiri unaweza kunifurahisha katika hili, niachie mimi mwenyewe tu" mwanamfalme Piso alimjibu baba yake

"Piso nyamaza unamjibuje baba yako?"
"mwache azungumze anachojisikia maana anajiona kakua sasa ana mamlaka ya kunijibu mimi chochote kile anachojisikia" mfalme alimjibu mkewe

"huyu msichana ni nani?" malkia Zilpa aliuliza baada ya kumwona msichana amefungwa kamba nyuma mikononi anasukumwa na askari kama mwizi

"ni msichana aliyetumwa na watu walionishambulia auzuge msafara wangu ili wapate nafasi ya kunishambulia"

"alipaswa auwawe au akatupwe gerezani na siyo kuuleta huu uchafu hapa nyumbani" mama yake alimwambia

"nimemleta ili nimshughulikie mimi mwenyewe ili nijue hasa ni nani hao waliomtuma anishambulie, kamfungeni kwenye mabanda ya mavi ya nguruwe" aliwaamrisha askari wakamkokota Maya kama mwizi na kwenda kumpeleka msichana huyo wakamtupa mpaka kwenye mabanda ya mavi ya nguruwe na farasi wa wanyama wote wanaofugwa ndani ya kasri la mfalme, mavi hayo yakivundikwa humo ili baadae yaje kuchukuliwa na kutumika kama mbolea kwenye mashamba na bustani za mfalme,

Kulikuwa na mavi mchanganyiko, ya farasi, ya nguruwe, ya ng'ombe na ya kila aina ya mnyama aliyepatikana ndani ya kasri Maya akaangukia kwenye kinyesi kikavu cha wanyama hao na kufungiwa kwa nje kukiwa na madirisha madogo sana, likiwa linapatikana kwa mbali kidogo na jumba la mfalme, bondeni mita kadhaa kutoka kwenye bustani ya mfalme

Mwanamfalme Piso aliingia ndani ya jumba lao akiwa amekunja uso wake amekasirika, na aliyemkasirikia zaidi ni baba yake kwakuwa hataki amuoe binti wa Waziri Mkuu, Ritha ambae ndiye anampenda sana, wazazi wake hao wawili wakitaka amuoe msichana ambae lazima awe ni binti mfalme kutoka nchi fulani ili kulinda hadhi yao na kukuza mahusiano ya familia zao na maslahi ya nchi

"mume wangu msikilize mwanao huoni anavyokukasirikia?"
"upo upande wa watoto wako Zilpa?"

"hapana siyo kwamba nipo upande wa watoto wangu la hasha, lakini sipendi tu mtoto akose amani kwani anataka kumuoa msichana wa kawaida, si mtoto wa waziri mkuu?"

"mwambie Piso akitaka aendelee kuwa na huyo binti mtoto wa Waziri Mkuu mwambie nampa mtihani mmoja nao ni huu"

"mtihani upi huo?" malkia Zilpa alikaa vizuri tayari kumsikiliza mumewe huyo...

Piso aliingia moja kwa moja chumbani kwake akaletewa chakula na mjakazi lakini akakataa kula akajilaza tu chali kitandani na ndugu yake, pacha wake wa pili anayemfuata, Teri alisimama mlangoni akimtazama tu

"pole sana kwa majanga unaonekana una mawazo sana Piso"

"asante nahitaji kupumzika Teri"
"najua lakini inaonekana kinachokuwazisha hasa siyo majanga ya kushambuliwa tu ila ni mapenzi"

"hayakuhusu Teri niache"

"mimi ni ndugu yako nina haki ya kukushauri ni bora ungechagua njia yangu, ungetafuta bintimfalme wa kuoa halafu hao wengine ungeinjoi nao tu kama huyo Ritha kwani ana kitu gani cha tofauti ambacho mwingine hana mbona namwona wa kawaida tu, mambo yangekuwa safi kabisa, mimi nafikiri baba na mama wapo sahihi kabisa, hadhi ya nyumba hii lazima ilindwe na itunzwe kwa gharama yoyote ile" Teri alimwambia ndugu yake

Mwanamfalme Piso alikerwa na kukasirishwa na maneno ya ndugu yake huyo, mwanamfalme Teri, akainuka haraka haraka kwa hasira na kumfuata ndugu yake huyo akamkunja na kumbananisha ukutani

"usije ukathubutu kuzungumza tena upuuzi wowote dhidi ya mchumba wangu na msichana ninayempenda sana,  Ritha, nina hakika nitakukata shingo yako Teri hata kama ni ndugu yangu wa tumbo moja"

"samahani Piso niachie unaniumiza, nachojaribu kufanya mimi ni kukuelekeza tu kama ndugu yako koh koh koh!!" Teri alikohoa kutokana na kukabwa koo na ndugu yake huyo mkubwa aliyemtangulia dakika moja tu kutoka tumboni

"nini kinaendelea hapo?" mama yao, malkia Zilpa alikuwa amesimama mlangoni, Piso akamwachia ndugu yake

"nilikuwa najaribu kumuelimisha Piso lakini hataki ushauri wangu mama badala yake anataka kunipiga"

"unaweza kutupisha Teri tubaki mimi na ndugu yako Piso?"

"sawa mama haina shida" Teri alijibu akimpita mama yake huku akijiweka weka vizuri nguo yake iliyokunjwa kunjwa na kujishika shingo yake akiwa anaugulia maumivu ya kukabwa

"sihitaji kuzungumza na mtu kwa sasa mama nahitaji kuwa mwenyewe tu"

"nachotaka kuzungumza nawewe ni kitu chema tu na ni baba yako aliyeniagiza nije nikuambie"

"kama ni baba sidhani kama kuna kitu cha maana anachoweza kuniambia kwa sasa"

"Piso unaongea nini kuhusu baba yako kuwa na adabu?" mama yake alikuwa mkali

"kama mnataka niwe na adabu basi acheni kuyaingilia maamuzi yangu mama, ninahitaji kuwa na mtu ninayempenda na siyo mnayemtaka ninyi, mimi ni mtu mzima sasa, na ndiyo maana sikutaka kuongea chochote kile naona bado unakuja kunifuata mpaka chumbani kwangu mama imetosha!!" Piso aliongea kwa jazba

"basi Piso basi imetosha, kama unataka kumuoa huyo binti mtoto wa Waziri Mkuu basi fanya hili baba yako analokuambia, ukimfurahisha baba yako basi ndoa yenu itakuwa imepitishwa lakini usipomfurahisha baba yako basi sahau kuhusu kumuoa huyo msichana unayemtaka"

"nikimfurahisha kivipi mama niambie hata sasa hivi nipo tayari kufanya baba analolitaka, lipi, pambano au, aniandalie kama pambano nipigane na yeyote yule, nitamshinda hakika na kumfurahisha baba, hata vitani nipo tayari kwenda mama" Piso alikuwa mpole akimshika mama yake mabegani

"atakapotupikia chakula kizuri sana mimi na baba yako, tukila na kukifurahia hiko chakula tena kiwe cha asili ya nchi hii siyo cha kigeni basi tutatoa baraka zote kwa ajili yenu na kuhakikisha mnafunga ndoa yenu"

"sawa mama nitafurahi sana sana, nitamwambia, nina hakika Sethi atawapikia chakula kizuri sana kitakachowafurahisha na mtakipenda na hamtajuta kumchagua awe mkwe wenu" Piso alimkumbatia mama yake kwa furaha

"unadhani utafanikiwa kwenye hilo, ninamjua vizuri Sethi mtoto wa Waziri Mkuu hana anachojua jikoni hata kimoja, kwa hapa Piso mwanangu umeshashindwa kabisa na mke niliyekuchagulia mimi ndiye atakayekuwa mkeo" malkia Zilpa aliongea kimoyomoyo huku akitabasamu wakati amekumbatiwa na mtoto wake huyo aliyetangulia kutoka tumboni mwake kati ya mapacha watatu alionao

Hatimae usiku uliingia ndani ya nchi ya TSALA na ndani ya kasri la mfalme, Maya alikuwa ndani ya banda la mavi ya wanyama peke yake amefungiwa kama adhabu akiwa hajatia chakula chochote kinywani wala maji....

*MAYA* 💃

*SEHEMU YA 08*

Usiku uliingia ndani ya nchi ya TSALA, mwanamfalme Adrian alikuwa bado yupo nje ya kasri, vikosi kwa vikosi vya askari vikiwa mtaani kumtafuta, chini ya mlinzi mkuu wa mfalme Bono, jenerali Fidel, hakuna kurudi ndani ya kasri la mfalme bila kijana huyo mmojawapo wa vijana watatu mapacha wa mfalme na mkewe malkia Zilpa,

Mwenyewe Adrian alikuwa wala hana habari alikuwa mtaani usiku huo anatembea tu na nguo zake za kike na alipopita kwenye mtaa mmoja mbele barabarani aliona kikosi cha askari kikija akageuka haraka na kujiziba kwa mtandio ulio kwenye vazi lake la kike wasije askari hao wanaomsaka yeye wakamuona na ndipo walipopita wakiwa wanatembea kwa miguu, Adrian akabaki amejibanza kwenye uchochoro mmoja mpaka walipopita akataka kutoka kwenye uchochoro huo lakini akavutwa gauni lake la kike alilovaa

"habari mrembo" jamaa mmoja alimwambia akiwa amemvuta nguo yake, Adrian alipotazama aliona kumbe kuna wahuni wanaendelea na shughuli zao kwenye uchochoro huo aliojibanza, Adrian hakuwajibu kitu

"mlete hapa mtoto mzuri huyo tumshughulikie hapa" jamaa mwingine alimwambia mwenzake na ndipo wakamvuta mguu kutaka kumwangusha, Adrian alipokamatwa mguu mmoja akaurusha wa pili na kumtandika jamaa huyo aliyemshika teke zito la shingoni lililompepesua na kumwangusha, wenzake wakainuka, wakiwa takribani nane

"wewe ni msichana ty au mpelelezi" mmoja alirusha ngumi ikadakwa na Adrian akamchapa jamaa huyo ngumi mfululizo za kwapa akamtegua na kumsukuma kwa wenzake waliokuwa wanakuja wakaanguka nae, kisha Adrian akachomoka na kuanza kukimbia akiwaepuka wasije wakamgundua kuwa yeye ni mwanamfalme

Jamaa hawakumwacha wakaanza kumfuata kwa nyuma akiwakimbia na wao wakimkimbiza, wakampata na kumzunguka

Moja kwa moja wakaanza kumtandika kisawasawa lakini nae akiwatandika mmoja baada ya mwingine, uwezo wa kupambana nao alikuwa nao lakini gauni la kike alilolivaa lilimpa shida kupambana nao na kingine ni kuwa hakutaka wajue kama yeye ni mwanaume tena ni mwanamfalme na pia alikuwa ameshajiongeza make up za kike za kutosha na nywele za kike alizoziiba sokoni, hivyo haikuwa rahisi kumgundua kama yeye ni mwanaume mpaka labda umvue gauni lake la kike na makorokoro aliyokuwa ameyavaa mwilini

Alipoona mambo magumu akawachomoka na kukimbia nao wakaendelea kumkimbiza, Adrian alikona uchochoro mmoja na kutokeza barabarani kwa bahati mbaya akajikuta anaingia kwenye msafara wa kikosi kimoja cha wanaume wa kazi ambao walikuwa wana shughuli moja tu ya kumtafuta mwanamfalme Adrian wamtie mikononi mwao kabla hajarudi ndani ya kasri, msafara huo ukiongozwa na mzee Samba ulisimama kwa kufunga breki ghafla baada ya kuona mtoto wa kike ametokea kwa mbele yao almanusura wamgonge, Adrian akapushiwa na farasi mmoja kwenye msafara huo akaanguka chini na kubiringika mpaka akajigonga kwenye pipa moja, na wale jamaa waliokuwa wanamfukuza

wakatokea na wao wakajikuta wanasimama mbele ya msafara huo

"kuna nini mbele?" mzee Samba aliyekuwa kwenye gari (la farasi) la katikati aliuliza baada ya kuona msafara wake umesimama ghafla ghafla almanusura wapate ajali

"kuna wanaume wanamkimbiza msichana nahisi wanataka wambake nahisi" alijibiwa na msaidizi wake mzee huyo asiyependa purukushani alishuka kwenye gari lake na kwenda mwenyewe kujionea kinachoendelea akawakuta jamaa hao wakimwinua msichana huyo waondoke nae

"mwacheni huyo msichana" msaidizi wake aliwaamrisha wakiwa wamemkamata Adrian, wawili miongoni mwa wale jamaa nane

"wewe kama nani kwanini msipite na yenu" mmoja alijibu, wakiendelea kumwinua Adrian na ndipo aliposhangaa mwenzake akiwa anaanguka chini na nyundo imezama kichwani mwake ikiwa imemtoboa, jamaa akageuka na kukuta yule msaidizi wa mzee Samba yupo nyuma yake

"unaweza kujibu kama ulivyojibu?" msaidizi wa mzee Samba alimwuliza jamaa

Jamaa badala ya kujibu akataka kumrushia ngumi msaidizi huyo wa mzee Samba, akadakwa mkono na kukatwa na shoka begani na mkono wake ukaanguka hapohapo abaki ametoa macho huku damu nyingi zikimtoka, akakimbia huku akilia na wenzake hao wakakimbia walipoona mwenzao huyo amekatwa mkono bila huruma,

"unaitwa nani msichana mzuri?" Adrian aliulizwa na mzee Samba mwenyewe akiwa ametoa macho alipoona tukio hilo

"naitwa Yu....lis alijibu kwa kigugumizi akitunga jina la uwongo

"namtaka huyu msichana mpakizeni kwenye gari"

"sawa mkuu" msaidizi wake alijibu na kumkamata Adrian mkono akimvuta kumpeleka kwenye gari

"wananipeleka wapi hawa watu na wanaenda kunifanyia nini?" Adrian alijiuliza kimoyo moyo na hakukubali kiurahisi hivyo akamng'ata yule jamaa msaidizi wa mzee Samba meno na kuchomoka kwenye mikono yake akaanza kukimbia, msaidizi huyo akachomoa upinde akaweka mshale na kuanza kuuvuta akimlenga Adrian na jamaa huyo akilenga mtu kwa mshale huwaga hakosei shabaha

"mwache tu huyo msichana" mzee Samba alimzuia, jamaa akaurudisha mshale chini na ndipo alipoona kijitabu kidogo alichokiangusha Adrian, jamaa akakitazama na kukifungua kukisoma wakati akirudi kwenye gari na ndipo aliposhtuka na kugundua kuwa kimeandikwa jina la mwanamfalme Adrian na kina saini yake

"mkuu siyo mwanamke yule kumbe ndiye mwanamfalme Adrian" aliwaambia
"unasemaje?" mzee Samba alimwuliza

"tazama kitabu hiki alichokiangusha itakuwa amevaa tu nguo za kike ili asijulikane"

"mnasubiri nini mkimbizeni na muhakikishe mnamkamata akiwa hai" mzee Samba aliwaamrisha wakaanza kumfukuza Adrian ambae wala hakukimbia mbali alikuwa amepanda juu ya mti mmoja amekaa juu akiwachungulia chini wanavyopita kwa kasi ya kimbunga na msafara wao

"oooooooopppps!" Adrian akashusha pumzi ndefu....

.....
......

Kulikucha mapema asubuhi ndani ya nchi ya TSALA, ndani ya jumba la Waziri Mkuu, mzee Gonde, asubuhi asubuhi nje ya geti kukiwa na ulinzi mkali wa kikosi cha askari msafara wa mwanamfalme Piso unawasili na anapokelewa na mzee mama wa Sethi mke wa mzee Gonde na anakaribishwa ndani, Sethi akiwa ndani ya chumba chake anajipodoa na kujipamba ili atoke aende safari zake

"Sethi mchumba wako Piso amekuja" mama yake alimwambia
"nae kafuata nini asubuhi asubuhi?"
"wewe vipi yaani mwanamfalme ametoka ndani ya kasri amekuja kukuona unalalamika wakati mabinti wenzako wanaitamani hiyo nafasi?"

"aah mimi simpendi kivile nipo nae tu kwa ajili yenu"
"hutaki kuwa malkia siku moja uamue maamuzi ya hii nchi au hao unaowapenda akina kajamba nani watakupa nini ambacho hauna na hujawahi kukipata maishani?"

"basi mama yameisha"
"kaongee na mwenzio usikilize kilichomleta" mama yake alimwambia Sethi akamalizia kujipodoa na akatoka mpaka sebuleni akamkuta mwanamfalme Piso anamsubiri amekaa kwenye kochi

"Sethi barafu wa moyo wangu"
"Piso mpenzi wangu" walikumbatiana

"nina habari njema"
"zipi mpenzi"
"leo baba na mama yangu wamekualika kwenye chakula cha mchana"
"waaaoh" Sethi alionyesha furaha ya usoni tu huku akimtazama mama yake aliyekuwa anamfuatilia kwa karibu sana

"sasa wanataka uwapikie chakula kizuri sana cha asili ili waidhinishe ndoa yetu" Piso aliongea kauli iliyombadili uso Sethi akashtuka akimtazama mama yake ambae alimkonyeza aonyeshe tabasamu

"sawa mpenzi wangu"

"haya mchana huu uwe nyumbani mimi naenda kwaheri Sethi kwaheri mama"

"hukai mwanangu?"
"sikai naenda kufanya maandalizi"
Piso alimjibu mama mzazi wa Sethi akatoka haraka haraka akiwa na msaidizi wake na kuwaacha Sethi na mama yake wakitazamana

"mama mbona mtihani huu sasa??"
"mtihani kwelikweli na utapika vinini na mtu mwenyewe hujui kupika chochote hata chai tu kuchemsha huwezi"
mama yake alimjibu....

*MAYA* 💃

*SEHEMU YA 09*

Adrian alipiga miayo na kujigeuza geuza asubuhi akidhani yupo kitandani mwake chumbani, kumbe masikini alikuwa juu ya mti akataka kuanguka chini akashtuka na kulishikilia tawi moja akabaki ananing'inia watu wakimtazama chini kukiwa kumekucha tayari asubuhi na mapema

Akaning'inia na kushuka kwa tabu kumbe usiku mzima alilala juu ya mti huo watu wakimshangaa tu akabaki anaondoka huku ameinamisha uso wake watu wasije wakamgundua kuwa ni mwanamfalme...

Mchana uliingia ndani ya kasri la mfalme, mwanamfalme Adrian akiwa bado hajarudi na askari waliotumwa kufanya msako wa kumtafuta nao wakiendelea na kazi hiyo wakiwa bado hawajarudi kwa mfalme kuleta taarifa yoyote kwa sababu taarifa iliyotakiwa mbele ya mfalme ni moja tu nayo ni mwanamfalme awe amepatikana

Mchana huohuo aliingia kwenye geti kuu la kasri la mfalme mwanadada Sethi, binti wa Waziri Mkuu akiwa amefuatana na mama yake na wajakazi wake na askari wa waziri mkuu wakiwa katika gari maalumu (la farasi) la baba yake Waziri Mkuu, wakapokelewa na mchumba wake, mwanamfalme Piso ambae alikuwa akimsubiri mchumba wake huyo kwa hamu kubwa, wajakazi wa mwanadada huyo walishuka na vyakula walivyovihifadhi vizuri wakiwa nyuma yake wamevibeba wakiingia navyo ndani ya kasri huku Piso akiwa amemshika mwanadada huyo mkono

"naamini hujaniangusha Sethi?"

"siwezi kukuangusha Piso nimewatengenezea wakwe zangu chakula kizuri ambacho naamini watakifurahia na kukipenda sanasana"

"nakuaminia mpenzi wangu" Piso alikishika kiganja cha mwanadada huyo na kukibusu, Sethi akatabasamu huku akitembea kwa mwendo wa madaha na nyuma kukiwa na mama yake na wajakazi waliobeba vyakula hivyo kwenye vyombo maalumu vya dhahabu tayari kuvipeleka kwa mfalme na malkia ili wakale na kutoa maoni kuhusu uzuri wa chakula hicho

Walipoingia ndani ya kasri waliwakuta mfalme Bono na mkewe malkia Zilpa wakiwa sebuleni wameketi kwenye viti vyao vya enzi vya dhahabu huku wakipepewa na wajakazi na kila mmoja akiwa na askari wake aliyesimama upande mmoja kumlinda,

"uishi milele mtukufu mfalme na mtukufu malkia"
"muishi milele mtukufu mfalme na mtukufu malkia" Sethi na mama yake waliinamisha vichwa vyao (salamu ya heshima)

"karibuni sana" malkia Zilpa alitabasamu

"asante mtukufu malkia tumekuja kuleta chakula alichokitengeneza binti yangu kama amri yenu mfalme na malkia watukufu tunaomba mkipokee tafadhali"

"asante sana, mume wangu mtukufu tunaweza kwenda kushiriki sasa chakula cha mkwe wangu mtarajiwa" malkia alitabasamu akimgeukia mfalme huku Piso akimtazama mpenziwe Sethi na kumkomyeza, Sethi akatazama chini kwa aibu

"chakula kakitengeneza nani?" mfalme aliuliza, Sethi akamtazama mama yake lakini akaonyeshwa ishara na mama yake huyo kuwa alijibu swali hilo yeye mwenyewe

"ni mimi mtukufu mfalme"
"lakini nitakuwaje na uhakika kuwa ni wewe uliyekitengeneza chakula hiki wakati kimekuja tu kutoka nyumbani?"

"mume wangu mfalme jamani?" malkia alimshangaa mumewe

"nahitaji kula chakula ambacho kimetengenezwa hapahapa ndani ya nyumba yangu, mpeni vifaa vyote anavyovitaka kwa ajili ya mapishi" mfalme aliongea wajakazi wakamwitikia na kumsogelea Sethi kujua anahitaji nini na nini kwa ajili ya mapishi, Sethi akashusha pumzi ndefu akimtazama mama yake akiwa amejawa na wasiwasi, mama yake akamtazama tu kwa kumuhurumia bintiye huyo

"usijali Sethi mzoee tu baba yangu, ulichokifanya nyumbani ndicho hichohicho kifanye na hapa" Piso alimnong'oneza akatikisa kichwa chake akiingiwa na wasiwasi mwingi

"samahani mtukufu mfalme na mtukufu malkia naweza kujiandaa?"

"ndiyo unaweza kujiandaa unalo lisaa limoja la kufanya hivyo, na hautatakiwa kusaidiwa na mtu yeyote yule utakuwa peke yako jikoni na kila kitu utakachokitaka utawekewa" malkia alimjibu, Sethi akaitikia na kutoka mbele ya mfalme akiwa mnyonge sana akaruhusiwa tu kuongea na mama yake kwa dakika moja tu

"mama ninafanyaje sasa?"
"sijui hata tunafanyaje binti yangu kwani unakumbuka jinsi nilivyokipika hiki chakula tulichokuja nacho hapa kutoka nyumbani, uliniangalia kweli wakati napika?"

"nilikuangalia mama kidogo lakini sijaelewa hata kimoja"

"jitahidi hivyo hivyo binti yangu usiniaibishe mama yako"

"oooppssss" Sethi alishusha pumzi ndefu akaomba kutoka aelekee bustanini akatafakari kidogo, akasindikizwa na mlinzi mpakq bustanini akaachwa maana hapakuwa na mtu akabaki anatembea tembea peke yake akiwaza na kuwazua cha kufanya ili zoezi la kupika lifanikiwe na yeye akiwa hajui kuchemsha hata chai akitembea tembea kandokandi ya bwawa la samaki, lakini hakuna kilichobadilika hakuna alichopata kichwani wala kugundua

Maya alikuwa bado kwenye banda la mavi ya wanyama amefungiwa kwa nje huku njaa na kiu vikimbana kweli kweli maana hakula kitu chochote tangu jana, ikabidi achungulie akitafuta hata wa kumpa maji ya kunywa na ndipo alipomwona mwanadada kwa mbali anatembea tembea kama anawaza jambo linalomsumbua kichwani

"dada samahani dada samahani nisaidie hata kunichotea maji hapo nimebanwa na kiu sana!!" alimwita msichana huyo kupitia kwenye madirisha madogo bila mafanikio

Maya akaamua kuviringisha mavi na kuyafanya kama tonge la ugali kisha akalirusha halikufika mbali akalirusha la pili halikufika mbali akalirusha la tatu likafanikiwa kufika mbali tena likampiga mwanadada Sethi mguuni akashtuka na kuokota kitu alichopigwa nacho

"mh kumbe ni mavi, mshenzi gani huyu kafanya hivi" alililitupa tonge hilo kwa kinyaa na kutazama kwa hasira akaona kitu kama mkono unampungia kwenye mabanda akaamua kwenda kutazama na kweli aligundua ni mkono wa mtu, Maya akafurahi kumuona mwanadada huyo amekuja maana sasa atapata maji ya kunywa angalau hata ya kwenye bwawa la samaki

"samahani dada habari yako mimi nimefungiwa humu nisaidie maji kunichotea ya kwenye bwawa ninywe"

"unathubutuje kunipiga na mavi wewe mjinga nini unanijua mimi vizuri?"
"sikuwa na namna samahani dadangu"
"sina muda wa kupoteza kwako nina kazi ya kumpikia mfalme na malkia chakula cha asili inanichanganya nawewe usinichanganye na ujinga wako" aligeuka akipiga hatua kuondoka

"naweza kukusaidia kupika hicho chakula kama utahitaji msaada wangu" Maya alimwambia Sethi aliyekuwa amepiga hatua kadhaa akitaka kuondoka, akasimama na kugeuka akamtazama Maya bandani, kisha akarudi kumfuata

"una uhakika na unachokisema?"
"ndiyo nina uhakika
"hapana mtu mchafu kama wewe utanielekeza nini wewe?" aligeuka kutaka kuondoka
"naitwa Maya, mama yangu wakati nikiwa mdogo sana aliwahi kuwa mpishi mkuu wa mfalme wa wakatu huo" Maya aliongea kauli ambayo ilimfanya Sethi ageuke tena na kumtazama

"vipi kama unachoniambia hakitafanikiwa?"
"basi nitakuwa mtumishi wako maisha yangu yote bila malipo yoyote, nawewe ninachokitaka kwako nitakapokuelekeza ukafanikiwa unipe maji ya kunywa na unisaidie kutoka humu ndani"

"vizuri naishika ahadi yangu"
"naishika ahadi yangu pia" Maya na mwanadada huyo waliapizana huku wakitazamana uso kwa uso .....

*MAYA*💃

*SEHEMU YA 10*

Mwanadada mrembo Sethi alibaki akitazamana na mwanadada aliyekuwa ndani ya banda la mavi ya wanyama,

"sasa unanielekezaje nawewe upo humu?"

"tafuta cha kuandikia" Maya alimjibu mwanadada huyo ambae aliangaza angaza kulia na kushoto akaona unyoya wa ndege ambao wanatumia kuandikia akaufuata na akachovya kwenye utomvu kisha akaja na kulibinua gauni lake kwa ndani, akaanza kuandika maelekezo yote aliyoambiwa na Maya ambae ana kipaji kikubwa cha upishi, anaweza kupika kwa kichwa tu na kuivisha na kujua kiasi cha chumvi na utamu utakavyokuwa kabla hata hajaingia jikoni kabisa

"ndiyi haya mahitaji na njia?"
"ndiyo hayo"

"una uhakika yatafanya kazi na chakula kitakuwa kitamu?"
"nenda kapike halafu utaniambia"

"basi sawa"
"nisaidie maji ninywe" Maya alimwambia mwanadada huyo ambae alitikisa tu kichwa na kuondoka taratibu na wala hakujali kuhusu maji aliyoombwa na Maya akapitiliza moja kwa moja mpaka ndani ya kasri wakati akipandisha ngazi kuingia ndani mama yake alimfuata

"ulikuwa unafanya nini muda wote huo Sethi?"

"wewe mama subiri utaona mambo makubwa nitakayoyafanya" alimjibu mama yake na akampita Piso aliyekuwa amesimama pembeni akamtazama kwa tabasamu wakati akiingia ndani akiwa anasindikizwa na askari mmoja na wajakazi wawili maalumu ambao atawatuma chochote ambacho kitapungua katika mahitaji yake

Sethi aliingia jikoni akakuta kila kitu kimeandaliwa tayari yaani mahitaji yake yote anayoyataka yamewekwa, akiwa na wajakazi wawili na askari akiwa amesimama mlangoni anatazama kuhakikisha hakuna njia yoyote ya mkato mpishi atakayotumia kama kusaidiwa na kuelekezwa chochote na mtu yeyote yule

"sihitaji usaidizi wenu ninaweza kuyafanya yote mnaweza kwenda" aliwaambia wale wajakazi ambao waliinamisha vichwa vyao na kutoka jikoni wakimwacha yeye mwenyewe na askari wa kumlinda aliyebaki amesimama mlangoni tangu mwanzo mpaka mwisho wa mapishi

Sethi akalifunua gauni lake refu na kuanza kusoma hatua za upishi kiasi na vipimo alivyoelekezwa na mwanadada Maya, na akaanza kuvifuatisha kimoja baada ya kingine

Masaa mawili yalikatika, mfalme Bono akiwa na mkewe malkia Zilpa walikuwa mezani wamekaa kwenye meza ya chakula wakisubiri mapishi ya mkwe wao mtarajiwa wayaonje ikibidi na kula kabisa kama kitakuwa chakula kitamu, mama wa Sethi yaani mke wa Waziri Mkuu alikuwa mezani hapo hapo akiwa anachezea chezea vidole vyake kwa wasiwasi mkubwa akimuwaza bintiye ambae yupo jikoni anapika chakula maana bintiye huyo anamjua tangu mtoto alivyomlea yeye mwenyewe 'kimayai mayai' akishindwa kumfundisha hata kupika chai, akijiandaa kwa aibu itakayompata muda si mrefu

Mwanamfalme Piso hakuweza kukaa muda wote alibaki amesimama akitembea tembea kulia na kushoto, kushoto na kulia huku akijikuna kichwa akiwa anatamani kujua mustakabali wa mpenziwe Sethi kuhusu chakula atakachokipika kama kitamfurahisha baba yake na mama yake na wakamkubalia nia yake ya kumuoa mwanadada huyo anayempenda sana

Ndipo taratibu wakamwona Sethi akija na nyuma yake wajakazi wamebeba vyakula alivyoviandaa, Piso akabaki amekodoa macho akimtazama na mama yake akasimama, mwanadada huyo akafika mpaka mbele ya meza ya mfalme na malkia na kuinamisha uso wake huku akimtazama mama yake kwa tabasamu usoni akimtoa mashaka aliyonayo juu yake

"mtukufu mfalme, mtukufu malkia, kazi mliyonituma nimeimaliza tayari karibuni chakula" aliongea huku chakula kikitengwa mezani

"asante sana Sethi"

"nitawanawisha mimi mwenyewe mikono leo" Sethi alilipokea bakuli na birika la dhahabu la kunawia mikono mfalme na malkia kutoka kwa mjakazi mkuu akaanza kuwanawisha wazazi hao wawili wa mpenziwe Piso, Piso mwenyewe akiwa pembeni amesimama tu anatazama wasiwasi ukiwa umemuanza akiweka weka taji yake ya kifalme vizuri kichwani akiona kama inamlegea legea

Mfalme na malkia walinawa na malkia Zilpa akawa wa kwanza kuonja chakula alichokitia kidogo kwenye sahani yake, akaonja vyote, kukipita ukimya, Sethi na mama yake na Piso na mjakazi mkuu wakiwa wanatazama wakiwa wametulia tuli, Sethi mapigo ya moyo yakimuenda mbio huku akimtazama mama yake ambae alishusha pumzi ndefu ya wasiwasi

"mhmh" malkia Zilpa aliguna huku akitikisa kichwa chake

"vipi mama chakula kipoje?" Piso alimsogelea mama yake huyo ambae alitabasamu na kumtazama mumewe aonje nae, mfalme akaonja cha kwanza, mboga mboga na kutulia tuli akitafuna na kumeza wote wakimtazama na kusubiria atakachosema

"unaweza kuniongezea zaidi mke wangu" mfalme aliongea kauli iliyomfanya Sethi afurahi na Piso aruke ruke na kumkumbatia mchumba wake huyo, mama Sethi akafurahi na kushusha pumzi ndefu

"chakula kitamu sanasana sijawahi kuona, hongera sana Sethi" malkia alimpongeza

"asante mama mtukufu malkia"

"karibuni na ninyi muonje chakula kitamu sana sasa Piso unaweza kumuoa huyu msichana ameshinda mtihani wangu niliompa" mtukufu mfalme aliongea huku akiongezewa chakula hicho

Sethi alimtazama mama yake ambae alifurahi lakini alionekana ana wasiwasi na maswali mengi kuhusu bintiye huyo,  wakaungana wote kula chakula hicho mezani

Baada ya kula chakula cha pamoja Sethi pamoja na mama yake waliaga na kuanza kutoka ndanj ya kasri wakisindikizwa na mwanamfalme Piso na mama yake malkia ambae aliishia kwenye ngazi tu za baraza kuu mpaka karibu na geti kuu

"Piso samahani"
"bila samahani mpenzi wangu"

"kuna msichana nimemuona kwenye mabanda ya mavi ya wanyama kule amefanya nini kwani?"
"yule msichana amesababisha mimi nivamiwe alitumwa na washambuliaji"

"ohoo sawa" Sethi aliitikia akitikisa kichwa chake

Upande mwingine Maya alibaki ametulia tu kiu cha maji kikimbana na njaa kali akiwa amejiziba kwa kitambaa alichokikata kwenye gauni lake puani na mdomoni, Sethi aliyemuomba maji hajarudi na amesahau hata kumpa maji akijisikia mwili unapoteza nguvu na anataka kuzimia kwa kiu na ndipo aliposikia mlango wq banda hilo kubwa ukifunguliwa na askari

"wewe msichana njoo nje" aliitwa akainuka taratibu huku akipepesuka kutokana na njaa akamfuata askari huyo

"samahani naomba maji ninywe hata haya ya kwenye bwawa"
"maji utakunywa kwenu kwa sababu umeachiliwa huru usiwe msumbufu nitakurudisha tena Bandani?" askari alimjibu Maya akawa mpole akisindikizwa na askari huyo pamoja na askari wengine watatu mpaka kwenye geti kuu na ni wakati huohuo mwanamfalme Adrian alikuwa amerudi akiwa amekamatwa na askari waliompata mjini wakapishana na Maya aliyekuwa akitoka macho yao yakagongana

"huyu si ndiye yule kijana wa mtoni kule, kumbe ni mwanamfalme kweli??" Maya alishtuka alipomwona Adrian yupo juu ya farasi na mavazi ya kifalme lakini akiwa amefungwa kamba mikononi

"huyu si ndo yule msichana niliyekutana nae mtoni kule akanijijibu ovyo ovyo, amefuata nini humu ndani?" Adrian nae alijiuliza kimoyo moyo wakati wakipishana....

*Halopesa 0626363334 jina Neema, Tsh1000 kama hujalipia, lipia leo mwisho saa sita usiku*
*MAYA* 💃

*SEHEMU YA 11---15*

Macho ya mwanamfalme Adrian na msichana Maya yaligongana wakatazamana wakati wakipishana, Adrian hakukubali apishane na msichana huyo aliyemwonyesha dharau hivihivi,

"simama!" aliwaamuru askari wasimamishe msafara huo ulipokuwa ukiingia getini ndani ya kasri na ukasimama, Maya nae akasimama na kuinamisha uso wake chini akiona aibu mbele ya kijana huyo aliyemkoromea mtoni bila kujua ni mwanamfalme, lakini kilimuuma sana kuvunjika kwa mtungi wa shangazi yake na ujeuri wa kijana huyo hivyo Maya hakutaka kuonyesha unyonge mbele ya mwanaume hasa mkorofi korofi kama aina ya Adrian ambao hata wafanye makosa vipi, neno 'samahani' kwao ni mwiko kulitamka

Adrian alishuka juu ya farasi akiwa amefungwa kamba mikononi na kumsogelea Maya karibu

"uishi milele mtukufu mwanamfalme" Maya alijibu kiuwoga uwoga akijua hatimae siku ya kiama chake imeshafika, hakujua masikini kuwa anayebishana nae ni mwanamfalme yaani mtoto wa mkuu wa nchi

"ni wewe au ni mwingine ninayemuona humu ndani ya kasri letu?"

"samahani mtukufu mwanamfalme"

"ametoka kufanya nini huyu huyu kichaa ndani ya jumba letu?" aliwauliza askari

"alikuja kwa amri ya mwanamfalme Piso mtukufu Adrian"
"na sasa anapelekwa wapi?"

"ameachiliwa na tumeamriwa tumrudishe uraiani mtukufu mwanamfalme"

"ooh basi kama ametoka kutumikia adhabu humu ndani basi na mimi ninamwongezea adhabu mara mbili, arudi ndani, anajua mwenyewe alichonifanyia"

"sawa mtukufu mwanamfalme" askari walimjibu Maya ambae alikuwa kimya tu akageuzwa na kurudishwa ndani mpaka kulekule kwenye mabanda ya mavi ya wanyama tena akasukumwa ndani na kufungiwa kwa nje

Mwanamfalme Adrian akiwa amefungwa kamba mikononi alifikishwa mpaka mbele ya baba yake kwenye sebule kuu akafunguliwa kamba mikononi

"ulikuwa wapi?"
"nilikuwa mjini baba"
"kwanini unapenda kufanya uamuzi wa kijinga jinga, unajijua wewe ni nani na unatakiwa uishije, ulikosa eneo ndani ya kasri au ulishindwa kuomba ulinzi mpaka uondoke mwenyewe na kuhatarisha maisha yako bila sababu yoyote ya maana?"

"nina uhuru wangu baba kuna wakati sihitaji kufuatwa fuatwa kila mahali natamani niwe mwenyewe nijichunge mwenyewe nifanye mambo yangu kwa uhuru"

"usimjibu baba yako hivyo funga mdomo wako Adrian" mama yake aliyekuwa nyuma alimkaripia

"mwache tu azungumze maana amezaliwa kwenye familia ya kifalme lakini anayatamani maisha ya kimasikini sasa, usingezaliwa kwenye familia hii ungechagua kuzaliwa kwenye familia ya aina hiyo unayoitaka pumbavu sana"

"baba Adrian usimalize maneno yote"

"askari mtoeni huyu mpelekeni kwenye banda la mavi ya wanyama akalale huko siku nzima msimpe chakula wala maji" mfalme alitoa amri askari wakaja mbio mbio na kumkamata Adrian

"baba Adrian usimfanyie hivyo mtoto wako utampelekaje mahali pachafu pasipo na hadhi yake"

"neno langu likitoka halirudi kinywani" mfalme alimjibu mkewe na askari wakatoka wakiwa wamemshika kijana Adrian wakashuka nae mpaka bondeni mpaka kwenye mabanda ya mavi ya wanyama yanayotunzwa kwa ajili ya mbolea, wakalifungua banda kuu na kumwingiza Adrian humo taratibu bila kumbughudhi wala kumsukuma kisha wakamwomba radhi na kufunga mlango kwa nje

Maya alikuwa ameegemea nguzo moja ya mti akiwa anasinzia na ndipo aliposikia miguu inatembea 'kwacha kwacha' akashtuka na kukurupuka usingizini na ndipo aliposhangaa kumwona mwanamfalme Adrian ndani ya banda

"Wewe unafanya nini humu!??"
"unafanya nini humu wewe?" walijikuta wote wakiulizana kwa pamoja wakagongana kwenye kusema kisha kila mmoja akabaki kimya akitazama upande wake

"usifikiri nimekuja humu nitakaa sana kama wewe lakini siyo nitaondoka muda si mrefu"

Maya aliambiwa hakujibu kitu akabaki ameinamisha uso wake chini kwa woga, hapo awali alikuwa akijiziba pua lakini sasa harufu ya kinyesi cha wanyama hao mchanganyiko alishaanza kuizoea lakini Adrian kwake ukawa mtihani kwa sababu hajazoea maisha ya kusikia harufu mbaya mbaya akawa anahangaika kujiziba pua huku akipiga piga chafya na kukohoa

Tangu asubuhi mpaka mchana Adrian hakutulia alikuwa akiinuka na kukaa, akitembea na kusimama, akijikuna kidevu akijikuna kichwa na njaa ikaanza kumuuma kwa sababu tangu asubuhi aliporudi ndani ya kasri hakutia kitu chochote kinywani, wakati Maya njaa ilimkong'ota tangu jana mpaka ameizoea sasa na kiu juu

Adrian alizunguka zunguka na kuchungulia chungulia mwishoni akachoka na kukaa tuli chini akiegemea nguzo yake na yeye usingizi wa uchovu na njaa ukimnyemelea,

Maya alimgeukia kijana huyo na mara akamuona nge mkubwa amempanda mgongoni, tena nge mwenye sumu kali, Maya akanyata kimya kimya maana angemshtua tu Adrian akakurupuka basi nge huyo asiyependa mitikisiko angemuuma mwanamfalme na kumwingizia sumu ambayo ingeweza kumpotezea maisha yake

Alinyata na kumtandika Adrian kofi zito la mgongoni ambalo lilimwingia kisawa sawa kijana huyo akatoa macho na kumgeukia Maya kwa hasira akamzaba kofi zito shavuni lililomwingia kisawa sawa, Maya akabaki amejishika shavu la kulia akiugulia maumivu

"wakati mwingine usijaribu kunizoea" alimuonya Maya

"samahani mtukufu mwanamfalme" Maya alinyong'onyea na kukaa chini akiwa amevimba shavu baada ya kuzabwa kofi zito na kijana huyo

Adrian alirudi kukaa akiwa na hasira, njaa, kiu na uchovu juu kisha akageuka kumtazama Maya kwa hasira akimchukia kwa kitendo alichokifanya cha kumtandika kofi la mgongoni na ndipo macho yake yalipomwona nge mkubwa wa kijani akiwa ameuawa pale alipokuwa amekaa awali na kuzabwa kofi zito, akagundua kumbe msichana huyo alikuwa anamuua nge aliyemdandia mgongoni mwake, Adrian akataka amfuate amuongeleshe Maya amshukuru lakini akasita na kukaza uso wake vilevile

"mwanamfalme Adrian chakula hiki nimekuletea" ilisikika minong'ono dirishani Adrian akainuka haraka haraka na kuchungulia akamwona mjakazi mmojawapo ndani ya kasri lao, mwanadada mnene sana aitwae Lela akiwa amebeba sahani ya chakula na maji

"asante sana Lela hakuna aliyekuona, amekutuma nani mama?" aliipokea sahani hiyo ya chakula na maji
"hapana nimekuandalia mimi mwenyewe na hakuna aliyeniona kula mwanamfalme siwezi kuvumilia kukuona ukishinda na njaa" Lela alicheka cheka huku akijing'ata vidole mwanadada huyo mjakazi akiwa anampenda sana mwanamfalme Adrian ingawa hajawahi kumtamkia

"hakuna sahani ya chakula kingine huko?"
"kwa ajili ya nani Adrian jamani?" Lela aliuliza
"kwa ajili ya rafiki yangu huyu niliyenae huku ndani" Adrian alimjibu Lela ambae alikuwa akicheka cheka na mara ghafla tabasamu lake likapotea ghafla alipochungulia na kumwona msichana Maya amefungiwa ndani pamoja na mwanamfalme Adrian....

*MAYA* 💃

*SEHEMU YA 12*

Mwanamfalme Adrian alikipokea chakula hicho na kumshukuru Lela kwa kumpa chakula hicho na maji na Lela akaondoka akiwa amenyong'onyea baada ya kugundua kuwa kumbe mwanamfalme hakuwa peke yake ndani ya banda hilo la mavi ya wanyama ila alikuwa na msichana aliyekuwa amefungiwa nae

"Lela mbona umenuna na umetoka kumpa mpenzi chakula!?" mjakazi mwenzake ambae ni rafiki yake wa karibu alimwuliza alipomuona

"aaah niliyoyakuta mule kwenye mabanda alimofungiwa mwanamfalme Adrian kipenzi changu siyo mazuri"

"Yapi hayo?"
"si kuna sijui msichana gani sijui wamefungiwa pamoja nakosa amani mwenzako sijui hata wanafanyaga nini mule wakiwa peke yao"

"mh jamani we nawe Lela kuwa na amani yule mdada si alifungwaga na mwanamfalme Piso kipenzi changu mie na akaachiliwa sasa sijui amerudije tena mule?"

"mnazungumza nini?" walisikia sauti ikiwauliza, walipogeuka wakamwona malkia Zilpa akiwatazama

"ooh samahani mtukufu malkia tulikuwa tunaongea tu kuhusu mapishi namuelekeza teh teh" Lela alijichekesha wote yeye na mwenzake wakaondoka taratibu kila mtu njia yake wakiwa wameinamisha vichwa vyao chini

"mnawataja taja watoto wangu wanawahusu nini wajinga sana nyie wasichana" malkia Zilpa alisonya akapita akielekea nae kwenye mabanda ya vinyesi cha wanyama kwenda kumtazama mtoto wake Adrian kama yupo salama

Ndani ya banda kubwa Adrian alikuwa ameshika sahani ya chakula mkononi akamtazama Maya aliyekuwa amegeukia upande mwingine akiwa amejiinamia amejishika shavu akiugulia kofi zito alilozabwa na kijana huyo dakika chache zilizopita

"karibu chakula"
"sihitaji"

"Karibu uonje kidogo inaonekana una njaa sana" alimwambia tena, Maya akamgeukia na kumtazama kijana huyo akatikisa kichwa chake kutokukubaliana na ombi hilo, Adrian alipomtazama Maya akamwona usoni amevimba amekuwa mwekundu shavuni, halafu kutokana na kujishika shavuni kwa mikono iliyokuwa michafu alikuwa amejichafua usoni, Adrian akachana kijipande cha nguo yake na kukichovya kwenye maji aliyoletewa ya kunywa akakikamua na kusogeza kwenye uso wa Maya ambae hakumruhusu afanye hivyo akaushika mkono wake asimguse

"mwanamfalme samahani hupaswi kunigusa"
"nataka nikusafishe nilipokuumiza"

"haina haja nipo sawa"
"mimi ndiye naona palivyovimba najisikia vibaya naomba nipahudumie wala sitapagusa kwa mkono wangu isipokuwa kwa kitambaa tu hiki cha nguo yangu"

"hapana siwezi"
"basi nakuomba ufanye kazi hiyo wewe mwenyewe kama hutaki mimi nikufanyie"

"sawa" Maya aliitikia na kukipokea kitambaa kile cha Adrian alichokichana kwenye nguo yake akaanza kujifuta mwenyewe huku akichovya kwenye glasi ya maji hayo ambayo yalikuwa ya moto aliyoletewa Adrian kwa sababu hakula kitu tangu asubuhi ili ashtue tumbo kwanza kabla ya kula chakula

"na upande huu umesahau" Adrian alimwonyesha kwa kidole akimgusa Maya shavuni

"unanitonesha si nimekuambia usinguse wewe, samahani mwanamfalme nilikuwa namaanisha hivyo"

"Samahani Mau..."

"Maya"
"ooh Maya sawa nimelishika sasa jina lako" Adrian aliitikia

Malkia Zilpa alikuwa ameshafika nje anawachungulia tu dirishani wawili hao wanachokifanya ndani

"Adrian nini kinachoendelea?" aliita, Adrian akageuka na kutazama akamwona mama yake anachungulia dirishani

"mama!" alishusha bilauri ya maji chini akainuka kutaka kuondoka kwenda kuongea na mama yake kwa bahati mbaya hakuuona mwiba

"mwanamfalme!!" Maya alikiona kisiki hicho kilichotaka kumchoma mwanamfalme akategesha mguu mkono wake akitaka kuutoa lakini akachelewa, mguu wa Adrian uliokuwa peku peku ukamkanyaga yeye mkononi na mwiba huo ukamchoma Maya mwenyewe mkononi

"Maya!!" mwanamfalme akamtazama na kumshika mkono mwanadada huyo akaona mkono wake kwenye kiganja unavuja damu

"Adrian si nimekuita mwache huyo msichana mchafu mchafu na masikini na muhalifu kwani nini kinaendelea humo ndani??" mama yake alimkaripia kwa ukali

"ameumia mama anavuja damu"
"kwahiyo??"
"akapate matibabu tafadhali"
"Nipo sawa tu mwanamfalme"

"hauko sawa Maya, mama nisaidie kuita askari wampeleke akatibiwe mkono wake ameumia"

"hivi Adrian unajua kilichonileta mimi huku?"

"samahani mama unaweza kunisaidia kwa hili kwanza halafu tukazungumza" Adrian alimwambia mama yake ambae alitikisa kichwa chake kumsikitikia kijana wake huyo kisha akaita askari wakaja na kuingia ndani na kumtoa Maya wakaondoka nae kwa ajili ya matibabu

"kwanini hutaki kumsikiliza baba yako Adrian na unakua mkaidi?"
"mama mimi siyo mkaidi na baba namsikiliza lakini ninyi ndio hamnisikilizi"

"nataka nikuombee msamaha kwa baba yako akutoe humu"
"wala sihitaji kutoka humu mama acha tu nimalizie adhabu yangu"

"Adrian unaona hali ya humo ndani ilivyo au unataka uumwe ndiyo uelewe?"

"nipo salama mama"
"nakuombea msamaha kwa baba yako akutoe"
"sitaki kutoka humu mpaka nimalize adhabu yangu" Adrian alimjibu mama yake ambae alimtazama tu akimshangaa

Maya akiwa chini ya ulinzi wa askari alifikishwa mpaka nje ya kasri akaitwa muuguzi ili ampatie matibabu na akaanza kumfunga jeraha lake

Mjakazi mkuu ndani ya kasri la mfalme na msimamizi mkuu wa wajakazi wote Bi. Kalla alikuwa anapita kwenye korido ya vyumba vya ndani ya kasri akikagua kuhakikisha kuwa kila kitu kinaenda sawa hasa suala zima la usafi

"dada dada!!" mjakazi mmoja alimkimbilia mbiombio akiwa na nguo (gauni) mkononi

"kuna nini?" alisimama kumsikiliza
"angalia hili gauni" alipewa gauni hilo akalitazama

"hili gauni limeandikwa maelekezo ya jinsi ya kupika hatua zote na vifaa vyote vinavyotakiwa, ni lile lile alilovaa Sethi binti wa Waziri Mkuu"

"ndiyo dada alipoondoka alioga akabadilisha nguo akaliacha gauni lake nahisi akijisahau, inaonekana hakupika kwa akili yake kuna mtu alimuelekeza"

"ni nani huyo aliyemuelekeza sasa?" bi Kalla aliuliza na wakati huo mwanamfalme Teri alikuwa anakatiza kwenye kona akasikia mazungumzo hayo

"ohoo kumbe mchumba wa braza ametupiga changa la macho kile chakula hajapika yeye, basi ataisoma namba lazima nimuumbue maana anamdanganya sana kaka amekuwa kama zoba kisa yule msichana" Teri alijisemesha huku akitabasamu kisha akajitokeza, bi Kalla akalificha lile gauni nyuma ili mwanamfalme Teri asilione

"mlikuwa mnazungumzia nini?"
"hakuna kitu mtukufu mwanamfalme"
"ooh hamuwezi kunificha naombeni hicho mlichokificha" alinyoosha mkono kuwaomba

"lakini mwanamfalme ni... "
"nimesema naomba"

"Tafadhali mtukufu mfalme jambo hili mfalme na malkia wasilijue"
"siyo kazi yenu" Teri aliongea na kuwanyang'anya gauni hilo wakabaki wanatazamana wametoa macho...

*MAYA* 💃

*SEHEMU YA 13*

Piso alikuwa amesimama kwenye baraza akitazama bustanini huku akitabasamu kwa sababu ya furaha aliyonayo baada ya kukubaliwa kwa mchumba wake Sethi kwa wazazi wake baba na mama baada ya kula chakula cha binti hiyo na kukisifia kuwa kitamu kama walivyompa mtihani

"nakuona una furaha mwenyewe" Teri alimkuta akamwambia na kusimama kando yake nae akitabasamu

"sana yaani furaha yangu imepitiliza kuliko kawaida Teri kwa sababu nitamuoa yule nimpendae na wazazi wangu wameshakubali sasa hakuna pingamizi tena"

"sikufanikiwa kukionja hiko chakula ila inaonekana aliyekipika huyo ni fundi kweli kweli mpaka Sethi akaelekezeka shemeji yangu kwa muda mfupi sana"

"unamaanisha nini Teri?"
"namaanisha hiki hapa, hili gauni ni la nani?" Alimwonyesha
"ni la Sethi"
"soma hapa" alimwonyesha Piso akaanza kusoma kilichoandikwa katika gauni hilo akashtuka na kumtazama Teri

"ni nani aliyeyaandika haya?"

"Sethi inaonekana dhahiri kuwa hakupika yeye kaka kwahiyo kuwa makini sana" Teri alimwambia huku akiondoka taratibu, Piso akamfuata nyuma nyuma na kumshika ndugu yake huyo akiwa amepoa kwelikweli

"Teri usimwambie baba na mama tafadhali"
"sitawaambia" Teri alimjibu ndugu yake huyo na kuondoka zake taratibu

"ni nani huyu aliyemsaidia Sethi kupika chakula kile kama siyo yeye Sethi aliyepika mwenyewe?" Piso alijiuliza akaamua kutoka kwenda nje kufuatilia kuhusu jambo hilo hilo akaenda mpaka nje akakutana na mwanadada Maya aliyekuwa anafungwa jereha lake la mkononi akampita na kwenda kwa askari mmoja aliye lindo ambae alikuwepo wakati ule ambao mpenziwe Sethi anahangaika na mambo ya mapishi na ndiye askari aliyemsindikiza mpaka kule bondeni bustanini

"mtukufu mwanamfalme"
"nina swali la kukuuliza"
"niulize mtukufu mwanamfalme"

"ulimwona na nani wakati ule mchumba wangu Sethi ulipomsindikiza kule akajiandae kwa ajili ya mapishi?"

"hakuwa na mtu mtukufu mwanamfalme, mchumba wako Sethi alikuwa mwenyewe tu"

"unazungumza ukweli?"
"hakika mtukufu mwanamfalme" askari huyo alimuitikia, Piso akatikisa kichwa chake tu akionekana kutoridhika bado na maelezo hayo ya askari

Upande mwingine mwanadada Sethi alikuwa akiingia ndani na mama yake wakiwa wametokea ndani ya kasri la mfalme,

"nataka kujua ukweli Sethi ni nani aliyepika kile chakula"

"ukweli upi mama si mimi niliyepika au?"
"hapana siyo kweli, wewe ninakujua na nimekulea mimi mwenyewe tangu mdogo huwezi kupika chakula kizuri kama kile ambacho hata mimi mama yako sikiwezi kukipika"

"unanidharau mama?"
"hapana sikudharau binti yangu nachotaka tu ni uniambie ukweli kwa sababu nakujua binti yangu"

"mama!!" Sethi alisita kidogo
"nini tena?"
"nimesahau kitu ohoo balaa hili"

"nini hicho?"
"gauni langu"
"la?"
"nililoandika maelekezo ya mapishi yale niliyoyapika"
"uliandika kwenye gauni kivipi?"
"aaah mama turudi ndani ya kasri nitaumbuka mimi"

"kwanini?"

"mama uuwiiii gauni" Sethi aliruka ruka kwa wasiwasi alipokumbuka kuwa ameacha gauni lake lenye siri kubwa ndani yake ambalo aliliandika maelekezo aliyopewa na Maya ya jinsi ya kupika na mahitaji na vipimo na kila kitu ambalo kama likimfikia mfalme Bono na mkewe malkia Zilpa basi ukweli kuwa chakula kile kilichosifiwa na mfalme na malkia kutokana na utamu na ubora wake, kuwa hajakipika yeye na hilo litaonekana kuwa amemdanganya mfalme na huenda likasababisha ndoa yake na mwanamfalme Adrian isiwepo tena na hata akaadhibiwa

"sikuelewi ujue Sethi, gauni mara nini mara nini?"

"narudi ndani ya kasri mama narudi" Sethi aliongea huku akirejea kwenye gari lao (la farasi)

"Sethi Sethi" mama yake alimwita bila mafanikio binti yake huyo ambae alikusudia kabisa kuondoka kurudi ndani ya kasri

Upande mwingine ndani ya kasri la mfalme Bono, Maya alikuwa akisindikizwa na askari mmoja kurudishwa ndani ya banda la vinyesi vya wanyama akaendelee kukaa humo lakini njiani akasimamishwa na mjakazi Lela ambae alimtaka askari anayemsindikiza Maya akae pembeni kidogo

"Wewe!?"
"abee"
"kuwa makini na kaa mbali na mwanamfalme Adrian si umenisikia?"
"kwanini unaniambia hivyo?"
"nakupa tahadhari tu lasivyo nitakufanya kitu kibaya" Lela alimsonya Maya kisha akaondoka taratibu na mpambe wake aliyefuatana nae

Adrian alikuwa amebaki mwenyewe tu ndani ya banda la vinyesi vya wanyama akitumikia adhabu aliyopewa na baba yake, lakini akaanza kuhisi upweke wa ghafla alipomkosa Maya ndani ya banda hilo ambalo walikuwa wawili

"kwanini najihisi upweke kwanini Adrian tulia tulia hakuna kitu kama hicho" Adrian alijisemea moyoni na alipotazama mbele akamwona Maya akajikuta anatabasamu kwa furaha lakini akaukunja uso wake mwanadada huyo asije akamgundua kuwa amefurahi kumwona anarudi

"asante mtukufu mwanamfalme" Maya alimshukuru akiwa chini ya ulinzi wa askari wakati akirudishwa kwenye banda hilo la vinyesi vya wanyama

"asante ya nini?"
"kwa kujali jeraha langu mpaka nikaenda kupata matibabu"

"usijali, unakuja wapi huku?"

"nakuja ndani humo"
"hapana huku usije tena"
"mtukufu mwanamfalme"
"kwani si mimi niliyekupa adhabu hii basi adhabu yako imeshakwisha ruksa kuondoka humu"

"lakini mtukufu mwanamfalme ni..??"

"Maya nisikilize mimi" mwanamfalme Adrian alisisitiza na wakati huohuo ndugu yake mwanamfalme Piso alikuwa anakuja maeneo hayohayo, Maya akageuka na kumuona akainamisha kichwa chake

"wewe ndiye uliyemuelekeza Sethi jinsi ya kupika?" Piso alimwuliza Maya swali lililomshtua akageuka na kumtazama Adrian kisha akamtazama tena mwanamfalme Piso

"unazungumzia nini mtukufu mwanamfalme?"

"nilimwona Sethi akija maeneo haya wakati akiwa na mtihani aliopewa na baba wa kupika chakula kizuri na kuna mtu inaonekana ndiye aliyemuelekeza namna ya kupika chakula kile mpaka kikapendwa na baba na mama na wengine wote sema ukweli ni wewe uliyemuelekeza na kumwandikia mchumba wangu Sethi?"

"Piso acha kumsumbua msichana wa watu" Adrian aliingilia kati

"hili halikuhusu wewe Adrian ni baina yangu na huyu msichana, Maya nijibu swali langu niwewe uliyempa maelekezo ya kupika mchumba wangu Sethi ama siyo wewe?"

"samahani mtukufu mfalme siwezi kujibu swali hilo kwa sasa" Maya aliinamisha uso wake chini akiwa amejawa wasiwasi maana hakujua nia hasa ya swali hilo

"ni yeye aliyepika" mara ikasikika sauti ya kike ikijibu nyuma yao....

*MAYA💃*

*SEHEMU YA 14*

"ni yeye aliyepika" sauti ilisikika nyuma, Maya na mwanamfalme Piso wote wakageuka, Adrian nae akatazama kwa umakini, wakamwona mjakazi mkuu bi Kalla akija

"mwanamfalme Piso na mtukufu mwanamfalme Adrian samahani kwa kuwaingilia maongezi yenu" aliinamisha uso wake, Maya akabaki kimya ameinamisha uso wake

"ni kweli Maya wewe ndiye uliyemuelekeza Sethi ili apike kile chakula?" Piso alimwuliza tena Maya ambae aliwatazama wote usoni huku akiogopa ogopa

"mpenzi wangu" mara wakasikia sauti nyuma yao kutazama kumbe alikuwa ni mwanadada Sethi ambae alisharudi ndani ya kasri baada ya kugundua kuwa amelisahau gauni lake aliloandikia maelekezo ya mapishi aliyoambiwa na Maya, alilivua na kubadilisha jingine wakati anatoka na ndipo akaliacha kwa bahati mbaya

"Sethi vipi mbona umerudi?"
"nimesahau gauni langu mpenzi kuna nini kinaendelea hapa?"
"tunazungumza tu mambo fulani, kama umesahau gauni tu si ningekuletea jamani Sethi mpaka uhangaike kurudi tena kisa gauni tu, lina umuhimu gani sana jamani?"

"hamna nalipenda tu nilinunuliwa zawadi, ngoja nikalifuate kwa wajakazi"

"hautolipata ninalo mimi"
"unalo wewe?" Sethi alishtuka kidogo
"twende tukazungumze" Piso alimshika mchumba wake huyo na kuondoka nae,

"Maya samahani nina mazungumzo nawewe, samahani mtukufu mwanamfalme" mjakazi mkuu Kalla alimwita mwanadada huyo, Adrian akatikisa kichwa kukubali Maya achukuliwe pembeni na mwanadada huyo

Adrian akarudi ndani bandani maana alikuwa anachungulia tu dirishani

"kama huyu Maya anapika vizuri kwanini nisimwombe baba na mama awe mpishi wangu nikiondoka ndani ya kasri humu?" alijiuliza mwenyewe kimoyo moyo

Mjakazi mkuu Kalla alimwita Maya pembeni na kuanza kuzungumza nae akimwuliza historia yake na mahali alipotoka, mama huyo akabaki anatikisa kichwa kumsikiliza

"Maya nimekupenda sana na nimetokea kukipenda sana chakula chako, unapika vizuri sana na inaonekana una kipaji"

"asante dada"
"sasa nilitaka nikuombee nafasi kwa malkia ili uwe miongoni mwa wapishi humu ndani ya kasri la mfalme lakini utalazimika kuingia kwenye shindano la mapishi kesho kwa sababu lilishaitishwa ili uweze kurudi tena humu ndani ya kasri rasmi kwa utaratibu mzuri"

"sawa dada"
"fanya kadri uwezavyo ninakuandikisha sasa kwenye shindano hilo fanya uwezavyo uibuke mshindi urudi humu ndani ya kasri sawa?"

"sawa dada nitafanya kadri niwezavyo" Maya aliitikia mwanamama huyo alitabasamu na kumshika begani akaondoka zake na Maya akiwa ameongozana na askari akaanza kurudishwa kule kwenye mabanda ya vinyesi vya wanyama akiwa ananuka nguo zake amechoka hajala chochote wala kunywa chochote kile

Mwanamfalme Teri alikuwa amesimama tu juu ya baraza akiangalia kinachoendelea chini akamwita askari mmoja ambae ndiye mpelelezi wake ndani ya kasri akasimama kando yake wakinong'onezana maana alimtuma achunguze chunguze kinachoendelea

"yule msichana anaitwa nani?"
"Maya mtukufu mwanamfalme"
"vizuri, umefuatilia ukajua alikuwa anazungumza nini na mjakazi mkuu?"
"sijasikia vizuri lakini kuna tetesi za chini chini kuwa ni yeye aliyemuelekeza Sethi mchumba wa mwanamfalme Piso mpaka akapika chakula kile kizuri"

"najua kama Sethi hajui kupika lakini suala la yule msichana Maya kuwa mpishi mzuri wa chakula kama kile naona unaniongopea hebu fuatilia vizuri unipe taarifa iliyonyooka na siyo uwongo uwongo"

"nachokwambia ndicho nilichokisikia mtukufu mwanamfalme"

"nahitaji kuongea na huyo msichana akiwa msafi lakini"
"sawa mtukufu mwanamfalme nitahakikisha namleta kwako haraka iwezekanavyo"

"nisiuone uso wako hapa"
"sawa mtukufu mwanamfalme"
askari huyo mpelelezi wake, akaondoka haraka na kwenda lindoni akiwa na kazi ya kulinda na pia akiwa na kazi ya kukusanya taarifa ya kila kinachoendelea na kwenda kumpa taarifa mwanamfalme huyo

Mwanamfalme Piso hakumwingiza Sethi ndani tena akaishia nje tu nae, kwenye baraza ya nyuma ya kasri lao hilo akabaki amejishika kichwa akitembea tembea na kuzunguka zunguka tu

"mpenzi wangu Piso mbona huniambii kuna nini?"
"kwanini umeamua kunidanganya Sethi?"
"nimekudanganyaje Piso mpenzi wangu jamani?"
"kile chakula amepika nani niambie ukweli"
"nimepika mimi mpenzi wangu kwanini?"
"unanidanganya Sethi"

"kwanini nikudanganye kwani hukuniona nilivyokuwa napika mbona kila kitu kilikuwa wazi kabisa au unanichukuliaje sijui kupika au?"

"hapana sijamaanisha hivyo lakini vipi kuhusu maandishi ya kwenye gauni lako yale maelekezo ya mapishi?"

"maandishi kwenye gauni langu mbona sikuelewi Piso?"
"usijifanye hujui chochote Sethi tafadhali niambie ukweli"

"ni vyema ukatuambia tu ukweli shemeji yangu ni wewe uliyepika au msichana Maya aliyekuwa nyuma ya mgongo wako?" mara walisikia sauti wote wawili, Piso na Sethi wakageuka na kumkuta mwanamfalme Teri akiwa amesimama na lile gauni la Sethi lenye maandishi kwa ndani

"gauni langu tafadhali" Sethi alitaka kulichukua gauni lake mikononi mwa mwanamfalme Teri lakini kijana huyo akalikwepesha gauni hilo mwanadada huyo asiweze kulichukua

"ungejibu kwanza maswali magumu anayokuuliza Piso shemeji ndipo nikupatie gauni lako" Teri alitabasamu

"maongezi ni ya watu wawili mimi na mchumba wangu Sethi ni nani aliyekuruhusu kuingilia Teri"

"sijayaingilia mimi nilikuwa napita zangu nikasikia kinachoongelewa ushahidi ninao mkononi sasa kwani kuna ubaya kaka?" Teri aliuliza akimtazama kaka yake aliyemtangulia kutoka tumboni, pacha mwenzake Piso, kisha akamtazama na shemejie Sethi kwa tabasamu jepesi

"Piso naomba niondoke kwa sababu unanichanganya na hutaki kuniamini kwa lolote lile" Sethi aliondoka kwa hasira akiwapita ndugu hao wawili

"Sethi subiri nataka tuzungumze tu usiwe mwepesi wa hasira" Piso alimfuata mwanadada huyo nyuma nyuma huku akimshika mkono kumbembeleza

"shemeji umekuwa muongo sana, sitaacha kukusumbua Sethi mpaka nihakikishe nalipa kisasi kwa udhalimu ulionifanyia" Teri aliongea mwenyewe huku akilitazama lile gauni mkononi mwake na kutabasamu

Maya alikuwa amefuatana na askari mpaka kwenye mabanda ya vinyesi vya wanyama alipomwacha mwanamfalme Adrian aliyekuwa akitumikia kifungo chake bado

"Maya umekuja kufanya nini tena huku?" Adrian alimwuliza akiwa anakula chakula chake
"nimekuja ku..."
"we askari, huyu ni mimi niliyempa adhabu na ni mimi niliyemwacha huru kwahiyo asirudi tena humu"

"nimpeleke wapi mtukufu mwanamfalme?"
"tafuta popote pa kumpeleka" Adrian alimjibu askari

"mlete kwangu nina mazungumzo nae kidogo" wakasikia sauti nyuma walipotazama alikuwa ni mwanamfalme Teri

"mtukufu mwanamfalme?" Maya aliinamisha uso wake
"jina lako nani Maya siyo?"
"ndiyo mtukufu mwanamfalme, naitwa Maya"
"nimesikia sifa zako chache nahitaji kuzungumza nawewe kidogo nifuate" Teri aliongea akigeuka kuondoka taratibu, Maya akageuka na kumtazama mwanamfalme Adrian mule bandani akiwa ameinamisha kichwa chake kisha akageuka na kumfuata mwanamfalme Teri nyuma

"Teri ana shida gani na Maya??!!!" Adrian alijiuliza kwa hasira na kupiga ngumi ukuta wa banda hilo lililojengwa kwa magogo manene manene ya mti...

*MAYA* 💃

*SEHEMU YA 15*

Mwanadada Maya alimfuata mwanamfalme Teri nyuma nyuma mpaka bustanini, kijana huyo akasimama nae akasimama

"Maya!!"
"abee mtukufu mwanamfalme"
"najua wewe ndiye uliyetengeneza chakula kile kitamu na kizuri kama sikosei?"
"ndi.. hapana mtukufu mwanamfalme"

"teh teh teh huna haja ya kuogopa kusema ukweli ninajua kila kitu na hata gauni la shemeji yangu mtarajiwa Sethi ninalo mimi hapa nikiamua kukufanyia kitu kibaya naweza na nikiamua kukufanyia kitu kizuri naweza pia, chagua mwenyewe unataka nikufanyie kitu gani kibaya au kizuri?"

"kitu kikupendezacho mtukufu mwanamfalme" Maya alijibu akiwa ameinamisha kichwa chini kwa hofu na aibu mbele ya kijana huyo mwanamfalme

Ndipo Teri akamwita mjakazi mmoja aliyekuwa anakatiza akamnong'oneza sikioni mwanadadq huyo na kuwaacha Maya na mwanadada huyo wawili

"twende!!" yule mjakazi aitwae Hathra alimwambia Maya kwa ukali, Maya akiwa hajui ni jambo gani mjakazi huyo alilonong'onezwa na mwanamfalme Teri

"tunaenda wapi?"
"sitaki maswali" alimjibu kwa mkato na kwa hasira akiwa anamtazama Maya kwa jicho kali, Maya ikabidi anyamaze asizungumze chochote tena wakaongozana mpaka kwenye mabafu maalumu ya wajakazi Maya akaonyeshwa aingie bafu moja akaoge, akaingia na kuoga akiwa na maswali mengi kuhusu nini kinachofuata, alipomaliza kuoga akaletewa mavazi maalumu ya wajakazi akashangaa

"ya nini haya?" ilibidi aulize
"kwani sisi tumevaa ya nini?" mjakazi huyo aliyepewa kazi ya kumsimamia Maya alijibu vibaya kama kawaida yake

"yaani ni hivi inaonekana nawewe sasa umepata fursa ya kuwa mjakazi ndani ya jumba la mfalme na ni mrembo miongoni mwa warembo ndani ya kasri la mfalme waliopata fursa nyeti kabisa ya kumtumikia mfalme ndani ya jumba la kifalme karibu sana unaitwa nani?" mjakazi mmoja alimpa mkono

"Maya wewe je?"

"naitwa Zasha" mjakazi huyo alitabasamu na kumpa mkono Maya, ambae hakujua atabasamu au anune, acheke au alie, alibaki ameduwaa tu huku wajakazi wote wa jumba la kifalme waliokuwa mezani wakila walikuwa wakimtazama Maya mpaka akaona aibu

Maya aliwatazama wajakazi wote waliokuwa wamekaa pamoja walikuwa warembo sana na wamependeza kwenye sare zao, akajitazama yeye mwenyewe akajiona peke yake ndiye mshamba mshamba

Akalivaa gauni lake alilopewa na wote wakaanza kumcheka kwa sababu lilikuwa kubwa na panapana

"mbona umempa Maya gauni kubwa kubwa ambalo siyo saizi yake Hathra?" Mjakazi Zasha alimwuliza mwenzake huyo

"vipi kazi hii mwanamfalme Teri hakukuona wewe mpaka akanipa mimi mbona unaingilia majukumu yasiyo yako Zasha?" Hathra alimwuliza

"hapana Zasha linanifaa kabisa hili gauni usijali limenitosha" Maya alijibu huku akizunguka zunguka kujitazama lakini halikuwa saizi yake halikumkaa mwilini vizuri, Zasha na Hathra wakabaki wanatazamana wakiwa wamenuniana Zasha akiwa hajafurahishwa na kitendo cha Maya kuchaguliwa gauni kubwa kubwa tofauti na mwili wake

"haya mmalize kula muda wa majukumu mengine umeshafika akina dada msishangae shangae" mjakazi mkuu bi Kalla aliingia kuwahimiza na ndipo akamwona Maya akashtuka kumuona

"salamu dada" Maya alimsalimia mwanamama huyo

"Maya umefuata nini humu kwa wajakazi na kwanini umevaa nguo za wajakazi wakati wewe siyo mjakazi?"

"mtukufu mwanamfalme Teri ndiye aliyetoa agizo niletwe huku niwe mjakazi"

"Teri?? Basi una bahati sana Maya lakini jambo hili bado halijafika kwa mfalme na mtukufu malkia, usifanye chochote mpaka nisikie uamuzi wao wa mwisho..." kabla mjakazi mkuu Kalla hajamaliza sentensi yake alikuja mjakazi mwingine mbiombio

"dada Kalla Maya anaitwa na mwanamfalme Teri" alitoa taarifa, bi Kalla akamtazama Maya na kumshika begani

"bahati njema, unaweza kwenda kuanza kazi yako sasa Maya, mimi sina pingamizi tena kama aliyetoa maamuzi hayo ni mwanamfalme" bi Kalla alimwambia Maya ambae alitikisa kichwa na kuongozana na mjakazi huyo aliyetumwa kuja kumuita kwenda kusikiliza haja ya mwanamfalme Teri

"Hathra inakupasa kuwa makini kwa sasa kuliko wakati wowote ule" Lela alimwambia mwenzake

"huyu Maya lazima ataiona kazi yake chungu sitaruhusu ajisogeze sogeze karibu na mwanamfalme Teri hata kidogo asidhani kuwa mjakazi humu ndani ya kasri basi atakuwa ameshafanikiwa kila kitu, hilo asahau" Hathra aliongea

"kila mtu na achunge mzigo wake na kila mtu apambane mechi zake" Lela nae aliongea wote wakatikisa kichwa, mjakazi Lela akiwa anampenda sana mwanamfalme Adrian na mjakazi Hathra akiwa anampenda sana mwanamfalme Teri

Maya aliitikia wito na kwenda mpaka kwa mwanamfalme Teri akasimama mbele yake na kuinamisha uso wake chini

"Mbona umevaa gauni kubwa sana Maya?"
"ndilo nililolipenda hili mtukufu mwanamfalme"
"ooh vizuri sasa nataka uniandalie chakula kisha uniletee chumbani kwangu nina njaa sana, chakula ukitengeneze kwa mikono yako, chakula cha asili cha (... )"

"sawa mtukufu mwanamfalme" Maya aliitika kijana huyo akaondoka taratibu na Maya akarejea mpaka kwa mjakazi mkuu bi Kalla ambae aliongozana na mwanadada huyo mpaka ndani ya kasri akiwa ametangulia mbele na Maya yupo nyuma ameinamisha uso wake, kwa mara ya kwanza katika maisha yake Maya akajikuta anaingia ndani kabisa ya jumba la kifalme akiwa hajawahi kutegemea wala kuwaza maishani mwake

Mjakazi Hatra wakati akiwa na wenzake baadhi wanachuma matunda bustanini kwa ajili ya kutengeneza juisi, mmojawapo wa wajakazi waliokuwa ndani ya kasri ambae ndiye rafiko yake wa muda wote na mpelelezi wa kumletea habari zote alimfuata Hathra mbiombio

"Hathra!!"
"kulikoni mbona mbio mbio?"
"Maya huko mwe"
"kafanyaje tena?"
"nimeona anaongozana na bi Kalla inaonekana anaenda kumpikia chakula mwanamfalme Teri sasa wewe umewahi hata kumpikia mwanamfalme ukizubaa imekula kwako, mimi nimeleta tu ripoti habari ndo hiyo"

"haiwezekani kitokee kitu kama hicho"
"wewe sema tu haiwezekani na huku umetulia utakuja kushangaa imewezekana fanya jambo umuharibie Maya ama sivyo itakula kwako" mwenzake alimwambia Hathra ambae alishusha pumzi ndefu ya hasira kisha akamtazama mwenzake huyo na kutikisa kichwa chake akiashiria yupo tayari kwa vita....

*Msiolipia MAYA nawazoom tu, tsh1000 Halopesa hii 0626363334 jina Neema*
*MAYA*💃

*SEHEMU YA 16---20*

Adrian alibaki akitembea tembea na kuzunguka zunguka peke yake ndani ya banda huku akijikuna kichwa usiku ukiwa umeshaingia ndani ya kasri akiwa ameshaizoea harufu ndani ya banda hilo lakini alichokuwa hajakizoea bado ni kukaa peke yake ndani ya banda akitazama kila wakati pale ambapo Maya alipendelea kukaa kwenye nguzo moja ya mti aliyopenda kuegemea akawa anaona kama bado yupo na Maya wapo wawili bandani

"mtu anawezaje kumzuia mtu mwingine asiumie kwa kuweka mkono wake akaumia yeye mwenyewe?" alijiuliza kimoyo

"mwanamfalme Adrian?" alishtuka alipoitwa
"Maya" akaita na kugeuka akidhani ni sauti ya Maya labda lakini akakuta wala siyo Maya aliyemdhania

"ni mimi Lela mtukufu mwanamfalme nimekuletea chakula na juisi njoo uchukue haraka haraka kabla sijaonwa" Lela aliongea kwa kunong'ona kichini chini

"Lela, Maya yuko wapi vipi ameshaachiwa ndani ya kasri ameondoka, anaendeleaje ule mkono?" Adrian alimwuliza

"mara ya kwanza umeniita Maya nimevumilia lakini bado hujaridhika unaanza kuniulizia mimi habari za Maya bila kujali hata kilichonileta hapa wakati ni kwa faida yako, huyo Maya anakujali kama ninavyokujali mimi Adrian mpaka umtaje taje kila wakati kweli Adrian??!!" Lela aliongea kimoyomoyo huku akiwa amezubaa anamtazama Adrian usoni

Mwanadada huyu haumwambii kitu kwa mwanamfalme Adrian, anampenda sana na ni ndoto yake siku moja aweze kuolewa na mwanamfalme Adrian ambayo mwenyewe Lela ana imani kuwa ndoto hiyo siku moja inaweza ikawa kweli

"Lela??!" upo hapa Lela

"abee mwanamfalme samahani kuna kitu nilikuwa nakumbuka mara moja, umeulizaje?"

"nimeuliza Maya vipi anaendeleaje?"
"ooh Maya yupo anampikia chakula mwanamfalme Teri ndani ya kasri nadhani ndiyo anaanza muda huu"

"anampikia chakula kivipi na mkono wake ule wenye jeraha?" Adrian alionekana kutofurahishwa kabisa na habari hizo

"ndiyo mtukufu mwanamfalme hebu chukua chakula mimi nataka kuwahi nisije nikakutwa bure hapa na kugundulika kuwa nakuletea letea chakula kwa kujiiba iba" mjakazi Lela alimwambia mwanamfalme aliyekipokea chakula hicho na kinywaji mikononi mwake na kutikisa tu kichwa chake, Lela akaondoka kwa mwendo wa taratibu akisindikizwa na askari mmoja ambae ndiye anakula nae dili akitegemea mwanamfalme Adrian angemshukuru kwa kumwambia neno asante kama alivyozoea lakini leo akiambulia patupu, Adrian hakujibu chochote, akili yake ilikuwa mbali sana

"oooopppsss" Adrian alishusha pumzi ndefu na kukaa chini kiunyonge huku akikitazama kile kitambaa alichokitumia kumpoza Maya jeraha la kofi alilomzaba usoni kwa sababu ya hasira...

Upande mwingine ndani ya kasri, Maya ameshaingia jikoni tayari kuandaa chakula kwa ajili ya mwanamfalme Teri kama alivyoagizwa ampikie kijana huyo chakula kizuri sana kama kile alichomuelekeza Sethi mchumba wa mwanamfalme Piso, Maya akawa anahangaika jikoni peke yake huku kwenye korido askari mmoja anayelinda mazingira ya jikoni akiwa lindoni anatembea tembea, na ni muda huohuo mjakazi Hathra alikuwa ameshaingia ndani anaelekea huko huko maeneo ya jikoni akiwa ameshika kijikaratasi alichokifunga vizuri na kukifichia ndani ya gauni lake refu la sare ya wajakazi

"wewe unakwenda wapi?" askari aliyekuwa lindo maeneo ya jikoni alimuuliza
"jamani askari wewe kijana mtanashati sana mh sijapata kuona" Hathra alianza kumsifia sifia askari huyo

"mh kweli unayoyasema mrembo jamani?"
"ni kweli kwanini nikudanganye jamani ili nipate nini eeh!?"
"asante sana teh teg tunaweza kuonana baadae?"
"tunaweza ila nisaidie kitu kimoja kwanza"
"kipi hicho mrembo?"

"naomba uende hapo nje ukaniitie rafiki yangu yule nayeongozana nae sana maana malkia ametuita sasa kutoka nje nashindwa kuna kazi naifanya"

"bila shaka" askari alijibu na kutoka haraka kwenda kumuita mjakazi mwenzake Hathra na ndipo Hathra aliposogea mpaka kwenye mlango wa jiko alimokuwemo Maya akamchungulia na kumkuta mwanadada huyo akiwa bize anatengeneza chakula hicho kilichokuwa kinatokota jikoni akiwa kwenye hatua za mwisho kabisa za kukiivisha na kumbe licha ya Hathra kuwa na kijikaratasi alichofunga kitu pia alikuwa na kibakuli kidogo cha udongo amekishika mkononi akakitupa kwa nyuma ya ukuta wa jiko kikaanguka na kuvunjika

"nini hicho tena kinaanguka na kuvunjika?!!" Maya alishtuka na kutoka jikoni akazunguka nyuma ya ukuta kutazama kilichoanguka na ni wakati huohuo mwanadada Hathra aliyekuwa amejibanza kwenye ukuta wa upande wa pili akajitokeza na kuingia jikoni akafungua kijikaratasi chake haraka harak chenye pilipili nyingi, chumvi nyingi na majani fulani machungu sana ya porini akakitia kwenye mchemsho uliokuwa unatokota jikoni na haraka haraka akatoka jikoni, wakati anamalizikia kuondoka na ndio Maya alikuwa anarudi jikoni akaona kijipande cha nguo kinamalizikia na aliposogea kuchungulia hakuona mtu zaidi ya askari yule mwenye lindo aliyekuwa anakuja kwa mbali

Maya akatikisa kichwa chake na kurudi jikoni, akakuta mchemsho wake unatokota jikoni akaepua na kuuweka pembeni kitu kikamtuma moyoni aonje chakula hicho lakini hakuthubutu kuonja akaogopa maana alisikia kwa wajakazi wenzake kuwa sheria za mapishi ndani ya kasri haziruhusu mjakazi kuonja chakula chakula cha mfalme jikoni ila kuna muonjaji maalumu mezani anayeonja chakula cha familia ya mfalme

"Maya!" ndipo alipoitwa nyuma yake akageuka kutazama akamkuta ni mjakazi mkuu bi Kalla akamtazama kwa tabasamu

"abee dada?"

"umemaliza mapishi?"
"ndiyo dada"
"waaaoh kinaonekana kitamu sana"
"mh dada"
"ndiyo ninachosema ni kweli kabisa Maya, mimi ni mpishi sasa kwa zaidi ya miaka thelathini ninajua aina nyingi za mapishi na chakula kitamu nakijua tu kwa harufu yake na kibovu vile vile nakitambua kwa harufu yake pia"

"kumbe dada?"
"kabisaaaa!"
"umekionja?"
"hapana dada"
"kwanini?"
"nimesikia hairuhusiwi kuonja"

"nani amekwambia, hakuna mpishi asiyeonja mapishi yake, walizuia kwa sababu kuna wapishi walikuwa hawazingatii usafi"

"basi kwa sababu dada umekuja naomba wewe uonje chakula changu kwa niaba yangu na utoe neno karibu" Maya alimfunulia bi Kalla vyakula hivyo alivyoviandaa

"ewaaa tena naanza na huu mchemsho wenyewe wa mboga mboga na nyama" bi Kalla alichukua kijiko na kuchota chakula akakipeleka taratibu mdomoni na kuanza kukitafuna huku Maya akiwa amemtolea macho akisubiri maoni ya mwanamama huyo ambae mara ghafla wakati anatafuna akatoa macho na kusita kuendelea kutafuna akimtazama Maya

"dada kuna nini?" Alimwuliza lakini kabla hajajibu bi Kalla aliinama na kukitema chakula hicho chote chini kutoka kinywani

"Maya fanya haraka naomba maji ya kunywa!!"....

*MAYA* 💃

*SEHEMU YA 17*

Mwanamama Kalla alitema chakula chote alichokuwa akikitafuna mdomoni na kumuomba Maya maji ya kunywa, mwanadada huyo akakimbia haraka haraka na kumchotea maji akamletea na kumnywesha bosi wake huyo ambaye pia aliyasukutua na kutema mara kadhaa huku akikohoa

"Maya!!?"
"abee dada jamani kuna nini kwenye chakula tena?"

"hilo swali nikuulize wewe umeweka nini kwenye chakula?"
"sijaweka kitu zaidi ya mboga mboga na nyama na viungo na chumvi kwani kuna nini?"

"aisee umeweka vitu vibaya sana"
"vitu gani tena dada?"
"pilipili nyingi, chumvi nyingi na vitu vichungu sana yaani hiki chakula ndiyo ulitaka umpelekee mwanamfalme hivi kweli?"

"mbona mimi sijaweka kitu chochote dada vitu kama hivyo sijaweka dada sijaweka"

"unataka unikoseshe kazi Maya nionekane siwasimamii vizuri koh koh!!"

"pole dada pole, sasa vimeingiaje hivyo vitu mbona mimi sijaweka?" Maya alijiuliza huku akimkalisha bi Kalla kwenye kiti na kuanza kumbembeleza bembeleza akimpiga piga mgongoni

"usijali nipo sawa kabisa futa futa tu hapo nilipopachafua"

"sawa dada mh imekuwaje?" Maya alishusha pumzi ndefu akachukua dekio na kuanza kufanya usafi jikoni hapo na alipotupa macho mbele akaona kijikaratasi chini kimeanguka chini sakafuni akakifuata na kukishika taratibu akikitazama na bi Kalla akamwambia

"nini hicho ulichokishika Maya?"
"sijui ni nini naona kimefungwa fungwa tu dada hapa"
"hebu nikione" alimwomba akakishika na kukitazama akakinusa nusa huku akimtazama Maya usoni

"ni nini hiko dada?"

"nasikia mchanganyiko wa harufu za pilipili na majani machungu sana na chumvi kali ya chuma, nusa" bi Kalla alimnusisha Maya

"mimi pua zangu hazinusi harufu yoyote nimezaliwa hivyo"
"ooh sikujua, samahani"
"usijali dada, kimetokea wapi hiki kikaratasi na nani amekileta na kukiangusha??!!"

"inaonekana ndiye aliyetia kwenye chakula humu"

"ni nani aliyenifanyia hivi na amefanya kwa nia gani?"
"wote hatujui"
"halafu nimekumbuka kitu"

"kipi hicho?"
"wakati naingia jikoni niliona kama kulikuwa na mtu anatoka lakini niliona nguo tu inaishia ishia"

"atakuwa nani huyo mtu?"
"sijui dada sikuweza kumwona maana nilisikia kitu kikivunjika nikatoka kujua kulikoni ndo wakati narudi nikaona nguo inaishia ishia"

"mh atakuwa nani?" bi Kalla aliuliza tena

"sielewi" Maya akanyanyua mabega juu kumaanisha kuwa hajui chochote wote wakabaki wanatazamana tu wakiwa njiapanda hawaelewi kinachoendelea

Nje bustanini mjakazi Hathra alikuwa ameongozana na mwenzake wakitembea aitwae Verda

"Yaani mimi mwenzako Hathra sijui nipoje sikuhizi?"
"kwanini?"
"yaani nikimwona mwanamfalme Piso nachanganyikiwa mwenzako"
"unamwogopa au?"
"wala siyo kumuogopa ila tu nahisi kama naanza kumpenda penda sijui kumtaka taka yaani hata sielewi elewi"

"ana mchumba wake mwenzio si ulimwona Sethi mtoto wa Waziri Mkuu sasa wewe jichanganye uingie kichwa kichwa tu pale utakuja kupigwa ngumi za uso"

"sasa anipige nani mimi kuna mtu namuogopa unadhani halafu mimi nakuambia mambo yangu angalau unipe ushauri wewe ndo kwanza unaniponda ponda wala hunitii moyo sijui upoje Hathra?"

"eeh basi yaishe nilikuwa nakutania tu" Hathra alijibu akatokea rafiki yake mkuu wa siku zote, Lela akamwita na kumtenganisha na yule aliyekuwa amefuatana nae

"vipi Lela mambo yako yameendaje?"
"mimi nashukuru tu sasa hivi yule Maya hayupo tena na mwanamfalme Adrian, hawajafungiwa wote ila nakuwazia wewe tu shoga yangu nasikia jumba bovu limekuangukia wewe eti mwanamfalme Teri ameomba atengenezewe chakula na yule Maya?"

"we acha tu yaani ingenitokea mimi mwenye mali yangu fursa kama hiyo ningejitutumua mpaka jasho la mwisho nihakikishe chakula kinachotoka hapo siyo cha nchi hii, lakini cha kushangaza fursa kama hizo wanazipata akina kajamba nani"

"nawewe umekaa tu umetulia hujafanya jambo lolote lile?"

"nani atulie mie au mtu mwingine, subiri tu kitakachotokea nimeshaharibu huko Maya atajuta kuingia humu ndani ya kasri yaani na kuingilia mapenzi ya watu"

"umefanya fanya nini hebu nipe kaubuyu kidogo namimi nimung'unye" Lela alikaa mkao wa kupewa umbea

"niliingia jikoni wakati anapika nikamzuga zuga ili atoke kisha nikatia chumvi nyingi na mapili pili na unga wa majani mchungu huko alipo Maya anahenya tu hana ujanja nadhani na makofi atapigwa leo"

"duh wewe ni kiboko" Lela alimsifia Hathra

"koh koh" mara wakasikia mtu anakohoa nyuma yao wakashtuka na kugeuka wakamwona mjakazi mwenzao ambae hawampendi kwa sababu haungi mkono vitendo vyao hata mara moja na amemkaribisha Maya vizuri tu, Zasha

"kumbe ndo tabia zenu eeh kuwaharibia watu wengine?" alitikisa kichwa Hathra na Lela wakatazamana kwa aibu kisha wakamtazama Zasha na kusonya, wakaondoka na Zasha akabaki anawatazama tu na kuwasikitikia kwa kitendo chao hicho dhidi ya msichana mgeni asiyewakosea jambo lolote lile, Maya

Upande mwingine mwanamfalme Teri alikuwa ametulia kwenye kitanda chumbani kwake akisubiri chakula alichoagiza apikiwe na Maya

"mwanamfalme Teri!" aligongewa mlango
"nani?"
"ni mimi Hathra"

"unasemaje?"
"chakula tayari unahitajika mezani"
"hapana leo siji mezani nimeshaagiza naletewa"
"au nikuletee mimi huku huku chumbani mtukufu mwanamfalme?"
"nimekwambia naletewa"

"jamani mtukufu mwanamfalme nani anayekuletea uliyempa oda hiyo tena?" Hathra alifungua mlango taratibu ili aingie ndani chumbani kwa mwanamfalme Teri amtege tege kidogo wa mwili wake wenye maumbile ya kuvutia

Lakini kabla hajafanya hivyo

"hodi!" alisikia sauti nyuma yake, alipogeuka kutazama alimwona Maya mlangoni

"pita Maya, Hathra mpishe Maya"
"ooh kumbe ndo huyu uliyemwagiza mtukufu mwanamfalme basi sawa ngoja niwapishe" aliongea huku akitoka mlangoni na kutabasamu kinafiki mbele ya Maya akakaa nje ya chumba,

"mbona umechelewa sana Maya?"

"samahani mtukufu mwanamfalme kulitokea changamoto kidogo ambayo nilifanikiwa kuitatua" Maya alijibu akimwandalia mwanamfalme Teri kisha nae akatoka nje ya chumba akasimama akisubiri mwanamfalme amalize kula ili atoe vyombo na Hathra hakuondoka alibaki amesimama pale pale nje ya chumba akijifanya bize kufagia fagia kwenye korido nia na madhumuni ni kumwona Maya atakavyoaibika na kukaripiwa na kupewa adhabu yoyote na mwanamfalme huyo

"Maya!!" mwanamfalme aliita mudq huohuo zikiwa hazijapita hata dakika mbili

"abee!" Maya akaitika na kuingia chumbani kwa mwanamfalme

"hapa ndipo nilipokuwa napasubiri kwa hamu sana yani" Hathra alitabasamu huku akijiweka vizuri aone kitakachomkuma Maya lakini akashangaa kumuona Maya akitoka huku anatabasamu kwa furaha, akiwa na kijiboksi kidogo cha zawadi mkononi....

*MAYA* 💃

*SEHEMU YA 18*

Hathra alishangaa alipomwona Maya anatoka chumbani kwa mwanamfalme Teri huku akitabasamu kwa furaha na akiwa na kijizawadi mkononi, Hathra akaondoka mbiombio kabla Maya hajamuona kama alikuwa pale amesimama anamtazama...

....

....

Hatimae Kulikucha mapema asubuhi ndani ya kasri la mfalme, wajakazi kama kawaida wapo waliokesha na wapo waliolala, warembo hao wakipokezana kazi kwa zamu, Maya akiwa miongoni mwa wajakazi waliolala siku hiyo, alipoamka moja kwa moja alipewa kazi ya kufanya usafi pamoja na wenzake kadhaa ndani ya kasri sebuleni mapema asubuhi sana, akiwemo Hathra msichana ambae anamchukia sana Maya kwa sasa

"Maya!" Zasha aliyekuwa karibu sana na Maya, wakiivana, alimwita mwanadada huyo wakati wakifagia pamoja
"abee Zasha?"

"kuwa makini sana na Hathra na rafiki zake Maya"
"kwanini Zasha?"
"nimekuonya tu kuwa makini nao"

"sawa" Maya aliitika akitikisa kichwa asijue anachomaanisha rafiki yake huyo

"vipi huna mpango wowote leo Hathra wa kumkomesha huyu mgeni wetu?" Lela alimwuliza rafiki yake

"nina mipango kibao naishiwaje kwa mfano, lakini wewe nawe umesahau ya Adrian Lela, fanya mambo leo mimi wangu ngoja niutafute mpango kabambe" Hathra alimjibu Lela ambae alitikisa kichwa akikumbuka fika kuwa hata yeye yupo kwenye harakati za kumpigania mwanamfalme Adrian ambae anaonekana kumtajataja sana Maya mara kwa mara

Waliyazungumza wakiwa pale pembeni wakimtazama Maya na Zasha ambao walikuwa mita kadhaa nao wakiwa wanafanya usafi

Bi Kalla msimamizi wao mkuu akaja kama kawaida kutazama zoezi la usafi linaloendelea alfajiri ya siku hiyo, akawa anapita pita akimtazama mmoja mmoja

"Maya!"
"abee dada"
"wewe hapo mwachie Zasha nenda kaendelee pale kwenye ngazi kafute nguzo za chuma za ngazi zile"

"sawa dada" Maya alijibu na kutembea haraka haraka kuelekea kwenye ngazi zile, Hathra akamtazama Lela kisha akatazama kichupa cha sabuni alichoshika Lela mkononi mwake, sabuni ya kudekia akampa ishara, Lela akasogea akijifanya anaendelea kudeki mpaka karibu na ngazi ya kushukia chini kisha akanyunyiza sabuni hiyo ya maji wakati Maya akiwa ndo anafika mitaa hiyo hiyo waliokuwepo yeye na Hathra ambayo mbele kuna ngazi kidogo

Maya akiwa hajui hili wala lile akiwa na kitambaa chake cha kufutia mkononi kama kawaida akapita pale pale palipomwagwa sabuni bila kujua akataka kuteleza kwa bahati nzuri akapepesuka tu na kuwahi na kujishikiza kwenye nguzo ya ngazi, Zasha akaona tukio hilo na akawatazama Hathra na Lela akaona wanacheka na kunong'onezana

"Maya kuwa makini!" Zasha alimwambia
"umeumia?" bi Kalla nae alimwuliza

"nipo salama dada sijaanguka" Maya alijibu na kuanza kazi yake ya kufuta futa huku akishuka ngazi taratibu lakini kwa kuwa alishaikanyaga sabuni ile ya maji iliyotaka kumwangusha, viatu vyake vililowana tayari sabuni hivyo akajikuta anateleza tena kwenye ngazi lakini safari hii alikosa pa kujishikia kabisa akaenda mzima mzima kwenye ngazi hizo ndefu

"Mayaaa!" Zasha ndiye aliyekuwa wa kwanza kumwona akapiga makelele na wote wakageuka kumtazama Maya aliyekuwa anaanguka kitambaa akikiachia kikiruka juu lakini kabla hajatua chini ili aporomoke kwenye ngazi hizo alijikuta ameangukia kwenye mikono salama ya mwanaume ambayo ilimzuia asiende chini, alipogeuka na kutazama ni nani huyo aliyemuwahi asianguke na kwenda chini akauona uso wa mwanamfalme Piso akimtazama, huku mikono yake ikiwa imemshika kiunoni

"safari nyingine uwe makini msichana" Piso alimwambia akimwinua

"asante na samahani mtukufu mwanamfalme" Maya alijibu kwa kuona aibu akitazama chini, mwanamfalme akapandisha juu taratibu akiendelea na safari yake, wajakazi wote wakasimama wakiinamisha vichwa vyao wakati akipita akawasalimia, Verda ambae anampenda sana mwanamfalme Piso alimkata jicho kali Maya baada ya kumwona ameshikwa kiuno na kijana huyo

"siku nyingine uwe makini we dada sawa, mtu gani wa kuanguka anguka ovyo kila wakati na kuteleza teleza mbona sisi hatuanguki anguki kama wewe" Verda alikuwa mkali mwanamfalme alipopita tu

"kweli kabisa mvivu huyu"
"ndiyo legelege sana sijui kwanini amekuwa mjakazi" Hathra na Lela na wajakazi wengine walichochea kuni wakimsimanga Maya ambae alikuwa amesimama kiunyonge akiwa ameinamisha uso wake akipokea lawama hizo kutoka kwa wajakazi wenzake, bi Kalla akiwa hayupo ameshaenda zake kabla hata mwanamfalme hajapita

Zasha alimfuata Maya taratibu na kumshika begani mwanadada huyo

"usijali maneno yao Maya kuwa makini tu" alimfariji Maya ambae alimtazama rafiki yake huyo kiunyonge na kutikisa kichwa chake

Upande mwingine kwenye mabanda ya vinyesi vya wanyama alipofungiwa mwanamfalme Adrian, alikuwa amejitandikia nguo yake ya juu (koti) chini amelala akiuchapa usingizi alfajiri ya siku hiyo na ndipo mlango wa banda ukafunguliwa akaingia askari ndani

"mtukufu mwanamfalme!" alimwita lakini aliendelea kuuchapa usingizi ikabidi amfuate kijana huyo na kumtikisa tikisa

"Maya Maya njoo tucheze kwenye maji unakwenda wapii??" Adrian aliongea mwenyewe usingizini huku akitafuna tafuna midomo yake

"mtukufu mwanamfalme??" askari alimpiga piga kijana huyo begani akaona haamki akausogeza uso wake karibu amtazame usoni askari akashangaa anapigwa busu zito la shavuni

"nakupenda Maya mmwaah" Adrian alitabasamu

"mwanamfalmeee!!!" askari huyo aliongea kwa ukali akikasirika kupigwa busu la shavu kama mtoto wa kike na ndipo Adrian alipokurupuka kutoka usingizini akakaa kitako akiwa ametoa macho akamkuta askari amemkazia macho huku akiwa anajifuta shavuni

"saa ngapi saa hizi?" Adrian alizuga "alfajiri saa hizi adhabu yako imeisha mtukufu mwanamfalme" askari aliongea na wala hakumsubiri kijana huyo kwa hasira akatoka bandani akimuachia tu mlango wazi na ndipo Adrian akainuka taratibu na kujikung'uta kung'uta mwilini akiwa amechafuka na siku moja tu amekuwa mweusi akatoka ndani ya mabanda hayo akiwa amemaliza adhabu yake ya siku moja nzima

Alipotoka tu akakutana na mama yake aliyekuwa anakuja hukuhuku mabandani kumfuata kijana wake huyo

"Adrian?!"
"mama?!"

"upo sawa?"
"nipo sawa mama" Adrian alimjibu mama yake huyo ambae alimshika kumkagua akamtazama mikononi akagundua kuna vipele vimeota kwenye ngozi ya Adrian kutokana na mazingira machafu aliyolala na akiwa hajawahi kupitia maisha kama hayo kabla

"ngozi yako imeharibika twende ukamwone daktari haraka"
"hapana mama nipo sawa"
"unajua kesho kutakuwa na nini hapa nyumbani?"

"kesho ni siku yenu ya kuzaliwa kutakuwa na sherehe kubwa haina mfano kwa hiyo wageni waalikwa wakikukuta namna hii utaniaibisha mimi na baba yako" mama yake alimvuta na kuondoka nae haraka haraka...

Wakati huo huo wajakazi wakiwa wanaendelea na usafi, bi Kalla aliwaita wote pamoja wakamfuata kumsikiliza

"nisikilizeni kesho kutakuwa na sherehe kubwa ya kuzaliwa wana wa mfalme pacha wote, Adrian, Piso na Teri kwahiyo itatakiwa mvae mpendeze hamtafanya kazi yoyote kwa sababu watakuja wajakazi wote kutoka kwenye nyumba za mawaziri na wakuu wa majimbo kumtumikia mtukufu mfalme na malkia" aliwaambia wote wakatazamana...

*MAYA* 💃

*SEHEMU YA 19*

Wajakazi wote walishangilia siyo kwa ajili ya sherehe tu ya kesho ila kwa ajili ya kuvaa viwalo vyao baada ya muda mrefu wa kuvaa sare maalumu za wajakazi, tena walipewa kila mtu gauni jipya na kali yakishushwa na askari kila mtu akitakiwa akajaribishe wakaenda na kuanza kujaribisha vyumbani mwao kwenye vioo vyao vya ukutani kila mmoja akiwa anajitazama na kugeuka geuka akimuuliza mwenzake kama amependeza

Maya alikuwa amevaa na yeye gauni lake anajitazama kwenye kioo, akiwa na rafiki yake Zasha

"Zasha umependeza sana"

"yaani kesho ni kutokelezea tu ila Maya rafiki yangu umependeza sanasana lazima mwanamfalme kesho achanganyikiwe" Zasha alimsifia Maya kwa sauti, akina Hathra, Lela na Verda wakasikia na kugeuka waliposikia jina 'mwanamfalme' linatajwa ingawa Zasha hakubainisha ni mwanamfalme gani aliyemkusudia

"mh jamani Zasha nawewe bwana kha"

"unadhani uwongo Maya lakini hizo nywele zako sasa usingezifunga funga namna hiyo ungezifungua na kuziachia mtu umejaaliwa nywele nzuri halafu unazifunga funga hebu" Zasha alianza kumfungua Maya kilemba ambacho mara zote mwanadada huyo hujifunga kichwani na hakitoki kichwani mwake, Maya alikuwa anazifunga ili kuzilinda na uchafu maana hakuwa na uwezo wa kuzihudumia, kwa mara ya kwanza akaziachia nywele zake hizo zilichanua na kuachia kila mjakazi aliyekuwemo akabaki anamtazama

"nyie jamani huyu Maya ni mrembo ana nywele nzuri kweli yaani" mjakazi mmoja alimsifia Maya akiwa yupo na akina Hathra, Verda na Lela, watatu hao wakamgeukia na kumtazama mwenzao huyo kwa macho makali sana

"umekosa stori yoyote zaidi ya hiyo?" Lela alimwuliza

"mh samahanini jamani" mjakazi huyo alijishtukia na kugeuka kuondoka alipoona hakuna anayemuunga mkono kwenye hilo katikati yao.....

......
......

Siku ilipita na hatimae siku mpya iliingia na ndipo wajakazi kutoka kwa waziri mkuu na mawaziri wengine waliingia ndani ya jumba la kifalme pamoja na wasimamizi wao wakuu asubuhi sana kwa ajili ya maandalizi ya mapishi na mambo mengine mengi

Wajakazi wote walikuwa vyumbani mwao wakijipamba kujiandaa tayari kwa ajili ya sherehe ya siku hiyo, kila mtu akiwa mbele ya kioo akihakikisha atakapotoka atakuwa anatazamwa na watu wote kwenye sherehe hiyo

Wageni walianza kuingia kwenye kasri mmoja baada ya mwingine, mawaziri wote na watoto wao wa kike kwa wa kiume akiwemo Waziri Mkuu mzee Gonde na familia yake, akiwemo bintiye Sethi, wakuu wa majimbo, na viongozi wote wa kuu wa nchi na familia zao waliingia ndani ya kasri, mfalme wa nchi ya KUSINI alikuwa amefika na familia yake akapokelewa na mkwewe mtarajiwa, mwanamfalme Teri ambae ni mpenzi wa binti yao Opra ambae miezi michache ijayo wanatarajia kufunga ndoa

"karibuni sana" mwanamfalme Teri akiwa na mama yake malkia Zilpa waliukaribisha msafara wa mfalme wa nchi ya KUSINI ambae ndiye alikuwa mgeni rasmi kwenye shughuli hiyo akiwa mfalme pekee aliyealikwa akaja wengine wote walituma wawakilishi yaani mawaziri wao

"asante mwanamfalme Teri unaendeleaje na mama?" mfalme wa KUSINI alimjibu wakati akishuka kwenye gari na mkewe malkia, Teri badala ya kujibu salamu ya mfalme huyo alikuwa bize kutazama tazama na kuchungulia chungulia ndani ya gari lao

"Teri si unasalimiwa?" mama yake alimkurupusha

"ooh umesema karibuni sana?" Teri alijichanganya, wazazi hao wa Opra wakatazamana na mama yake malkia Zilpa wakiguna

"unamtazama Opra mwanangu Teri?" malkia wa kusini alimwuliza

"ndiyo mama"

"hatujaja nae leo ameshindwa ana sherehe ya rafiki yake amealikwa nchi ya KASKAZINI hajarudi tangu juzi" mama yake Opra aliongea kauli iliyomkata maini' Teri akanyong'onyea sana

Ni miezi imekatika sasa, Teri hajaonana na mpenziwe huyo anayempenda sana, ingawa Teri siyo kijana mwenye msichana mmoja lakini mke wa maisha kwake ni bintimfalme wa nchi ya KUSINI, Opra

Teri siyo kijana anayependa kumuoa msichana ilimradi msichana tu, yeye anayetaka kumuoa ni bintimfalme tu, yaani mtu wa hadhi yake kama yeye mwenyewe, na hilo jambo lilimfanya apendwe zaidi na wazazi wake wote wawili mama yake malkia Zilpa na baba yake mfalme Bono kuliko ndugu zake pacha wenzake, mwanamfalme Adrian na mwanamfalme Piso ambao mmoja yeye amempenda msichana binti wa Waziri Mkuu na mwingine bado haeleweki ataoa lini na mchumba wake ni nani yaani Adrian, yeye akijali zaidi mazoezi ya mapigano kuliko kuwa na mchumba

Teri aliondoka taratibu akiwaacha wazazi wa mchumba wake na mama yake wakisindikizana kuingia ndani ya kasri yeye akaenda taratibu mpaka bustanini akakaa na kujiinamia kimya

Teri yeye sikuzote ni kijana anayependa sifa sana yaani kusifiwa na kuonekana bora kuliko wengine, alitamani mchumba wake Opra aje ili kila mtu auone uzuri na urembo wa msichana huyo uliopitiliza na kila mtu amsifie kwa kujua kuchukua msichana mrembo lakini leo ilikula kwake, Opra hakuja, jambo lililomtia hasira sana alipoona vijana wenzake watoto wa mawaziri wakiingia na wapenzi wao warembo, Teri akainuka kwa hasira na kwenda ndani ya kasri akaingia chumbani kwake na kujifungia kwa ndani akajitupa kitandani na kulala chali akiwa amekasirika na hana hamu tena na sherehe hiyo inayomuhusu yeye mwenyewe na mapacha wenzake wawili, Piso na Adrian, ya siku ya kuzaliwa kwao

Bi Kalla aliingia ndani kwenye nyumba ya wajakazi akawakuta wanaendelea kujipamba na kujiremba Maya akiwa bado hajajiandaa anahangaika na nywele zake kuziweka sawa akisaidiwa na rafiki yake wa karibu Zasha

"muda umebaki mchache wa kuanza sherehe jitahidini kujiandaa mapema"

"sawa dada!" waliitikia mara akaja mjakazi mmoja msaidizi wa. daktari mkuu wa familia ya mfalme akaja na kumnong'oneza bi Kalla sikioni

"mtukufu malkia alikuwa anataka mwanamfalme Adrian atumie chakula cha (...) na atengenezewe dawa ya kuchua ili apone mapele yaliyompata haraka ndani ya lisaa limoja lililobaki, ngozi yake irudi kwenye hali yake ili ahudhurie sherehe yake la sivyo atafanya maamuzi magumu sana, haiwezekani watu wapendeze wajakazi wapendeze lakini mwanamfalme abaki na mapele yake mwilini ni nani anayejua dawa ya kumtibu mwanamfalme kwa haraka atapata zawadi nzuri lakini kama hatojitokeza yoyote yule basi mtaadhibiwa wote" msaidizi huyo wa tabibu (daktari) mkuu wa mfalme alimwambia Maya akisikia pembeni

"mh sasa ni nani atakayeweza jambo hilo kama daktari ameshindwa kumpa dawa mwanamfalme?" bi Kalla aliuliza

"fanya chochote bi Kalla ili kuficha aibu ya mwanamfalme Adrian" mjumbe huyo alimwambia na kuondoka bi Kalla akabaki njiapanda

"dada kuna nini?" Maya aliuliza ingawa alishasikia

"mambo mazito Maya huyawezi"

"nipo tayari kumtibia mwanamfalme Adrian dada"

"Maya hii kazi haikuhusu wewe wala wenzako hapa ni kwenda nje kutafuta Tabibu mzuri wa kumtibu mwanamfalme Adrian lasivyo kaka yangu Tabibu mkuu atapewa adhabu kali kwa kushindwa kumtibu mwanamfalme"

"nitamtibia mimi dada naomba uniombee ruhusa kwa mtukufu mfalme na malkia"

"Maya??!!"
"nipe nafasi dada!" Maya alisisitiza kauli yake hiyo....

*MAYA* 💃

*SEHEMU YA 20*

Mjakazi mkuu na msimamizi wa wajakazi wote bi Kalla alimtazama Maya kwa umakini na akimlinganisha jinsi alivyo na maneno anayojaribu kumwambia

"Maya!"
"abee dada?"
"una uhakika na unayoyasema?"
"ndiyo dada"
"umesomea wapi utabibu huo?"
"nilifundishwa na marehemu babu yangu wakati nikiwa mdogo"
"sasa wakati ukiwa mdogo mpaka leo?"

"unaweza kunijaribu kwanza dada?"
"sawa twende ukaonyeshe hiyo dawa unayoijua ambayo tabibu aliyesomea utabibu miaka mingi ameishindwa na wewe ukaweza au unadhani ni vipele vya kawaida tu vilivyompata mwanamfalme Adrian, hivi vya joto, tetekuwanga sijui na ukurutu?"

"dada nipe nafasi"

"sawa ngoja tuone" aliinua mabega juu akimaanisha hana cha kupinga wakaanza kufuatana kuelekea ndani ya kasri wakafika mpaka sebuleni wakamwona malkia Zilpa akiwa kwenye korido ya chumbani anatembea tembea hana amani kabisa na hali ya kijana wake ambae upele wa ajabu umemtoka alipotoka kula mabandani, ulianzia kwenye mikono ukaanza kusambaa mwili mzima

"mbona unarudi mwenyewe Kalla umemkosa tabibu yeyote huko ambae ataweza kumtibu mwanangu ili atoke chumbani kwake na kuhudhuria sherehe bila fedheha yoyote?"

"nimekosa mtukufu malkia ila..." kabla hajamalizia sentensi yake walikuja matabibu kumi walioitwa ndani ya kasri kwa amri ya mfalme ili wamtibie mwanamfalme Adrian upele uliomkumba wa ajabu ajabu

"mtukufu malkia tunaomba samahani tumeshindwa kulifanya zoezi"

"matabibu wote mmeshindwa kulifanya zoezi hilo dogo?"
"siyo vya kawaida vile vipele inaonekana ni laana iliyompata kutoka kwa miungu"

"laana kivipi mwanangu amelaaniwa mtoto wangu mwanamfalme?"

"samahani mtukufu malkia"
"askari wakamateni hawa kawafungieni maana wameshindwa kazi wanaanza kumtukana mtoto wangu"

"tusamehe mtukufu malkia hatujamaanisha hivyo tafadhali" waliogopa wazee hao wakimsihi mama huyo asiwatie kifungoni

"mtukufu malkia tafadhali usiwafunge kwanza mwache mtu mmoja ajaribu kumtibia mwanamfalme Adrian"

"mtu gani atakaeweza kuiondoa fedheha ya mwanangu, yupo wapi huyo mtu mbona hujaja nae Kalla au ndiye wewe huyo mtu?"

"hapana ni huyu hapa" Bi Kalla alimshika mkono Maya

"nani?"
"Maya"
"Maya yupi?"
"ni mimi hapa mtukufu malkia naweza kupata dawa ya kumtibia mwanamfalme Adrian na akapona ugonjwa wake wa ngozi"

"hahaha Kalla umeishiwa cha kuniambia au mbona unanichekesha?"

"kwanini mtukufu malkia ni kweli ninaweza"
"wewe ni Tabibu?"
"hapana mtukufu malkia"
"utafanyaje fanyaje hebu nieleze eleze kidogo njia utakayotumia" malkia alimwuliza Maya ambae kabla hajajibu swali hilo la malkia Zilpa akamtazama kwanza bi Kalla aliyekuwa ametulia kimya baada ya kugombezwa na malkia

"nitatumia mate yangu mtukufu malkia"
"mate yako?"
"Maya umesema nini utatumia mate yako?" malkia Zilpa na bi Kalla wote walimtazama Maya kwa mshangao kutokana na kauli yake hiyo ya kutatanisha

"ndiyo mate yangu mtukufu malkia"
"naona Kalla umeamua kuniletea watoto sasa wanitanie hapa ili wapandishe hasira yangu vizuri"

"samahani mtukufu malkia sikuyajua haya, Maya twende" alimshika mkono Maya ambae aliwatazama kwa unyonge malkia Zilpa na bi Kalla ambao alijua wanahitaji msaada wake sana lakini ni wabishi tu na wasiomwamini kabisa

"mwacheni kwanza huyo binti tuone kama anachotaka kukifanya kitafanikiwa na kisipofanikiwa akamchafua tu mwanangu nitamkata kichwa chake na kukitundika kwenye mti" walisikia sauti nyuma yao wakatazama, hakuwa mwingine ila mfalme Bono

"mume wangu mfalme lakini..."
"acha tuone mke wangu sikuzote penye uwongo hujitenga, nenda binti unahitaji nini na nini?"

"nahitaji tu maji kwenye kibakuli asali mbichi kwenyd chupa ndogo"

"mpatieni" mfalme aliwaagiza askari wakaleta vitu hivyo viwili tu alivyotaka Maya

"mume wangu unamwamini huyu msichana?"
"ni kwa ajili ya mtoto wetu na asipofanikisha alilolisema atapata adhabu mara mbili zaidi ya aliyoipata aliyopewa hapo awali, si nyingine ila ni kifo" mfalme aliongea na kuondoka taratibu akiwaacha watatu hao wanatazamana

"unaweza kuanza zoezi lako sasa" malkia Zilpa alimwambia Maya ambae alimtazama bi Kalla ambae alibaki anamtazama Maya kwa macho ya huruma akiijua amri ya mfalme huwa haitenguliwi akisema amesema

Askari wakamletea Maya kila alichokitaka, bakuli la maji, asali mbichi, unyoya, Maya akaomba aingie chumbani kwa mwanamfalme Adrian peke yake bila mtu yeyote, akaruhusiwa kishingo upande na mama huyo

Mambo yaliendelea kimya kimya huku wageni wakimalizika kuingia ndani ya kasri la mfalme kwa ajili ya shughuli kubwa ya sherehe, wakiwa hawajui kinachoendelea kwa mwanamfalme Adrian, mwanamfalme Piso alikuwa yupo na mchumba wake Sethi huku mwanamfalme Teri akiwa bado yupo chumbani mwake amekasirishwa na kutokuonekana kwa mpenziwe Opra kwenye sherehe hiyo kubwa ya kuadhimisha kuzaliwa kwao, hata alipogongewa mlango na wajakazi hakufungua mlango maana walikuwa wamemletea nguo zake ikabidi waende kumuita mama yake, malkia Zilpa ambae alikuja kujaribu kumgongea mtoto wake huyo lakini wala hakufungua mlango

Dakika zilisogea nje ya chumba cha mwanamfalme Adrian hakuna aliyetoka, siyo Maya wala mwanamfalme Adrian mpaka mjakazi mkuu bi Kalla na malkia Zilpa wakaingiwa na wasiwasi lisaa lizima lilivyopita

"naenda kuingia" malkia aliongea lakini bi Kalla akamshika mkono kumzuia asiingie

"hapana mtukufu malkia subiri inawezekana ukaenda halafu ukaharibu tiba na ndiyo ilikuwa kwenye kumalizikia" bi Kalla alimtuliza malkia huku na yeye akiwa amejawa wasiwasi mkubwa, malkia Zilpa akatulia kama dakika kumi nyingine tena alipoona kimya akachomoka haraka kwenda kuingia chumbani kwa mtoto wake Adrian lakini kabla hajafika mlango ulifunguliwa na Maya alionekana amesimama mlangoni huku amelegea kisha akaanguka chini mzima mzima

"Maya!!" bi Kalla alimkimbilia pale chini lakini malkia Zilpa akamruka Maya na kuingia chumbani kwa mtoto wake mpaka kitandani akamkuta amelala usingizi mzito

"Adrian Adrian umefanyaje tena?" alijaribu kumtikisa tikisa na bi Kalla akaingia muda huo huo

"mtukufu malkia ngozi ya mwanamfalme Adrian imerudi kama kawaida hakuna mapele wala nini mtazame" bi Kalla alimwambia malkia Zilpa akamtazama Adrian mtoto wake akakuta kweli ngozi yake imekuwa nyororo kama awali

"lakini mbona sasa mwanangu haamki tena??"....

*Poleni, nimefanikiwa kurudi kule Facebook, Msiolipia Tsh1000 namba ya malipo 0626363334 Halopesa jina Neema*
*MAYA* 💃

*SEHEMU YA 21---25*

"koh koh koh!" mwanamfalme Adrian alikohoa kitandani huku akiwa anatazamwa na mama yake malkia Zilpa na mjakazi mkuu bi Kalla

"unajisikiaje mwanangu?"
"najisikia vizuri mama, mbona mwili wangu umerudi kwenye hali yake ya kawaida?"

"ni Ma.." bi Kalla alitaka kumtaja Maya lakini malkia Zilpa akamkata jicho akimzuia asizungumze chochote kuhusu msichana huyo waliyemwacha akiwa amelala pale chini mlangoni

"kama una nguvu amka mwanangu ujiandae sherehe imekaribia kuanza kama hauna basi pumzika pumzika kidogo"

"usijali mama nipo vizuri"
"mwondoe Maya hapo mlangoni"
"sawa mtukufu malkia" bi Kalla aliitika na kutoka chumbani humo na kumkuta Maya bado amelala chini, ambae alimsogeza pembeni hapo awali

"aaaachyaaa!" Maya alipiga chafya na kufumbua macho
"Maya upo sawa?"
"nipo sawa!" Maya alimjibu huku akikaa kitako...

Upande mwingine wageni wameshaingia ndani ya kasri tayari kwa ajili ya sherehe hiyo kubwa ya siku ya kuzaliwa kwa watoto watatu pacha wa mfalme

Aliyeonekana ni mwanamfalme Piso tu akiwa ameambatana na mpenziwe Sethi, lakini wana wawili wa mfalme, mapacha wenzake Teri na Adrian hawakuonekana, jambo hilo likaanza kuzua minong'ono ya chini chini kila mtu akiongea lake

"wako wapi shemeji Adrian na shemeji Teri mpenzi?" Sethi alimwuliza Piso "sijajua nini kinaendelea ngoja nikawatazame"

"hamna usiniache peke yangu twende" Sethi alimshika mkono Piso wakaongozana wote watatu kwenda kuwatazama ndugu zake wawili Teri na Adrian

"Mh!" mjakazi Verda alibaki amekunja mdomo ameubinua akimtazama mwanamfalme Piso na mpenziwe Sethi

"vipi shoga?" Hathra alimwuliza

"kwani huoni kule Hathra kinachoendelea, mahaba mahabani kati ya mwanamfalme Piso na kale kadada kwa hiyo Verda haki yake kabisa ateseke" Lela aliongea wakiwa wameshaingia sebuleni na magauni yao mazuri huku wakiwa wamejipamba wajakazi hao kama siyo wao huku wakiwa na glasi za mvinyo mikononi

"wala siumii chochote naona wananichefua tu"
"aah wapi Verda lazima uumie usitupwage hapa, chezea mapenzi wewe, mapenzi hayanaga baunsa au nadanganya Hathra?"

"yaani hapa mnanichanganya tu wewe na Verda, sijamwona mwanamfalme Teri alivyopendeza leo sasa sijui kama nitakuwa na amani sijui anaumwa,, mpenzi wangu yule jamani?"

"wewe kama mimi Hathra, mwanamfalme Adrian nae simuoni mpaka saa hizi sijui hata ana tatizo gani?"

"bora msiowaona kabisa hao watu wenu kuliko mimi niliyemwona halafu yupo na jitu hata halieleweki kichwa kipo wapi miguu ipo wapi"

"mh Verda unataka kutudanganya kuwa wewe na yule Sethi wewe ni mrembo zaidi yake?"

"wewe unanionaje Hathra, nitazame huyo Sethi anaingia mara ngapi kwangu kwa unavyoniona?"

"mwanamke kujiamini ila pale kwa Sethi wala Verda asikudanganye Hathra, msichana mrembo sana yule ila cha kufanya ni kumkomesha tu Verda usizubae zubae" Lela aliongea wakiwa wamesimama pamoja wajakazi hao watatu

"tazameni kule?!" Verda aliwaambia wenzake wakatazama na kumwona Maya kwa mbali akiwa na sare zake zilezile za kijakazi akiwa ameongozana na bi Kalla wakitoka nje kupitia mlango wa mbele mdogo kimya kimya

"yaa,ni mngejua hilo jina ninavyolichukia wala msingelitaja taja" Lela alijibu

"kama kawaida kujifanya mpole sijui kimefanya nini.   huko hata mimi nakachukia sana" Hathra nae alichangia, mada na muda huo huo wakamwona mwanamfalme Adrian akiwa anakuja amevaa mavazi mapya ya kofia nzuri kichwani kila mtu akamwangalia"!Hathra na Verda wakamshtua Lela aliyekuwa amezubaa anatazama upande mwingine, mjakazi huyo akageuka na kumwona mwanamfalme Adrian

"Adrian jamani waooooh" aliropoka kwa sauti kwa sababu ya furaha aliyoshindwa kujizuia watu wakamsikia na kumgeukia, wenzake Hathra na Verda wakamfinya akaziba mdomo akibaki ametoa macho tu baada ya kuropoka tu bila breki

Mwanamfalme aliienda na kukaa mpaka kwenye kiti chake akatulia akiangaza kulia na kushoto na ndipo alipowaona Verda, Hathra na Lela wanamwangalia akamwita mmojawapo lakini kwa sababu wanamjua Lela kuwa anampenda sana wakakajua moja kwa moja aliyeitwa au anayepaswa kwenda ni Lela wakamsukuma aende akaenda huku akicheka cheka wenzake wakabaki wanamkonyeza konyeza akafika mpaka kwa mwanamfalme Adrian ambae alimwita amsogezee sikio ili amnong'oneze sikioni

'Lela alijiona yupo kwenye dunia ya kwake, dunia ya mahaba akiwa na mwanamfalme Adrian kwenye bwawa la kuogelea, kijana huyo akiwa na taji ya kifalme kichwani na Lela akiwa na taji ya kimalkia kichwani, akiwa amekumbatiwa kwa nyuma na kijana huyo

"mpenzi wangu Lela na malkia wangu" mwanamfalme alimwita Lela akiwa amemkumbatia kwenye maji

"abee baba, kipenzi changu Adrian na mfalme wangu wa moyo"

"natamani nikuambie jambo zuri na nikubusu shavuni"

"niambie kipenzi" Lela aliitika na kusogeza shavu lake mwanamfalme Adrian akasogeza midomo yake ili ambusu kwanza mwanadada huyo'

"Maya mbona simuoni yupo wapi?" swali hilo lilimtoa Lela kwenye mawazo na ndoto aliyokuwa anaiota huku akiwa amesimama alipoambiwa anong'onezwe

"abee?"
"Maya yupo wapi mbona simuoni?"
"sijajua, aliondoka na bi Kalla"
"sawa waweza kwenda"

"sawa mtukufu mwanamfalme" Lela alijibu na kurudi kwa wenzake akiwa amenyong'onyea kweli na amekasirika baada ya kuulizwa swali asilolitarajia na kutajiwa jina asilolipenda

Upande mwingine Piso alikuwa mlangoni kwa Teri akimgongea ndugu yake huyo bila mafanikio maana alijifungia kwa ndani, Piso akaona isiwe tabu akatoka kwa nje kupitia dirishani na kuingia chumbani kwa ndugu yake huyo kupitia dirishani na kumkuta amelala kitandani

"Teri unaumwa?"
"umefuata nini chumbani kwangu Piso?"

"sijakuona sebuleni nimekuja kukutazama kama una tatizo"

"nipo sawa unaweza kwenda ukasherehekee"
"nawewe je?"
"sijisikii leo"
"lakini hautawatendea haki baba na mama mbele ya wageni waalikwa"
"wewe na Adrian mnatosha kuwatendea haki"

"yote haya ni kwa sababu Opra hajaja?"
"Piso niache!" Teri alimwambia ndugu yake huyo akiinuka kitandani na kusogea mpaka dirishani

"lakini Teri mimi ni ndugu ya... "

"Maya???!!!" kabla Piso hajamalizia sentensi yake Teri aliongea huku akiwa anashangaa kinywa kikiwa wazi akitazama chini nje maana walikuwa chumba cha juu dirishani, Piso nae akasogea wakamwona msichana huyo akiwa amevaa gauni lake refu la kupendeza na nywele zake ameziachia akiingia ndani wote wakabaki wamesimama dirishani wakimtazama....

*MAYA* 💃

*SEHEMU YA 22*

Msichana Maya alipita chini nje akiingia ndani akiwa hajui kuwa juu wanamtazama wana wa mfalme wawili, Teri na ndugu yake

"yule msichana ni nani?" Piso aliuliza
"Maya kwani hujasikia au humjui au?"
"Maya yule msichana niliyem.."
"ngoja nijiandae tangulia Piso nakuja sebuleni"

"umebadili mawazo mara hii?"
"ndiyo!"
"kwanini?" Piso alimwuliza Teri ambae hakumjibu chochote, Piso akainua mabega tu akiguna na kutoka akimwacha nduguye huyo akiwa anajiandaa nae aje sebuleni ambapo ndipo sherehe inafanyika

Adrian macho yake hayakutulia alibaki anaaangaza angaza, kama atamuona Maya mpaka mama yake akamwona na kumtazama akamshika mkono akimzuia alipotaka kuondoka wakati huo baba yake mfalme Bono ndiyo alikuwa anakuja akitokea chumbani kwake ili afungue hafla hiyo sherehe ianze rasmi, watu wote wakasimama (kwa heshima) mfalme Bono akakaa kitako kwenye kiti chake akipokelewa na mkewe akiwa ameongozana na mgeni wake mfalme wa nchi ya KUSINI walipokaa ndipo sherehe ikafunguliwa rasmi na mlango ukiwa umeshafungwa tayari Maya akiwa ndiye mtu wa mwisho kuingia na hakuruhusiwa mtu mwingine yoyote kuingia ndani ya sebule na ukumbi huo mkubwa wa kasri la mfalme

Maya aliingia akitembea kwa wasiwasi akihofia viatu vyake virefu alivyovaa akiwa hajavizoea watu waliosimama aliowapita wakimtazama hasa wanaume, akiwa amelishikilia gauni lake refu akihofia kulikanyaga macho ya watu wengi yakimwangalia mwanadada huyo mrembo sana mwenye nywele ndefu na nzuri za kuvutia akiwa kwenye mavazi asiyoyazoea

Mwanamfalme Adrian alibaki amekodoa macho akimtazama mwanadada huyo wakati anakaa kwenye kiti huku watu wakiendelea kunong'ona wakiulizana alipo mwanamfalme Teri ambae mpaka sasa hajaonekana kwenye sherehe

"mh!" Hathra aliguna akiwatazama wenzake wawili aliokaa nao

"kama kawaida bi fulani ameshaingia sasa anajitembeza ili watu wote wamtazame yeye" Lela aliongeza
"sijui ni mshamba wa kuvaa vizuri umeona anavyotetemeka akitembea?" Verda aliongeza wakageuka na kumtazama kwenye meza ya nyuma aliyokaa, Maya akatabasamu na kuwapungia mkono akiwa amekaa na Zasha rafiki yake nao wakampungia mkono

"umependeza sana Maya tazama watu walivyokutazama ulivyoingia" Zasha alimsifia

"mh Zasha yaani mimi nikuzidi wewe kupendeza hiyo haiwezekani"

"siwezi kukudanganya Maya yaani leo umependeza sana"

"samahani kuna mtu hapa?" kijana mmoja aliuliza alipowakuta Maya na Zasha wamekaa na kiti cha pembeni cha Maya kikiwa hakina mtu

"hakuna mtu kaa Tu" Zasha alimjibu kijana huyo akakaa huku akitabasamu, macho yote yakiwa kwa Maya

"naitwa Odri sijui unaitwa nani mwenzangu?" alimnyooshea mkono Maya kumsalimia

"naitwa Maya!" alijibu akimpa mkono wakatazamana akaushika mkono wa Maya na kuubusu kiganjani kisha akampa mkono Zasha ila juu juu tu siyo kama Maya aliyemshika kwa dakika kadhaa

"waooooh Maya jina zuri kama ulivyo uzuri wako mrembo"
"asante sana" Maya alitabasamu

"unanifahamu?"
"hapana sikufahamu"
"eti dada wewe unanifahamu maana nakukutaga hapa" kijana huyo alimwuliza Zasha

"nakufahamu wewe si mtoto wa Waziri Mkuu nakufahamu nilikuona mara moja "

"hujakosea mimi ni mtoto wa Waziri Mkuu nashangaa Maya eti hanijui, wewe Maya ni mtoto wa Waziri yupi na umekuja na wazazi wako au umekuja mwenyewe tu?" Maya aliulizwa akamtazama Zasha huku mwenzake huyo akijizuia na kutaka kucheka na Maya nae akajikuta anacheka tu maana swali hilo halikulingana nae hata kidogo

"Maya mbona unafurahi niambie tu wewe ni mtoto wa Waziri gani na kwanini umekaa hapa na wajakazi tu badala ya kwenda kukaa na wazazi"

"mimi siyo mtoto wa Waziri yeyote mimi ni mjakazi tu humu ndani ya kasri samahani"
"Maya unataka unidanganye sasa mrembo kama wewe unasema siyo... "

"hivi wewe Odri meza zote hujaziona kule za watoto wa mawaziri na wazazi wao mawaziri mpaka unakuja kukaa na wajakazi hapa una akili kweli wewe?" Sethi alimnong'oneza ndugu yake huyo lakini kwa sauti, Maya na Zasha wakimsikia

"jamani si nimekuja kusalimia tu mrembo mmoja tu hapa dada?"

"hebu inuka inuka watu wote wanakushangaa hebu fichaga tabia yako nawewe" Sethi alimshika mkono watu wakiwatazama, Odri akainuka kwenye kiti taratibu na kumbusu Maya hewani

"nitakutafuta mrembo" alimwambia mwanadada huyo wakati huo mwanamfalme Teri alikuwa ndo anakuja kwenye sherehe sebuleni akitokea chumbani kwake akaona kinachoendelea kwa Maya na mwanamfalme Adrian akaona nae kinachofanyika kwa Maya akawa anasaga meno akitamani akamtwange ngumi kijana huyo, mwanamfalme Piso alikuwa kimya ametulia ndipo Sethi akarudi alipokaa nae na kumuweka weka vizuri nguo yake mchumba wake huyo

"kilikuwa kinaendelea nini pale?" Piso alimwuliza Sethi
"Odri shemeji yako aliacha meza yake na kwenda kukaa na mjakazi yule pale mtu asie na hadhi yake"

"unaweza kutumia lugha rafiki ukamuheshimu kidogo huyo mjakazi?"

"Piso?!!" Sethi alimshangaa Piso ambae hakutaka kusema neno jingine lolote akavuta glasi yake ya juisi na kuanza kuishusha kinywani taratibu ikiteremka mpaka kooni kumbe nae aliona kinachoendelea

Malkia alikaribishwa ili azungumze jambo la kushtukiza (surprise) aliyoiandaa kwa watoto wake yaani zawadi, akainuka na kuanza kuongea

"karibuni sana wageni waalikwa ndani ya nyumba yangu na mume wangu mtukufu mfalme leo nina zawadi ya kwanza kabisa kwa mtoto wangu aliyetoka tumboni mwangu wa kwanza kabla mapacha wenzake wawili hawajafuata yaani mwanangu Piso, naomba niletewe hiyo zawadi" malkia aliagiza akaletewa kidubwana kidogo kilichofungwa kwenye boksi zuri la zawadi, mwanamfalme Piso akiwa anatazama kwa umakini huku amesimama na mpenziwe Sethi, kwa heshima akasogea mpaka kwa mama yake na kupokea zawadi hiyo aliyotakiwa kuifungua akaifungua taratibu na kukutana na pete nzuri ya dhahabu

"mama ya nini hii?" alimwuliza mama yake
"kwa ajili ya Sethi mchumba wako tunataka leo umvishe pete rasmi ya uchumba na maandalizi ya harusi yaanze mara moja ifungwe ndoa yenu siku yoyote kuanzia sasa" malkia Zilpa aliongea watu wote wakashangilia na kupiga makofi akiwemo mfalme Bono mwenyewe, Sethi akiwa amesimama amejishika mdomo kwa mshangao, mwanamfalme Piso akaitazama pete hiyo na kumtazama mama yake kisha akamtazama Sethi mpenziwe aliyetamani kumuoa na aliyepambana ili wazazi wake wamkubali binti huyo mrembo mpaka wakamkubali

Cha ajabu badala ya Piso kwenda kumvisha Sethi pete hiyo akaishika na kuirudisha kwenye kiboksi chake kisha akamrudishia mama yake....

*MAYA* 💃

*SEHEMU YA 23*

Watu wote walibaki wakimtazama mwanamfalme Piso ambae badala ya kwenda kumvisha pete hiyo ya dhahabu mwanadada mrembo Sethi, mpenziwe kama walivyotarajia badala yake aliirudisha kwenye kiboksi chake na kumrudishia mama yake

"unafanya nini Piso mbele ya wageni na mbele ya baba yako?" mama yake alimwuliza akimshangaa sana na hata Sethi mwenyewe alimshangaa mpenziwe huyo huku akiwa amesimama vile vile, watu wakianza minong'ono ya chini chini

"afadhali uuuwiii maana moyo nilihisi unachomoka yaani dah siyo kwa tukio lile" mjakazi Verda alishusha pumzi ndefu akiwaambia wenzake, Hathra na Lela aliokaa nao

"itakuwa mchawi wewe Verda umeroga nini watu wasivalishane pete leo?" Lela alimwuliza

"lazima atakuwa ameroga huyu kwa bibi yake maana haiwezekani litokee tu hivihivi, utufundishe na siye basi na akina Teri wetu" Hathra nae alimwambia

"ndo mtajua hamjui sasa" Verda aliwajibu huku akicheka huku wakiendelea kufuatilia kujua kitakachojiri baada ya hapo

"samahani ndugu na wageni waalikwa kwa sasa sipo tayari kwa tukio hili, samahani baba, samahani mama nilishaandaa tayari kitu kwa ajili ya mpenzi wangu Sethi hiki naomba nimvalishe siku ya harusi yetu na kile cha kwangu ndiyo nimvalishe siku niliyoipanga kumvalisha lakini siyo leo, aliongea kaa sauti wakampigia makofi lakini minong'ono ikiendelea chini kwa chini"

"sawa kama mlivyomsikia kijana wetu subirini muone atakachokifanya siku chache zijazo, hii tunaitunza kwa ajili yao na namrudishia yeye mwenyewe Piso aitunze kwa ajili ya tukio lao tuendelee kula na kunywa" malkia Zilpa aliongea akitabasamu huku akimtazama mumewe mfalme ambae hakuzungumza neno alikuwa anatikisa fimbo yake ya dhahabu tu akiwa kimya anatafakari jambo

Mwanamfalme Piso alirudi mpaka pale alipokaa na Sethi mpenziwe awali akamkuta mwanadada huyo akiwa amekasirika uso amegeuzia pembeni

"samahani Sethi nina maana kubwa kufanya nilichokifanya najua kwanini sijakufanyia sasa, usinielewe vibaya nimeandaa kikubwa zaidi ya hiki" Piso alijiongelesha tu mwenyewe bila kujibiwa chochote, Sethi alikuwa wala hamtazami tena

Malkia Zilpa alitoa zawadi za pete za dhahabu ya thamani kubwa kwa watoto wake wawili Teri na Adrian kisha akaruhusu muziki uendelee, watumbuizaji maalumu wakaitwa mbele na kuanza kutumbuiza huku Piso akitakiwa acheze na mpenziwe Sethi, Adrian akitakiwa acheze na mwanadada yeyote yule ambae atamchagua na Teri hivyo hivyo

Mfalme Bono kusimama na mkewe malkia Zilpa walikuwa wa kwanza kusimama kuufungua muziki huo wakicheza huku wameshikana na ndipo mwanamfalme Piso akafuata sambamba na mpenziwe Sethi wakaanza kucheza na wageni waalikwa wakasimama na wenza wao wakaanza kucheza na wake zao wengine wachumba wao wawili wawili kama sehemu ya tamaduni za nchi hiyo

Mwanamfalme Teri alichungulia huku na huku akaona ndiyo fursa iliyobaki akapita pita ili amuone Maya lakini alipokuwa anakatiza katiza tu kumtafuta Maya ili acheze nae akakutana na mwanadada mmoja mtoto wa Waziri mmoja aliyemvuta mkono na kumweka kifuani mwake

"halow mwanamfalme ni siku nyingi hatujaonana" mwanadadq huyo alitabasamu huku akitazamana na Teri ambae hakuwa na mpango wa kucheza nae

"Merita?"
"ndiye mimi umenisahau"

"siwezi kukusahau mbona umepotea sana mrembo uliamua kuhamia hukohuko ulipokuwa unaposoma?" alimwuliza akiwa amemshika kiuno mwanadada huyo kwa mikono miwili huku mwanadada huyo akiwa amemshikilia mabegani

"baba alitaka niongeze miaka mingine lakini nikakataa nikasema lazima nirudi nyumbani"
"kwa ajili yangu mimi au?"
"hapana kwa ajili ya Adrian"
"sawa niache basi niendelee na safari yangu Adrian yule pale anakuja" mwanadada huyo alimwambia Teri wakati Adrian akija

"nataka unishike kiuno na kunitazama kimahaba zaidi ili Adrian ajisikie wivu kwa ajili yangu"

"sawa haina shida ila kwa dakika chache tu kwa sababu kuna mtu namuwahi"

"ni nani tena mbona Opra sijamwona?"
"hajaja"
"sawa!" Merita alijibu na kujibinua zaidi walipomwona Adrian akija kwa sababu ni rafiki mkubwa wa Merita na mwanadada huyo anampenda sana Adrian alifanya hivyo kwa makusudi akijaribu kumfanya Adrian ajisikie wivu

Adrian alipowakaribia ndo kwanza alimpungia mkono tu mwanadada huyo ambae hawajaonana muda mrefu sana kisha akawapita akiendelea na safari yake akionekana kama kuna mtu anamtafuta

"kazi yangu imeisha Merita inaonekana kama Adrian ameshakuona lakini hajajisikia chochote naweza kuendelea na safari yangu sasa?" Adrian alimwuliza mwanadada huyo ambae pia wana undugu nae wa mbali

"mmh!" Merita aliguna akimtazama Adrian anapoelekea

"mfuate tu sasa tumia fursa" Teri alimjibu mwanadada huyo na kumyachia akaendelea na safari yake ya kumtafuta Maya wakati huo huo kumbe Adrian nae alikuwa anamtafuta Maya

Wajakazi Hathra, Verda na Lela walikuwa wanacheza wenyewe huku wakitazama tazama wakawaona mwanamfalme Teri na mwanamfalme Adrian wakija huku huku walipo

"haya wenzangu wenye bahati zenu fursa hizo jibebisheni kwa wanamfalme hao mimi wangu ndo ameng'ang'aniwa na jitu lake kule nakereka" Verda aliwaambia wenzake hao ambao walianza kujiweka vizuri magauni yao na nywele zao ili wawadake Adrian na Teri walipowaona wanakuja hukuhuku walipo

"yaani mimi nataka nimshike mwanamfalme Adrian mabegani nimkumbatie, nimtazame kwa jicho la mahaba nimwambie nakupenda mwanamfalme nipo tayari kuwa malkia wako" Lela aliongea akifanya mazoezi ya kucheza pale atakapomfuata mwanamfalme Adrian

"mimi nishaanza kuogopa mwenzenu hivi mwanamfalme kwa mfano akija kweli na kuniomba tucheze maana ananitaniaga taniaga sana si nitazimia jamani Teri wangu uuuwiii nahisi mapigo ya moyo yameanza kunienda mbiombio"  Hathra aliongea akijishika kifuani upande wa moyo

Maya akiwa hajui ili wala lile alikuwa na Zasha wameshikana mikono wanacheza tu huku wanaongea

"mbona mwanamfalme Adrian na mwanamfalme Teri wanakuja huku, wanakutafuta wewe nini?" Zasha alimwuliza Maya alipomwona mwanamfalme Adrian na mwanamfalme Teri wakija kila mmoja akitokea njia yake

"mimi tena mh umeshaanza Zasha mambo yako?" Maya aligeuka kutazama kama anachokisema Zasha kina ukweli ndani yake ndipo akamwona mwanamfalme Adrian

"Maya!!" mwanamfalme Adrian alimuita na kuanza kuja mbiombio alipomwona

"nimekwambia mimi" Zasha aliguna na kuanza kurudi nyuma kidogo kidogo ili ajitenge na Maya ni kama alishajua kitakachofuata

Maya akageuka kulia na kumwona mwanamfalme Teri akija nae wakaonana uso kwa uso

"Mayaaa nilikuwa nakutafuta" mwanamfalme Teri nae aliongea akija mbiombio akiwa hajamwona ndugu yake Adrian na wala Adrian akiwa hajamuona ndugu yake Teri...

*MAYA* 💃

*SEHEMU YA 24*

Maya alibaki anawatazama mwanamfalme Adrian na mwanamfalme Teri wakati wakija wakimfuata na wote wakimwita huku wakiwa hawajaonana bado akabaki anashangaa

Akina Hathra, Lela na Verda walikuwa wamesimama wakiusubiri ugeni huo wa mwanamfalme Teri na mwanamfalme Adrian wakiwa wamejiandaa kuwapokea vijana hao watanashati wakijua wanakuja kwao lakini walishangaa akina kaka hao wote wakimwita mwanadada mmoja, Maya, tena wakiwapita wao kwenye meza yao,  Teri na Adrian walionana lakini hawakusikiana walivyoliita jina moja hivyo hakuna aliyejua kati yao kama wanayemfuata ni mtu mmoja

"nilijua tu ni lile lidada ligeni tena" Verda aliongea

"yaani nalichukia, sijui kwanini limekuja ndani ya kasri humu yaani shida tupu" Lela nae alichangia mada huku akikaa kwenye kiti chake kwa hasira

"yaani mimi hata siongei neno nahisi kumpiga mtu hapa" Hathra aliongea akikataa hata kugeuka nyuma kutazama kinachoendelea

Maya alibaki ametoa macho tu wakati wawili hao wakija upande aliopo lakini walipokaribia kabla hawajamfikia kabisa akatokea Odri, mdogo wa Sethi mtoto wa Waziri Mkuu

"mrembo naweza kucheza na wewe tafadhali?" alimwuliza huku akimnyooshea mkono, Maya akageuka na kumtazama Zasha aliyekuwa amerudi nyuma mita kadhaa akamkonyeza akimwonyesha ishara kuwa akubali kucheza na kijana huyo

"bila shaka!" Maya alimpa mkono kijana huyo ambae aliushika na kuubusu kwenye kiganja kama kawaida akamshika Maya na kumvuta pembeni waliposimama watu wengine wanaocheza muziki akapitisha mkono wa kuume kiunoni mwa mwanadada huyo huku Maya akiupitisha mkono wake mabegani mwa kijana huyo wakaanza kucheza taratibu wimbo uliokuwa ukiimbwa mubashara (live) na watumbuizaji waliokodiwa maalumu kwa ajili ya kutumbuiza wakiwa ni wanamuziki mashuhuri ndani ya nchi hiyo ya TSALA

Mwanamfalme Adrian aliliona tukio hilo la Maya kuchukuliwa mbele yake na mtoto wa Waziri Mkuu, Odri, akakasirika na kusimama wakati Teri yeye akiendelea na safari akampita Maya aliyekuwa anacheza na Odri akaongoza moja kwa moja mpaka nje maana hakutaka ndugu yake Adrian ajue kama anamfuata Maya na hata Adrian hakutaka Teri ajue kama anamfuata Maya

"Lela fursa ndo hiyo ndugu changamka" Hathra alimwambia mwenzake huyo alipogeuka na kutazama nyuma

"Fanya hivyo Lela" Verda nae alisisitiza, Lela akawatazama marafiki zake hao kwa uwoga wakamkonyeza na kumsukuma sukuma, wakimuhimiza aende, akainuka na kwenda kumfuata mwanamfalme Adrian aliyekuwa anarudi baada ya kushindwa kufika kwa Maya aliyekwisha kuchukuliwa na Odri

"mtukufu mwanamfalme tunaweza tukacheza wote mimi nawewe?" alimwuliza

"Lela, bila shaka" Adrian alimjibu mwanadada huyo akamshika mabega kijana huyo na kuanza kucheza nae taratibu huku akishikwa kiuno chake, akijihisi yupo pepo nyingine na siyo duniani tena lakini kabla kucheza hakujanoga Lela alishikwa bega alipogeuka akamwona mwanadada asiyemfahamu, hakuwa mwingine ila ni Merita mtoto wa Waziri mmojawapo katika baraza la mawaziri la mfalme Bono ambae ni rafiki wa utotoni wa mwanamfalme Adrian, Lela akatikisa kichwa na kumwachia Adrian, akirudi nyuma kiunyonge na kwa aibu, mwanadada huyo akajimilikisha mabega ya Adriani akimshika begani kwa mkono mmoja na kifuani kwa mkono mwingine huku Adrian akimshika kiunoni, mwanadada huyo

akamlalia Adrian kifuani wakati wakicheza

Lela alirudi kwa wenzake akiwa amekunja sura, Verda aliangua kicheko kikali akimcheka mwenzake huyo

"unacheka nini sasa Verda kipi kinachokuchekesha sasa?"
"si wewe hapo Lela yaani hata hujamfaidi mwanamfalme Adrian anatokea mrembo mwingine anakufukuza hivihivi nawewe unaondoka kiboya boya, ningekuwa mimi ningemgomea ningesema haondoki mtu hapa kudadadeki tunabanana hapahapa" Verda alijisifu

"mh unaongea tu wewe huwezi wapi unamjua yule dada mtoto wa waziri yule siyo mwenzako wala siyo mjakazi tu kama sisi ingawa na sisi tunavimba kwa sababu tunafanya kazi kwa mfalme" Hathra alimtetea Lela

"mimi unanijua unanisikia, simwogopi mtu yaani hata awe mtoto wa nani haiwezekani eti umenikuta nacheza na mtu kama vile unanichomoa thubutuuu!!"

"aah wapi mbona kwa huyo mwanamfalme Piso unayempenda umeshindwa kwenda si bora hata mimi nimemshika mwanamfalme Adrian, wewe vipi umeshikwa na huyo mwanamfalme Piso au maneno mengi tu ilimradi umeongea nawewe umeonekana, nenda pale kamshike uone na Sethi akiwepo" Lela alikasirika

"basi jamani msije mkaanza kupigana bure saa hizi yaishe, ngoja namimi nikawinde mawindo yangu nje kwa mwanamfalme Teri kipenzi cha roho yangu" Hathra aliongea akiinuka kwenye meza aliyokuwa amekaa na wenzake hao wawili, Verda na Lela akiwaacha hawaongei wamenuniana, yeye akaelekea nje kwenda kumtafuta mwanamfalme Teri aliyetoka

Muziki uliendelea kutumbuiza, wageni wakiserebuka kwa muziki huo wa taratibu uliowaliwaza huku wengine wakiendelea kupata chakula na vinywaji vya kila aina, chakula chenyewe hakikuwa cha mchezo mchezo, vyakula vizuri vya kila aina na vinywaji vya kila aina, unajihudumia tu mwenyewe au unamwita muhudumu akuhudumie

Maya alikuwa akicheza na kijana Odri na mita chache nyuma yao alikuwa mwanamfalme Adrian na mwanadada Merita wakicheza lakini Adrian macho yake yote yalikuwa kwa Maya, alikuwa akicheza na Merita kama amelazimishwa tu

"Adrian hujanimimisi?"
"nimekumisi sana Merita"
"uso wako na unachoniambia havifanani halafu mbona unatazama tazama sana kule?"

"hamna, namtazama tu Teri nimeona ametoka sijui ameenda wapi"

"mh siyo kwamba kuna mtu unamtazama tazama hivi?"

"hapana Merita, ndo umerudi masomoni moja kwa moja hautoondoka tena?"
"ndiyo Adrian, nimerudi ili tuwe wote mimi nawewe, natamani uwe wangu wa maisha"

"Merita" Adrian akacheka
"mbona unacheka Adrian
"nimefurahi tu" Adrian alijibu huku akigeuza shingo na kutazama pembeni kama kawaida kule anapocheza mwanadada Maya

"Maya umesema jina lako?" Odri alimwuliza wakati wakicheza
"ndiyo Maya"
"unapenda mwanaume wa aina gani katika maisha yako?"

"kwanini unaniuliza hivyo?"
"nimekosea kukuuliza?"
"hapana, mimi napenda mwanaume tu atakaenipenda kwa dhati na muaminifu basi"
"vipi mimi sijakidhi vigezo hivyo?"

"mh kwanini umeuliza"
"hata sijui yaani kwanini nimeuliza hivyo lakini nimeshangaa tu nimeuliza eti"

"sawa, nimechoka naomba nikakae tafadhali nimefurahi sana kucheza nawewe Odire.."
"ni Odri, O D R I"

"samahani nimesahau jina lako"
"usijali hata ila naomba jambo moja kama hutojali"

"jambo gani?" Maya aliuliza lakini kijana huyo hakujibu akasogeza midomo yake kwenye midomo ya Maya akitaka kumbusu ila Maya hakuwa tayari akaukwepesha uso wake akitaka kujichomoa kwenye mikono ya mwanaume huyo mwenye nguvu ila hakuweza akajikuta akipigwa busu la shavuni bila ridhaa yake

Odri alipofanikisha jambo lake hilo alivutwa nyuma na mkono wa kiume

"nani huyo tena?" aligeuka kutazama anayemvuta nyuma kibabe akashtukia ngumi nzito ikitua mdomoni mwake iliyomchana mdomo akacheua damu akiyumba na kuanguka mpaka chini kama mzigo wa gunia la bangi akafikia kukaa kitako, akimtazama aliyempiga hakuwa mwingine ila ni mwanamfalme Adrian aliyekuwa anahema kwa hasira huku amekunja ngumi, watu wote wageni waalikwa wakageuka wakipigwa na butwaa kutokana na tukio hilo.....

😨😨😨🙆‍♂️🙆‍♂️ sherehe imekuwa uwanja wa masumbwi jamani

*MAYA* 💃

*SEHEMU YA 25*

Kijana Odri mtoto wa Waziri alikuwa chini amekaa kitako huku amejishika shavuni akiugulia baada ya kutandikwa ngumi na mwanamfalme Adrian ambae alikuwa na hasira amesimama huku amekunja ngumi

"mtukufu mwanamfalme tafadhali" Maya alimsihi mwanamfalme asiendelee kumpiga kijana huyo huku watu wakisogea kutazama kinachoendelea

"siyo kila mwanamke ni wa kumgusa gusa ovyo ovyo heshimu utu wa mwanamke yeyote unayemuona" Adrian alimnyooshea mkono kijana huyo akimtazama kwa hasira

"samahani mtukufu mwanamfalme sitarudia tena" Odri aliongea kiunyonge

"nini tatizo?" malkia Zilpa aliuliza alipokuja na kukuta watu wanatazama tukio hilo

"huyu kijana alimbusu huyu msichana bila idhini yake ndiyo hicho" mjakazi mkuu bi Kalla alimwambia malkia ambae alimshika mtoto wake huyo wa kiume

"yaani mwanangu unajidharirisha kwa ajili ya huyu mjakazi mbele ya wageni?" alimwambia kwa sauti ya chini

"mama hata kama mjakazi lakini alichofanyiwa na yule kijana hastahili kufanyiwa mtu yeyote yule"

"jamani wageni waalikwa kulikuwa na kutoelewana kidogo tafadhali tuendelee kuburudika na kucheza muziki, kula na kunywa" bi Kalla akawaambia wageni waalikwa ambao walitikisa vichwa vyao na kurudi mahali pao kuendelea na sherehe na Maya akarudi kukaa kwenye kiti chake

"Siwezi kuvumilia kinachoendelea hapa haiwezekani ndugu yako ampige kaka yangu leo imekuwa siku mbaya kwangu na kwa mdogo wangu" Sethi alimwambia mwanamfalme Piso huku akimshika mdogo wake huyo

"hapana Sethi usifanye hivyo ni mambo ya kawaida tu" alimbembeleza na wakati huo Waziri Mkuu mzee Gonde ndiyo kwanza alikuwa anaingia ndani ya kasri la mfalme na msafara wake akiwa ametokea safarini na mkewe kumuwakilisha mfalme Bono, aliposhuka na kwenye bustani ya mfalme akakutana na bintiye aliyekuwa anashuka kwenye ngazi mbio mbio akiwa na nduguye Odri huku nyuma mwanamfalme Piso akiwa anamfuata nyuma nyuma

"baba!"
"Sethi binti yangu"
"tuondoke baba hapanifai tena"
"kwanini Sethi?"
"Odri amepigwa na mwanamfalme Adrian"
"kwa kosa gani?"
"hajafanya kosa lolote"
"ipo hivi ilikuwa ni bahati mbaya tu Adrian ali...." Piso alitaka kuzungumza kumuombea msamaha ndugu yake lakini Sethi akamnyamazisha kwa kidole asiendelee kuzungumza chochote

Wakati huo huo mwanamfalme Adrian aliitwa na baba yake mfalme chumbani wazungumze wawili tu wakati sherehe zikiendelea

"ndiyo nidhamu niliyokufundisha ya kupigana mbele yangu na mbele ya wageni Adrian?" aliulizwa huku akiwa amepiga magoti mbele ya baba yake huyo

"samahani baba nilishindwa kuvumilia unyanyasaji dhidi ya mwanamke"

"ni nani kwako yule mwanamke ni mchumba wako au?"
"ni mjakazi Tu"
"mjakazi ndiyo akufanye ufanye jambo la kipumbavu mbele yangu?"

"samahani baba nimekosea"
"sijakulea ufanye ujinga kama ule askari mchukueni mkamning'inize kwenye mti, kichwa chini miguu juu"

"sawa mtukufu mfalme" askari walijibu wakimchukua mzima mzima safari hii hawakumbeba kistaarabu ila walimbeba kama watuhumiwa wengine kutokana na amri ya mfalme wakipitia mlango wa nyuma wageni wasijue kinachoendelea

Askari hao walimpeleka mwanamfalme Adrian mpaka kwenye mti mkubwa na kumfunga kama wakimning'iniza ikiwa kichwa chini miguu juu ikiamriwa hivyo aning'inizwe kama popo mpaka kesho asubuhi

"huyu binti msipoangalia atatuchafulia kasri zima inaonekana kama mtoto wako Adrian anaanza kumpenda penda Zilpa, dalili ya mvua ni mawingu" bibi aliongea yaani mama mzazi wa malkia Zilpa

"haiwezekani jambo kama hilo mwanangu ampende mjakazi na likitokea sitaruhusu hata kjdogo"

"subiri tuone siku bado zipo" bi Jane aliongea akitikisa kichwa wakati huohuo Waziri Mkuu aliingia ukumbini na kupokelewa na malkia Zilpa huku Sethi akiwa hajakubali tena kuingia ndani ya kasri na mdogo wake Odri wakiwa wamebaki kwenye gari la baba yao nje wakibembelezwa na mwanamfalme Piso, mpenziwe

Upande mwingine bi Kalla alimtoa mwanadada Maya kwenye sherehe na kumtaka aende akapumzike ili kumuepushia lawama, Maya hakusita akarudi kwenye nyumba yao ya wajakazi na kuvua nguo zote alizovaa kwa ajili ya sherehe

"Maya!"
"abee dada"
"kuwa makini wakati mwingine"
"halikuwa kosa langu dada"
"lakini wewe ndo chanzo cha yote haya"
"samahani dada" Maya aliitikia na muda huohuo wakasikia mlango unagongwa, bi Kalla akaufuata na kuufungua akashtuka alipomwona mwanamfalme Teri mlangoni akitabasamu

"mtukufu mwanamfalme??!!"
"naweza kuzungumza na Maya kwa dakika chache?" aliulizwa bi Kalla akamtazama Maya ndani ambae alitikisa kichwa kumruhusu kijana huyo aingie ndani

"bila shaka mtukufu mwanamfalme" bi Kalla alimruhusu mwanamfalme aingie lakini yeye akataka kutoka ila Teri akamshika mkono kumzuia mwanamamama huyo asitoke abaki tu wakati akizungumza na Maya kwa sababu hakutaka ahisiwe vibaya kama kuna kitu anachotaka kufanya na Maya, bi Kalla akabaki mlangoni akiishangaa tabia ya kijana huyo ambayo imeanza kubadilika ghafla

"upo sawa Maya?"
"nipo sawa mtukufu mwanamfalme" Maya alisimama akiinamisha kichwa chake

"kwanini umetoka sasa kwenye sherehe?"
"ni..."
"ni mimi mtukufu mwanamfalme ndo niliyemshauri aje kupumzika huku kutokana na mambo yaliyotokea" bi Kalla alimsaidia Maya kujibu

"angebaki tu kwenye sherehe lile kosa siyo lake hata mimi ningekuwa ndiye yeye Adrian jambo lile lingetokea mbele yangu ningemtandika ngumi yule jamaa asiye na adabu na siyo ngumi tu na mateke juu"

"hapana mtukufu mwanamfalme haina shida hakunijeruhi"

"lakini aliushusha utu wako, twende Maya ukumbini sasa hivi" Teri alimyooshea mkono msichana huyo

"hapana mtukufu mwanamfalme"
"nimesema twende urudi ukumbini kabla sijakubadilikia sasa hivi" Teri aliongea, Maya kabla ya kuongea chochote akamtazama bi Kalla mlangoni ambae alitikisa kichwa akimtaka Maya asipingane na mwanamfalme

"nakuja mtukufu mwanamfalme"

"nipo mlangoni nakusubiri" Teri alijibu na kutoka nje na ni kweli akasimama mlangoni akimsubiri Maya ambae baada ya dakika kumi alitoka na akashtuka alipomkuta mwanamfalme Teri amesimama nje anamsubiri na siyo yeye tu, aliyeshtuka sana ni bi Kalla akishindwa kuelewa kwanini Teri anajali namna hii

Mwanamfalme Teri alimnyooshea mkono Maya ambae aliushika mkono wa kijana huyo kiuwoga uwoga wakaanza kuelekea ndani ya kasri akiwa amemshika mkono, Maya akiwa amejawa wasiwasi na siyo alishikwa mkono tu, alipokaa Maya ndipo hapohapo alipokaa mwanamfalme Teri

"Zilpa!!" bi Jane alimtikisa binti yake yaani malkia ambae alikuwa anaongea na malkia mwenzake wa nchi ya KUSINI na mke wa Waziri Mkuu akimwomba radhi wakati sherehe ikiendelea kama kawaida

"nini mama jamani mimi naongea mambo ya muhimu hapa?"
"ona mjukuu wangu kule na kale kasichana tena kajakazi amekarudisha tena amekashika mkono" alimwambia malkia ambae alitazama na kuona mtoto wake Teri akikaa kwenye viti vya wageni waalikwa huku amemshika mkono Maya ambae alitoka, amemrudisha tena, malkia Zilpa akashikwa na hasira

"wa kwanza Adrian na sasa Teri wana shida gani hawa watoto wangu?"
"usipokuwa makini Zilpa utaleta aibu ndani ya kasri, mtimue huyo msichana haraka sana ndani ya kasri, kabla hayajakukuta yaliyonikuta mimi kwa kijana wangu wa kwanza" malkia wa KUSINI alimshauri malkia Zilpa ambae alitikisa kichwa kukubaliana na ushauri huo wa mwanamama mwenzake.....

Inaendelea
*MAYA*💃

*SEHEMU YA 26----30*

Mwanadada Maya alikuwa amekaa meza moja na mwanamfalme Teri safari hii akiwa ametulia kimya wakati sherehe ikiendelea ndani ya kasri hilo la mfalme

Wajakazi wenzake, Hathra, Lela na Verda bado walikuwa hawana amani nae hasa Hathra ambae anampenda sana mwanamfalme Teri

Bibi Jane hakuweza kuvumilia kumwona mtoto wake amekaa na kijakazi tu, mtu asiye wa hadhi yake akaamua kunyanyuka yeye mwenyewe kwenye kiti chake ili aende akamtoe mjukuu wake huyo pale kwenye meza aliyokaa na mwanadada Maya

"mama unaenda wapi?" malkia Zilpa alimwuliza mama yake huyo

"naenda kuzungumza na Teri"

"mh kwanini ujipe tabu hivyo mwache"

"acha nikazungumze nae mimi bibi yake" aliinuka bibi huyo kwa mwendo wa taratibu askari wakimfuata nyuma kuangalia usalama wake asije akaanguka lakini akawazuia wasimfuate fuate akidai yeye siyo mzee sana kiasi cha kushikiliwa na kufuatwa fuatwa lakini kiuhalisia alikuwa ni mzee haswa

"Adrian yupo wapi?" malkia alimwuliza kijana wake Piso

"amekwenda na baba huko juu ghorofani kwahiyo lolote linaweza kutokea maana amefuatana na askari kadhaa"

"jamani anaenda kumwadhibu tena mtoto wangu jamani" malkia aliingiwa wasiwasi akiinuka na kuondoka kwenda kumtafuta mtoto wake Adrian lakini akakutana na mumewe mfalme akiwa anarudi na askari

"unamkimbilia mtoto wako?"

"ndiyo tafadhali mume wangu mtukufu usimpe tena adhabu bado mgonjwa" malkia alimshika mumewe ambae wala hakumjibu kitu akampita tu na kuendelea na safari yake, malkia Zilpa ambae nyuma alifuatwa na mjakazi mkuu bi Kalla walitembea na kutoka mpaka upande wa pili wa kasri nje kulipokuwa na mti mkubwa sana wa miaka mingi zaidi ya mia mbili ambao ni hazina kubwa na urithi na ukumbusho wa vizazi na vizazi, akamkuta mtoto wake Adrian akiwa amening'inizwa kichwa chini miguu juu akiwa chini ya ulinzi mkali

"mama"
"Adrian mwanangu jamani"

"usijali nipo sawa mama nitatoka tu hapa, baba yupo sahihi sikupaswa kufanya kitu kama kile mbele yake na mbele ya wageni"

"hapana imetosha, adhabu kama hii sitaivumilia tena" malkia Zilpa aligeuka kurudi ndani ya kasri lengo likiwa akazungumze na mumewe ili asiendelee kumuadhibu mtoto wao Adrian kwa staili hiyo lakini kwa bahati mbaya akakuta mumewe mfalme Bono ana mazungumzo ya faragha na mgeni wake mfalme wa KUSINI hivyo hakuruhusiwa kuingia kwenye chumba cha mumewe mfalme cha kujisomea

Bi Jane aliendelea kutembea taratibu mpaka akafika kwenye meza aliyokaa mjukuu wake mwanamfalme Teri lengo likiwa ni kumtoa mjukuu wake huyo asikae na wasichana wasio wa hadhi yake hasa mwanadada Maya,

"bibi" Teri alimwona bibi yake akija akasimama na Maya akasimama na kumshika bimkubwa huyo akitaka kumpa msaada wa kumshika

"niachie we msichana usithubutu kunishika unanichafua" bimkubwa huyo alikuwa mkali kwa Maya

"bibi njoo ukae hapa ujumuike nasi"

"siwezi kukaa hapa na hawa wasichana wasio na hadhi, twende ukakae kule Teri wewe ni mwanamfalme huoni kama unatutia aibu kukaa mahali popote tena na wasichana wasio na hadhi yako, mabinti wa mawaziri hujawaona kule mpaka unakaa huku na wajakazi?"

"bibi lakini si bado nipo ndani ya kasri na hao wajakazi si wapo humu humu wanatuhudumia kuna shida gani?"

"nimesema kakae kule mimi ndiye bibi yako naelewa nini namaanisha" bibi alikuwa mkali, mpaka watu wakageuka na kutazama kinachoendelea,

"usijisikie vibaya Maya" Teri alimshika mwanadada huyo mikono na kutabasamu kisha akamshika bibi yake huyo mgongoni ili waondoke, bi Jane akageuka na kumkata jicho kali mwanadada Maya aliyekuwa amesimama akitazama tu chini

"hawa hawajui tu tungeamua kuwafanya baya lolote si tungefanya wanatuchukuliaje sisi wakati tupo hapa kuwasaidia wao na walituleta wenyewe wala hatukujileta wala kuomba kazi humu?" Zasha aliongea kwa kunong'ona akiwa amemmaindi sana yule bibi

"oooooppppsss!" Maya alishusha pumzi ndefu akikosa cha kuzungumza wakakaa na mwenzake Zasha wakiendelea kula chakula na kunywa vinywaji wakati mwanamfalme Teri alipoondolewa na bibi yake eneo hilo,

"Maya!" Zasha alimtikisa
"Zasha!"
"nakuhurumia sana kuwa makini rafiki yangu" Zasha alimwambia Maya ambaye alimtazama tu na kutikisa kichwa akikosa cha kuzungumza mbele ya rafiki yake huyo

Sherehe iliendelea mpaka ikaisha ndani ya kasri la mfalme wageni jioni wakaanza kuondoka mmoja baada ya mwingine, muda wote huo mwanamfalme Adrian alikuwa anaitumikia adhabu yake ya kuning'inia kwenye mti kutoka kwa baba yake mfalme

Wajakazi wote wa kasri la mfalme baada ya sherehe kuisha bila hata kueleweka imeishaje ishaje maana mwanamfalme mmoja Adrian hakuonekana tena, walirudi kwenye nyumba yao ya wajakazi kubadili mavazi (magauni) yao mazuri kwa ajili ya sherehe na wakavaa mengine na kutoka kuendelea na majukumu yao usiku ukiwa umeingia tayari maana wale wajakazi wageni kutoka kwa mawaziri waliondoka na mabosi wao hao

Maya kama kawaida muda wote ukitaka umpate alipo kuwa wewe mtafute tu mwanadada Zasha na pembeni yake utampata Maya

"Maya!" aliitwa na bi Kalla
"abee dada?"
"fuatana nami" alimwambia akatikisa kichwa akiwa amelishikilia gauni lake refu na pana la kijakazi wakaenda mpaka ndani ya kasri sebuleni akashtuka alipomwona malkia Zilpa na mama yake bi Jane wamekaa wakimsubiri, alipofika akainamisha kichwa chake (salamu ya heshima)

Malkia akamtazama msichana huyo tangu juu mpaka chini na bi Jane vivyo hivyo

"ulikuja na nini humu ndani ya kasri?"
"sijaja na kitu mtukufu malkia"

"ooh vizuri nilifikiri umekuja na chochote nilikuwa nakupima tu ili nikwambie kusanya vitu vyako uende sasa kama haukuja na chochote basi jikusanye mwenyewe uende na hakikisha siri za ndank ya kasri hazitoki nje maana utauwawa"

"mtukufu malkia usimfukuze huyu ni binti mzu.."
"usiingilie maamuzi yangu Kalla" bi Kalla alikatizwa alipojaribu kumtetea Maya

"samahani mtukufu malkia" bi Kalla aliitikia kiunyonge na kumtazama Maya kisha akashusha pumzi ndefu akimshika mwanadada huyo mkono na kuanza kumtoa nje taratibu baada ya amri hiyo kutoka kwa malkia wakati huohuo mwanamfalme Teri alikuwa anakuja upande huu huu walipo mama yake na bibi yake akapishana na Maya na mjakazi mkuu bi Kalla lakini alipowapita akasimama na kugeuka

"Maya!"
"abee mtukufu mwanamfalme" Maya aligeuka na kusimama kichwa akiinamisha chini
"upo sawa?"
"nipo sawa mtukufu"

"basi vizuri" alitikisa kichwa akitaka kuondoka ila akawageukia tu na Maya na bi Kalla wakapiga hatua kuendelea na safari

"samahani Maya nimeshindwa kufanya chochote kwa ajili yako, amri ya malkia ikitoka imetoka hakuna wa kupinga"
"usijali dada, asante kwa ukarimu wako" alitabasamu na bi Kalla akarudisha tabasamu

"nini kinaendelea?" mara wakasikia sauti nyuma yao wakashtuka na kugeuka wakamwona mwanamfalme Teri kumbe alikuwa akiwafuata nyuma nyuma

"hakuna kitu mtukufu mwanamfalme" bi Kalla alijibu, kijana huyo akamkamata Maya mkono kwa nguvu na kuanza kuondoka nae

"mtukufu mwanamfalme tafadhali niachie" Maya alilalamika, lakini hakujibiwa kitu akamrudisha mpaka mbele ya mama na bibi yake

"bila shaka niwewe mama uliyemfukuza kazi Maya, vipi unaweza ukanipa sababu kuu tatu tu za kumfukuza ndani ya kasri?" alimwuliza mama yake huyo ambaye alitazamana na bibi yake...

MAYA 💃

SEHEMU YA 27

"Teri nini dhumuni la swali lako sijakuelewa?" malkia Zilpa alimwuliza kijana wake huyo wakati huo huo bi Kalla mjakazi mkuu aliyekuwa ameachwa nyuma nyuma alikuja mbiombio

"samahani mtukufu malkia" bi Kalla aliomba radhi

"kwanini umemfukuza Maya ndani ya kasri mama nataka kujua"
"nani aliyekuambia kama nimemfukuza Maya?"
"ni mimi hapa mtukuf.."

"hapana ni mimi hapa mwenyewe mtukufu malkia" Maya alimkatisha kauli bi Kalla ambae alivutia upande wake ili kumnusuru Maya na adhabu kutoka kwa mwanamama huyo

"hakuna aliyeniambia mama nimesikia mwenyewe kwa masikio yangu"

"Teri una mambo mengi ya kufanya"
"lakini huyu ni mpishi wangu anayenitengenezea chakula kizuri ninachokipenda sana, siyo haki kabisa kumfukuza bila mimi kujua kosa lake" Teri alimwambia mama yake ambae aligeuka kimya kimya na kumtazama mama yake bi Jane ambae alitikisa kichwa kumaanisha amuache tu Maya asimtimue

"sawa lakini wakati mwingine akisababisha vurugu ya aina yoyote ile sitamsamehe"
"asante mama" Mwanamfalme Teri alimbusu mama yake kwenye paji la uso na kumgeukia Maya akamtazama machoni ambae alitazama chini kwa aibu

"asante mtukufu" bi Kalla ilibidi ashukuru kwa niaba ya Maya, Teri akawapita na kuondoka nao bi Kalla na Maya wakainama mbele ya malkia na mama yake wakageuka na kuanza kuondoka taratibu

"Zilpa mbona simuelewi huyu mjukuu wangu kwanini amng'ang'anie huyu msichana namna hii?"
"hata mimi sielewi mama kabisa lakini nipo makini kutazama kila hatua ya huyu binti"

"hakikisha unafanya hivyo maana sitaruhusu aibu yoyote itupate kutoka kwa mjukuu wangu yeyote yule, wao ni uzao wa kifalme na wanatakiwa waoe mabinti wafalme wenye hadhi kama wao"

"hilo niachie mimi mama" malkia Zilpa alimjibu mama yake ambae alitikisa kichwa huku wakitazamana

Muda wote huo mwanadada Hathra hakuwa mbali akifuatilia nyendo za Maya, akiwa anamchunga mjakazi mwenzake huyo asije akamnyang'anya tonge mdomoni, tonge ambalo hata yeye mwenyewe bado hajalimeza bado, si jingine ila ni mwanamfalme Teri, kijana anayempenda sana

"unatazama nini Hathra?" Lela alimwuliza
"nahisi Maya alikuwa anagombezwa na malkia"
"kwa sababu ya yaliyotokea kwenye sherehe au?"
"inawezekana kabisa"
"nachotamani ni kumwona anafukuzwa ndani ya kasri"

"na ndicho kitakachotokea maana mimi sitaruhusu aendelee kuishi humu"

"hata mimi pia sitaruhusu hilo kamwe lazima tufanye jambo" Lela na Hathra waliongea wakitazamana na kutikisa vichwa vyao

Mwanamfalme Piso alikuwa chumbani kwake usiku huo, mchumba wake Sethi akiwa amesharejea kwao baada ya sherehe kuisha, alibaki amekaa kitandani akiwaza na kuwazua hasa akikumbuka kitendo cha udanganyifu aliofanyiwa na Sethi kwenye mapishi waliyoandaliwa baba na mama yake, akasimama na kuanza kutembea tembea huku akijikuna kichwa na ndevu zake chache kidevuni

"leo nimekubali uwongo wa Sethi kwa wazazi wangu lakini vipi kesho na keshokutwa nitakapokuwa nimemuoa nitakubali kudanganywa kila siku, na vipi atabadilika pale nitakapohitaji mapishi yake itakuwaje, hapana lazima jambo hili nihakikishe linakaa sawa" Piso aliongea peke yake akatoka chumbani haraka haraka na kuanza kupita kwenye korido lakini alipokunja kona kwa bahati mbaya akagongana uso kwa uso, kiifua kwa kifua na mwanadada Maya ambae alikuwa amebeba glasi ya juisi anampelekea mwanamfalme Teri aliyemuagiza akiwa kama mjakazi wake binafsi, glasi ikaanguka na kupasuka pasuka vipande vipande juisi ikamwagika yote chini Maya akabaki amejiziba mdomo kwa hofu

"samahani mtukufu mwanamfalme"
"wakati mwingine uwe makini" Piso alimjibu akitaka kumpita kuendelea na safari yake na ndipo Maya akaona damu ikitoka mguuni kwa kijana huyo ambae hakugundua kumbe kipande cha chupa kilichotoka kwenye glasi kilimchana kidogo mguuni

"mtukufu mwanamfalme damu inakutoka samahani" alimsimamisha kijana huyo ambae alijitazama mguuni

"haina shida ni kidogo sana wala sijaumia"
"hapana subiri nikuhudumie kwanza"

"nimekwambia jeraha ni dogo nina safari yangu" Piso alikuwa mkali lakini Maya hakutaka kumsikiliza kijana huyo akamshika mabega kwa nguvu na kumkalisha chini kiulazima mwanamfalme Piso akajikuta anakaa kitako mzima mzima sakafuni bila kupenda

Maya akachana kitambaa chake cha mapishi (epron) na kukigawa vipande viwili, kimoja akamfutia mwanamfalme damu akimsafisha jeraha lake hilo mguuni na kingine akamfunga kwenye jeraha lake mguuni, Piso akimtazama tu mwanadada huyo anavyohangaika

Chumbani kwa mwanamfalme Teri alikuwa amekaa kitandani kwake akisubiri juisi aliyomwagiza mjakazi Maya ili anywe alale maana hakupanga kula chakula cha usiku leo akiwa bado ameshashiba vinono vya kwenye sherehe

"huyu Maya mbona anakawia sana?" alijiuliza mwenyewe akainuka kitandani na kutoka chumbani taratibu na ndipo alipomwona nduguye Piso akiwa amekaa chini sakafuni kitako na msichana Maya, Teri akashtushwa na mikao hiyo akataka kusogea kujua kinachoendelea lakini akasita na kutazama vizuri akamwona Piso akifungwa fungwa kitambaa mguuni akabaki ametulia mlangoni akichungulia kwa umakini akitazama tukio hilo ambalo hakupendezwa nalo, akashusha pumzi ndefu na kurejea ndani taratibu akakaa kitako kitandani kwake huku akijisikia hasira, alipokaa hakutulia akainuka tena na kurudi mlangoni akichungulia na kukuta Piso akiinuka akiwa amedhafungwa kitambaa mguuni, Maya akiutazama

mguu wake huo, Teri akarejea tena ndani

"wakati mwingine uwe makini" Piso aliongea

"samahani mtukufu mwanamfalme" Maya akainamisha uso wake, kijana huyo akageuka na kuondoka zake akimwacha Maya anaanza kuokota vipande vya glasi aliyoivunja na kupasafisha pale chini

Piso alipofika mbele kidogo akageuka kumtazama Maya kisha akajitazama mguu wake na kuendelea na safari yake mpaka chumbani kwa baba yake mfalme ambapo aliruhusiwa na askari anayesimama kwenye mlango wa chumba hicho akaingia mpaka ndani

"baba!"
"Piso"
"naomba ruhusa"
"wapi saa hizi?"
"kwa Waziri Mkuu"
"kumuona Sethi?"
"ndiyo baba"
"mwambie hakuhitaji kunidanganya ili awe mkwe wangu, nimemsamehe kwa ajili yako tu"

"baba unamaanisha?" Piso alishtushwa na kauli ya baba yake "nenda" alimwonyesha ishara ya kumruhusu kwa mkono, Piso akataka kuuliza vizuri lakini hakuruhusiwa kusema neno tena akainamisha kichwa chake na kutoka taratibu chumbani kwa baba yake akiwa na maswali mengi kichwani

"ina maana baba ameshagundua kuwa siyo Sethi aliyepika kile chakula, na amegunduaje??" Piso alijiuliza maswali yasiyo na majibu...

MAYA 💃

SEHEMU YA 28

Mwanamfalme Teri alikuwa amekaa kitandani kwake akisubiri juisi kutoka kwa Maya ambae alimwona akiwa na nduguye Piso kitendo ambacho wala hakikumfurahisha kijana huyo

"mtukufu mwanamfalme" mlango uligongwa kijana huyo akasimama na kwenda kuufungua, siyo kawaida yake kwenda kupokea vitu mlangoni, kwa kawaida huwa anamruhusu mjakazi aingie akishaingia mpaka chumbani, anatengewa na kuondoka lakini leo hakutaka Maya aingie chumbani kwake amtengee kama ilivyo kawaida ya wajakazi, alitoka kumpokea

"nipe" alimwomba Maya ambae alishangazwa na kitendo hicho cha mwanamfalme Teri kuja mwenyewe kupokea vitu mlangoni

"mtukufu mwanamfalme lakini si ninakuteng..."

"nimekwambia nipe sitaki mazungumzo mazungumzo" Teri alikuwa mkali mpaka Maya akashtuka na kuingiwa wasiwasi akampa kijana huyo glasi ya juisi na kuondoka kiunyonge uso ukiwa chini akiwa amejawa wasiwasi, Teri akamtazama Maya kisha akaingia ndani kwake na kuufunga mlango kwa kuubamiza akaweka glasi pembeni na kujitupa kitandani akilala chali, akitazama juu kwenye dari, akashusha pumzi ndefu ya hasira na hakuishia hapo akasimama na kwenda dirishani kwake akatazama chini maana chumba chake kilikuwa ghorofani akamwona Maya anaelekea bustanini akiwa ametoka ndani ya kasri na kilichomuudhi zaidi ni alipomwona mwanadada huyo amesimamishwa na askari mmoja

aliyekuwa anamwongelesha huku akimchekea chekea, Teri akaufuata mlango haraka haraka akatoka ili aende nje lakini kwa bahati mbaya kumbe mlangoni alikuwepo mjakazi Hathra anasikiliza kinachoendelea chumbani kwa mwanamfalme Teri mlango ulipofunguliwa tu kwa sababu alikuwa ameuegemea akajikuta anaaangukia ndani mzima mzima

"uuuwiii samahani mtukufu mwanamfalme" aliongea akiwa chini amekaa kitako
"ulikuwa unafanya nini mlangoni kwangu?"

"nilikuwa nina..." alishikwa na kigugumizi akikosa cha kujibu, Teri akamtazama tu na kutoka akiendelea na safari yake ya kuelekea bustanini...

Upande mwingine kwa ruhusa ya baba yake, mwanamfalme Piso usiku huohuo anawasili kwenye jumba la Waziri Mkuu kwa ajili ya kuonana na mchumba wake Sethi anapokelewa na askari getini ambao wanamsindikiza mpaka ndani anapokelewa na mama mzazi wa Sethi na kukaribishwa ndani ya jumba hilo na Sethi aliyekuwa chumbani kwake anaitwa na kuja kumuona mchumba wake huyo

"karibu Piso mbona usiku usiku?"

"nimetamani tu kukuona na kuzungumza nawewe Sethi"
"ooh vizuri"
"haya ngoja niwaache muzungumze basi" mama Sethi aliongea akitaka kuinuka
"hapana tutaongelea nje bustanini mama wala usijali" Piso alimjibu mama huyo akatoka na mwanadada huyo mpaka nje kwenye bustani wakawa wanatembea pamoja wawili

"Unataka kuzungumza nini au yaleyale yaliyokwisha pita?"
"hapana ila baba amejua tayari"
"amejua nini?"
"kuhusu chakula cha siku ile"
"amejuaje jamani?" Sethi alishtuka akibaki amejiziba mdomo

"sijui ni nani aliyemwambia"
"yule msichana Maya ni mbaya kumbe jamani?"
"sina uhakika kama ni yeye aliyemwambia na hawezi kuzungumza na baba chochote yule msichana bila shaka lazima atakuwa mtu mwingine"

"umeamua kumtetea yule Maya kama Adrian?"
"simtetei ila nasema ukweli"
"ukweli wa wapi yule Maya inaonekana ana nyota sana ya kutetewa na kupendwa eeh mpaka amesababisha mdogo wangu Odri apigwe adharirishwe mbele ya watu na sasa anatetewa mbele yangu?"

"Sethi unaongea vitu gani?"

"naongea hivyo hivyo unavyosikia"

"aaasssh!" mara ghafla Piso alilalamika maumivu huku akijitazama mguuni,
"kulikoni?"
"nimejichoma na mwiba" alijibu akinyanyua mguu wake ambao ni kweli mwiba ulizama katikati ya unyayo wa mguu wake ukiwa umetoka kutoka kwenye mti wa maua ulio kwenye bustani hiyo, damu zikimtoka

"mh madamu damu tena jamani usinionyeshe bwana Piso aah" Sethi aliona kinyaa akamwita askari mmoja aliyekuwa upande wa bustanini akamwambia awaite wenzake wawili waje kusaidiana kumbeba mwanamfalme, lakini Piso akakataa na kutembea mwenyewe mpaka ndani akiwa ameshikwa mkono na Sethi, daktari wa familia hiyo akaitwa na kuanza kumpatia huduma ya kwanza ya haraka ili kumwokoa mguu wake usije ukavimba kutokana na sumu inayosemekana kuwa kwenye mti huo wa maua

Piso wakati anahudumiwa na daktari alibaki anamtazama Sethi ambae alikuwa pembeni akimtazama tu, daktari akashika kitambaa ili amfunge jeraha lakini Piso akamzuia

"Sethi nifunge hapa" alimpa kitambaa mwanadada huyo kwa makusudi akitaka tu kumpima
"mh jamani Piso daktari si yupo unataka nishike mavidonda tena jamani kha" Sethi alikataa katakata kushika jeraha la mpenziwe huyo ambae alitabasamu tu lakini kimoyomoyo kitendo hicho kilimkasirisha sana cha mkewe huyo mtarajiwa kulionea jeraha lake kinyaa

Wakati daktari alipokuwa akimfunga jeraha hilo mguuni kwenye mguu wa kulia, Piso akajikuta badala ya kumwona daktari akifunga jeraha alishangaa kumuona Maya akiwa anamfunga na jeraha hili la mguu wa kulia huku akimwangalia kwa tabasamu akiwa amevaa mavazi ya kidaktari, yaani yule daktari alikuwa ni Maya

"Maya???!!!" Piso alimshangaa
"pole mtukufu mwanamfalme" Maya alimwitikia Piso ambae alibaki kinywa wazi

"Piso umesemaje?" sauti ya Sethi ilimshtua akakurupuka, kumbr yalikuwa ni mawazo yake tu, wala hakukuwa na Maya eneo hilo, daktari huyo wa kike ndiye aliyekuwa anamshughulikia mguu wake

"vipi unasikia maumivu mtukufu mwanamfalme?" daktari alimwuliza baada ya kusikia Piso akiongea

"yaah kidogo tu" Piso alizuga ili Sethi asigundue kama alilitaja jina la Maya, ajue tu alikuwa analalamika maumivu kumbe wala hakuna maumivu aliyoyasikia kiasi cha kupiga mayowe na kwa bahati nzuri Sethi hakusikia vizuri alichokizungumza Piso, hasa jina Maya alimkatisha....

Upande wa pili ndani ya kasri la mfalme Bono kijana Adrian alikuwa ananing'inia kwenye mti akiwa ameshapitiwa na usingizi lakini amejivuta mpaka kwenye tawi moja amelishika huku akiuchapa usingizi ambao kama akijisahau tu anarudi tena chini lakini siyo chini kabisa kwa sababu kuna kamba imemshikilia miguuni

Akiwa usingizini alijikuta anaanguka kwenda chini na alipofungua macho haikuwa uwongo ni kweli alijiiikuta anaanguka chini mpaka kwenye manyasi yaliyokuwa chini ya mti huo kama mzigo puuuuh!!

"ndo kufunguana gani nyie wajinga mnashindwa kuniamsha kwanza nikashuka mwenyewe kistaarabu mpaka mniangushe au mmesahau kuwa mimi ni bosi wenu?" alilalamika akiwa chini amelala kifudi fudi tumbo na uso vikitazama chini ardhini

"samahani mtukufu mwanamfalme" askari mmoja alimuomba radhi kwa niaba ya wenzake

"samahani ya nini mnajisahau kama mimi ni mwanamfalme?"
"una amri ya mwisho kuliko mimi?" akasikia mtu anamjibu alipogeuka akamwona baba yake mfalme amesimama anamtazama

"baba??!" alikuwa mpole
"nenda kalale, kesho kuna ugeni wako, kuna mwanamke nimemuandaa kwa ajili yako"
"mwanamke baba??" Adrian aliuliza lakini baba yake hakumjibu kitu akaondoka taratibu na mlinzi wake mkuu jenerali Fidel, Adrian akabaki ametoa macho baada ya kusikia habari hizo...

MAYA💃

SEHEMU YA 29

Kulikucha mapema asubuhi, siku mpya ikiingia ndani ya nchi ya TSALA na ndani ya kasri la mfalme Bono, wajakazi kama kawaida wakiwa wameamka mapema asubuhi na kuanza shughuli zao za kuhakikisha kila kitu kipo sawa ndani ya kasri chini ya usimamizi wa bi Kalla, Maya nae akiwa miongoni mwao

"mbona leo heka heka nyingi sana ndani ya kasri kupita kawaida?" Hathra alimwuliza mwenzake Verda wakati wakihenya kufanya usafi na maandalizi makubwa ya kutosha kupita kawaida

"nahisi mchumba wa mwanamfalme Adrian nimesikia sikia kuwa anakuja ila usije ukaropoka mimi nilimsikia tu dada Kalla akiongea na malkia Zilpa ambae alimwambia ahakikishe kuwa kila kitu kipo sawa maana msichana mwenyewe ni bintimfalme anakuja na wazazi wake wawili yaani malkia na mfalme"

"duh kazi ipo basi Verda"
"tena ipo sana, hasa kwa Lela mwenzetu, afute tu ndoto yake ya kumpata mwanamfalme Adrian"

"mnazungumza nini mbona nawasikia mnanitaja taja?" Lela aliwauliza, Hathra na Verda wakatazamana na kucheka kicheko cha umbea, Lela akabaki anawashangaa tu marafiki zake hao

"subiri tu Lela usiwe na haraka utaona tu kinachotokea leo mama" Verda alimwambia Lela ambae aliwapita tu na kuendelea na safari zake na wakati huo huo Maya nae alipita na kwenda upande aliopo rafiki yake wa karibu, Zasha wakiwa kwenye ngazi za kupandishia ghorofa ya juu wakiendelea kufanya usafi mapema asubuhi, lakini hawakujua kuwa upande mmoja alisimama mwanamfalme Piso na upande mwingine alisimama mwanamfalme Teri wakiwa hawajaonana na wote wakimtazama Maya

"sijawahi kuhisi kitu moyoni mwangu kwa mwanamke kama ninavyohisi kwa huyu mjakazi" Piso aliongea kimoyomoyo huku akishusha pumzi ndefu

"Maya kwanini najikuta nakosa usingizi kwa ajili yako, sielewi inakuwaje nampenda mjakazi mtu asiye wa hadhi yangu, nahisi nimekutamani tu kwa ajili ya uzuri wako na tabia zako lakini sipo tayari kukuharibia maisha Maya najaribu kujizuia nitajaribu kila siku" Teri nae aliongea kimoyomoyo akishusha pumzi ndefu

"Maya!!" Piso ilibidi aite na Maya akageuka juu na kumuona mwanamfalme huyo akaacha kazi aliyokuwa anaifanya na kumfuata kijana huyo juu, Teri ikabidi ajifiche asionekane wakati huo akina Hathra, Verda, Lela na wengine ambao hawampendi Maya tangu aingie ndani ya kasri waligeuka kutazamana wakitamani kujua alichoitiwa Maya

"naam mtukufu mwanamfalme" aliinamisha uso wake chini akiwa amelishikilia gauni lake refu

"nimekuita kukushukuru kwa ulichonifanyia jana kwa huduma uliyonipa nilipoumia"

"ulishanishukuru mtukufu"
"nilikushukuru juu juu waweza kwenda"
"asante mtukufu" Maya aligeuka na kupiga hatua kuondoka

"Maya!" aliitwa tena akageuka
"abee mtukufu?"
"basi nenda tu" Piso alitabasamu Maya akatikisa kichwa na kuondoka taratibu

Teri alipomwona Maya anaondoka akachungulia tena kumtazama wakati akishuka kwenye ngazi na bila kujua kumbe upande huo huo aliokuwepo alikuwa akija mama na bibi yake wameongozana, bibi huyo akiwa ameshikwa na mtoto wake huyo akimfanyisha mazoezi ya asubuhi asubuhi wakiwa wanaelekea nje bustanini

"subiri" bibi aliongea
"nini mama"
"mbona Teri kazubaa sana anashangaa nini inaonekana kama anamtazama mtu"

"mh nani tena anayetazamwa namna hiyo na mjukuu wako mama?" malkia Zilpa aliuliza wote yeye na mama yake wakitazama anachokishangaa mwanamfalme Teri wakakuta kumbe alikuwa anamtazama mwanadada Maya mjakazi

"yule mjakazi tena ndiye anayemzubaisha mjukuu wangu namna ile Zilpa?" bibi aliongea kwa kuchukia, malkia Zilpa akashusha pumzi ndefu na kumfuata Teri kimya kimya, kijana huyo akiwa hana hili wala lile akimtazama Maya kwa chini aliyekuwa ameshuka anaendelea na usafi kama kawaida baada ya kutoka kuzungumza na mwanamfalme Piso aliyemuita

"unatazama nini hicho mpaka kinywa unaacha wazi mwanangu mpendwa??" alimnong'oneza sikioni, Teri akashtuka

"oooh mama nilikuwa naangalia angalia tu teh teh" alishikwa na kigugumizi akicheka cheka tu mbele ya mama yake

"Maya siyo?"
"hapana mama"
"niambie tu mimi ni mama yako Teri usiponishirikisha mimi utamshirikisha nani kama siyo mimi Teri?"

"kuna kitu nakiona kwa Maya mama"
"kitu gani tena mwanangu?"

"mkarimu, mpole, mchapakazi yaani jinsi tu alivyo alivyo naona kama ni msichana fulani hivi tofauti na wengine niliowahi kuwaona"

"ohoo kumbe ndiyo hicho tu?"
"ndiyo mama" Teri aliitikia mama yake akatikisa kichwa akitabasamu na kumtazama Maya chini huku uso wake ukimbadilika

"nadhani umeshaanza kufanikiwa kuuteka moyo wa mtoto wangu wewe msichana mjakazi lakini mimi kama mama sitaruhusu jambo kama hilo litokee" aliongea kimoyomoyo mwanamama huyo

Ni asubuhi hiyo hiyo maandalizi yakiwa yameshafanyika ugeni mkubwa unaingia kutoka nchi ya mbali, nchi rafiki mkubwa wa nchi ya TSALA, malkia wa nchi hiyo akiwa amefuatana na bintiye Nadia wanaingia ndani ya kasri na msafara wao wenye ulinzi mkali na kushuka wanapokelewa na malkia Zilpa mwenyewe na ujumbe wa mawaziri kadhaa wachache mpaka ndani ya kasri, kikao kinafanyika kifupi cha ukaribisho kati ya malkia huyo ambae ndiye mwenye utawala wa nchi anayotoka, akiwa amerithi utawala kutoka kwa hayati baba yake, mwanamama huyo akiwa mwanamke wa kwanza kushika utawala wa kifalme kwenye nchi anayotoka akiwa ndiye binti wa kwanza na mtoto pekee wa kike kwa hayati baba yake na mtoto

wa pekee

Mwanamfalme Adrian alifuatwa bustanini akiitwa kwa ajili ya kwenda kutambulishwa kwa ugeni huo akakutana na malkia huyo na bintiye waliokaa na mama yake baada ya kikao wakipata kifungua kinywa kwenye meza kuu

"huyu ndiye mwanangu miongoni mwa wale pacha wengine wawili niliokutambulisha, huyu anaitwa Adrian ndo wa mwisho kutoka tumboni mwangu" malkia Zilpa alimtambulisha kwa mwanamama mwenzake huyo

"hatimae familia zetu zitaunganishwa sasa na watoto wetu" malkia huyo alitabasamu akitikisa kichwa kumtazama Adrian ambae wala hakutabasamu alikuwa amekunja uso tu huku akiangaliwa na msichana mrembo sana, bintimfalme Nadia

"Adrian mnaweza kwenda bustanini kuzungumza na mwenzio" malkia Zilpa alimwambia kijana wake huyo ambae aliinuka kishingo upande na kuongozana na binti mfalme huyo mgeni mpaka bustanini wakakaa kimya, Adrian akiwa hazungumzi chochote

"naitwa Nadia!" alimpa mkono
"naitwa Adrian"

"nimefurahi kukufahamu Adrian nasikia tuliwahi onana tukiwa watoto wadogo sana"

"mimi pia" Adrian alijibu akijionea kero tu kukaa na msichana maana siyo kawaida yake

Wakati huohuo alikatiza mwanadada Maya akielekea upande wa bwawa la samaki kwenda kupeleka chakula cha samaki, Maya akiwa amebeba chombo chenye chakula hicho cha samaki kwa bahati mbaya alipokanyaga nyasi kutokana na kiatu alichovaa na unyevu unyevu wa asubuhi (ikiwa ni majira ya baridi) akajikuta anateleza na kutaka kuanguka lakini haikuchukua hata sekunde mwanamfalme Adrian alikuwa amemuwahi na kumdaka kabla hajaanguka kwenda chini na kwa bahati mbaya alikuwa amemshika kiuno

"upo sawa?" alimwuliza wakitazamana usoni, bintimfalme Nadia alikasirishwa sana na kitendo hicho na kumbe muda huohuo mwanamfalme Teri alikuwa akija bustanini akashtuka alipomwona ndugu yake Adrian amemshika Maya kiuno.....

MAYA 💃

SEHEMU YA 30

"Upo sawa Maya?"
"nipo sawa mtukufu mwanamfalme asante" Maya aliitikia akitikisa kichwa na kujitoa mikononi mwa Adrian aliyekuwa amemshika kiuno kwa bahati mbaya

"samahani" Adrian alijigundua kuwa amefanya kosa kumshika kiuno mwanadada huyo akautoa mkono wake taratibu na kugeuka kurudi alipokaa na Nadia lakini shingo akageuka akimtazama Maya alivyokuwa anaondoka mpaka alipotokomea akijisahau kuwa kuna Nadia anamtazama pembeni

"anaitwa nani yule msichana?"
"Maya, ni msichana mkarimu na mpole sana mpaka wewe mwenyewe utampenda Nadia"

"natamani nimjue zaidi" Nadia alitabasamu akimtazama Adrian lakini tabasamu lake halikuwa la kutoka moyoni lilikuwa la usoni tu kumzuga Adrian, moyoni alichukia kuona mwanaume anayempenda anampa sifa msichana mwingine tena mbele yake, na kilichomkasirisha zaidi ni kitendo cha Adrian kumshika kiuno mwanadada huyo muda ule

Teri alibaki amesimama tu kwa mbali akiwa amejishika kiuno huku akishusha pumzi ndefu na ndipo mkono ukamgusa begani kutokea nyuma, akashtuka na kugeuka akakutana na mwanadada mjakazi Hathra akitabasamu

"mtukufu mwanamfalme!"

"umenishtua Hathra"
"samahani mwanamfalme"
"bila samahani usijali"
"nilikuwa ninaaa..." Hathra alisita kuendelea kuzungumza akabaki anatazama chini kwa aibu

"una nini Hathra?"
"kwenye sherehe ya kuzaliwa kwako sikufanikiwa kutoa zawadi kwahiyo nilitamani nikupatie zawadi sasa ya siku yako ya kuzaliwa kama hutojali mtukufu mwanamfalme"

"ohooo haina shida ipo wapi hiyo zawadi"
"hii hapa!" Hathra alitoa bangili ndogo ya mkononi akaushika mkono na kuanza kumvalisha mwanamfalme Teri

"waaooh asante sana Hathra kwa zawadi nzuri sana"

"sina zawadi kubwa naomba uipokee hiyo tu"

"usijali ni kubwa sana hii yani thamani yake ni kubwa mno" Teri alimkumbatia mwanadada huyo ambae badala ya kukumbatiwa kidogo tu, alimng'ang'ania mwanamfalme akiwa hataki kutoka kifuani mwake, Teri alipojaribu kujichomoa kwenye kumbatio la mwanadada huyo akajikuta anashindwa kufanya hivyo

"nakupenda sana mwanamfalme Adrian nakupenda sana natamani uwe wangu wa maisha, mimi niwe malkia wako nawewe uwe mfalme wangu mmmywaaaaa mnywaaaa" Hathra aliongea huku akimbusu Teri mdomoni akiwa ameshikwa kiuno na kijana huyo wakitazamana usoni karibu kabisa na bwawa la kuogelea la mfalme'

Kumbe yalikuwa ni mawazo yake tu, alipofumbua macho alijikuta amesimama mwenyewe tu akiwa amenyoosha mikono kama amemkumbatia mtu, kumbe Teri alishamtoa kifuani mwake zamani na ameondoka zake, Lela na Verda wakiwa wamesimama kwa mbali wanamcheka ikabidi awafuate akiwa amekasirika akiwa anatamani mwanamfalme Teri angeendelea kumkumbatia zaidi lakini alichoambulia ni kumbatio tu la juu

Akawafuata wenzake hao waliokuwa wanamcheka

"vipi mwanamfalme Teri amepokea zawadi yako?" Verda alimwuliza

"amepokea na kunikumbatia amenikumbatia tena akaniambia oooooh nakupenda sana Hathra natamani uwe mke wangu siku moja asante kwa zawadi nzuri sana, siyo kubwa lakini ni ya thamani sana, wewe ni mrembo sana sana Hathra kupita wote" Hathra aliwaambia wenzake kwa ishara ya kujikumbatia mikono yake mwenyewe huku akiwarembulia, Verda na Lela wakatazamana na kuangua kicheko

"yaani wewe unaona sisi watoto wa kutudanganya wakati tumeona kapokea hicho kibangili chako akakukumbatia tu kidogo juu juu na kuondoka zake akakuacha umesimama tu kama sanamu umeinua mikono kama mgonjwa hahaha" Lela alimcheka

"kwani mnadhani mkiniamini au msiponiamini mnanipunguzia nini si mpambane na hali zenu, mmewapa zawadi hao Adrian na Piso wakapokea kama mimi na ndiyo kwanza wengine wachumba zao wamekuja kasoro mimi tu Teri yupo mwenyewe na nitahakikisha kuwa namweka mkononi, kila mtu apambane na hali yake"

"makubwa!!" Verda aliongea

"nini kinaendelea hapa?" wakaulizwa walipotazama wakamwona bi Kalla, kila mmoja akaondoka kimya kimya kuendelea na kazi yake baada ya kukutwa wakiwa wanapiga 'domo' badala ya kuendelea na kazi zao

Maya alisimama pembeni kabisa mwa bwawa la samaki la mfalme na kuanza kuchota chakula na kuwamwagia samaki hao wenye rangi nzuri za kupendeza, samaki tu wa urembo walionunuliwa kutoka katika falme tofauti tofauti

Aliendelea kutupa chakula huku akiwatazama samaki hao wa kupendeza na akataka kuinuka (maana alichuchumaa) ili ahamie upande mwingine wa bwawa hilo lakini kwa bahati mbaya alikuwa amelikanyaga gauni lake refu akajikuta anaangukia kwenye bwawa lakini mkono ukamdaka kabla hajatumbukia akawa anayatazama maji kabisa, mkono huo ukamvuta tena nyuma, alipotazama mtu huyo aliyemzuia kwa mkono ili asitumbukie ndani ya maji akakuta ni mwanamfalme Teri

"siku nyingi uwe makini Maya"
"asante mtukufu mwanamfalme"
"naweza kukusaidi kazi hii?"

"asante nitaifanya tu mwenyewe"
"namimi natamani niifanye"
"mwanamfalme hapana"
"lete Maya" Teri alikivuta chombo na Maya nae akakivuta upande wake akiwa hataki kumpa kijana huyo mpaka baadhi ya chakula kikammwagikia Teri kwenye nguo yake

"uuwiii samahani mtukufu mwanamfalme" Maya aliiweka ndoo hiyo pembeni na kulishika joho la kifalme la Teri akalishika gauni lake refu na kuanza kulitumia kufuta chakula cha samaki kilichomdondokea kijana huyo kwenye nguo yake

Teri alibaki akimtazama Maya wakati akimfuta futa uchafu kwenye nguo yake

"kila nikutazamapo nahisi kukosa amani ndani ya moyo wangu Maya, sijui kwanini lakini moyo unaniambia kabisa kuwa unakuhitaji, ila mbona wewe siyo msichana wa hadhi yangu kabisa itawezekanaje??!!" Teri alijiuliza kimoyo moyo wakati akimtazama Maya usoni

Ni wakati huohuo Adrian alikuwa akija na bintimfalme Nadia upande wa kwenye bwawa la samaki akimtembeza mwanadada huyo mgeni na ndipo alipimshuhudia ndugu na pacha wake Teri akiwa amesimama na Maya kandokando ya bwawa la samaki akiwa amemshika msichana huyo mikono akimng'ang'aniza akimlazimisha kumbusu mdomoni na Maya alionekana akiwa hataki anajitahidi kwa uwezo wake wote kutaka kujichomoa kwenye mikono ya kijana huyo mwanamfalme

Adrian uvumilivu ulimshinda akamwacha Nadia aliyekuwa ameongozana nae akawafuata Maya na Teri na alipofika wala hakuuliza akamshika Teri na kumsukuma pacha wake huyo bwawani akatumbukia kwenye maji

"mtukufu mwanamfalme!!" Maya alimshangaa sana kijana huyo akabaki ametoa macho mpaka Nadia akabaki amejishika kichwa, kinywa wazi

"mbona unanisukuma Adrian" Teri alishangaa akiwa kwenye maji anahangaika hangaika

"siku nyingine uwe na adabu kwa wasichana!" Adrian aliongea kwa hasira akimnyooshea kidole nduguye huyo wote wakimshangaa...

MWISHO WA SEASON 01,

Usisahau season two imetoka ina vipande 30 pia,

31-60 tsh 1000 tu ndio mwisho.